ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake

37.Mhe. Ashura Sharif Ali - Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Nne – Tarehe 22 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 163

Utambulisho wa Rais – BLW

Mhe. Omar Ali Shehe – Aliuliza:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar ni sehemu ya Muhimili wa Kutunga Sheria (*Legislative Council*).

Katika jengo la Baraza la Wawakilishi ni kitu gani kinachoashiria kwamba Rais wa Zanzibar ni sehemu ya Baraza hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 163 kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, toleo la 2010 ibara ya 63 (1) inasema kutakuwa na Baraza la Kutunga Sheria ambalo litajulikana kama Baraza la Wawakilishi litakalokuwa na sehemu mbili, Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wawakilishi kwa upande wa pili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, uhusiano mkubwa baina ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Baraza la Wawakilishi upo katika utendaji wa baadhi ya majukumu, ambapo Katiba inaelekeza kuwa majukumu hayo lazima yatekelezwe na pande zote mbili, yaani Baraza la Wawakilishi na Rais wa Zanzibar. Kwa mfano; katika kutekeleza jukumu lake la kutunga Sheria, Baraza la Wawakilishi haliwezi kutekeleza jukumu hilo peke yake kwani Katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 78 (3) kinaeleza kuwa Mswada wa Sheria uliopitishwa na Baraza la Wawakilishi utahitaji kibali cha Rais ili kuwa Sheria.

Vile vile, Katiba imempa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mamlaka ya kuitisha Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Wawakilishi mara baada ya Uchaguzi Mkuu kumalizika, kama inavyoelezwa katika Katiba na Kanuni za Baraza.

Aidha Katiba pia imempa uwezo Mhe. Rais wa Zanzibar kulivunja Baraza la Wawakilishi linapomaliza muda wake wa miaka mitano au wakati wowote endapo litatokezea jambo lolote kati ya mambo yaliyotajwa kwenye kifungu cha 91 (2) cha Katiba yetu ya Zanzibar.

Pamoja na kazi hizo, Rais anaweza wakati wowote kulihutubia Baraza la Wawakilishi atakapoona kuna haja ya kufanya hivyo (kifungu cha 84 cha Katiba)

Mhe. Naibu Spika, alama nyengine ambazo ni kielelezo cha uhusiano ni pamoja na Picha ya Mhe. Rais wa Zanzibar ndani ya Jengo la Baraza la Wawakilishi, Bendera ya Zanzibar na Mhuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao ni alama kubwa ya kiitifaki za nchi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kumuulia Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Uzoefu unaonesha kuwa nchi nyingi za Jumuia ya Madola kwenye mabunge yake zinakuwa na sehemu maalum za kuonekana zinawekwa alama ya Rais ikiwa kama ni bendera katika chombo kama kile. Kwa kuwa Zanzibar mbali ya Nembo ya Serikali pamoja na Bendara ya Serikali na kwamba Rais wetu anayo Nembo yake ya Rais.

Sasa kwa nini ili kumaanisha kwamba Rais ni sehemu ya chombo hiki kwa nini hatufanyi kama yanavyofanya mabunge mengine kuweka Nembo ya Rais katika Baraza hili.

Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ushauri alioutoa ni mzuri na tutashauriana na watendaji wa Baraza hili la Wawakilishi pamoja na wataalamu wa sheria kama jambo hilo linaweza kufanyika katika Baraza letu hili.

Kwa kweli jambo hili naona ni ushauri mzuri na tunaupokea na tutaufanyiakazi. *(Makofi)*

Nam. 98

Manaibu Masheha Kufanya Kazi za Masheha

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) – Aliuliza:-

Kwa kawaida Masheha husaidiana na Naibu Masheha katika kutekeleza kazi zao kwenye ngazi ya Shehia.

(a) Je, kuna sheria gani ambayo inawapa mamlaka Naibu Masheha kufanya kazi za Usheha wakati Sheha anapokuwa ana dharura.

(b) Kama hakuna, je, serikali ina mpango gani wa kuweka sheria hiyo, ili kuondosha usumbufu kwa hao Manaibu Masheha.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sasa hakuna sheria inayomtambua au kumpa mamlaka Naibu Sheha kufanya kazi za Usheha wakati Sheha anapokuwa na dharura. Sheria Nam. 1 ya 1998 kifungu 18(1) imetoa uwezo kuundaa Baraza la Ushauri la Sheha linaloteuliwa na Sheha kwa kushauriana na Mkuu wa Wilaya, ambalo lina jukumu la kumshauri Sheha kuhusiana na mambo mbali mbali yanayojitokeza katika Shehia husika.

Hata hivyo taratibu za serikali zinaruhusu wadhifa wowote kukaimiwa iwapo mamlaka ya uteuzi itathibitisha nafasi hiyo kukaimiwa. Taratibu hizi zimefuata misingi ya Katiba kifungu Nam. 131.

(b) Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupitia Idara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inajiandaa kupendekeza marekebisho ya baadhi ya vifungu vya Sheria ya Mamlaka za Mikoa Nam. 1 ya 1998 kwa kuingizwa vifungu vya kuwepo nafasi ya Naibu Sheha na Katibu wa Shehia, ili kuimarisha utoaji wa huduma bora za serikali kwa wananchi wake kwa urahisi na pia kuondoa huo usumbufu anaoupata Naibu Sheha. Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali hili ameeleza kuwa katika kuteua Baraza lake la Ushauri, yaani Sheha baada ya kuchaguliwa hushirikiana na Mkuu wa Wilaya na kweli hii ndio hali ilivyo.

Lakini kwa bahati mbaya Masheha wengi wanapochagua Baraza hili la Ushauri mara nyingi hulichagua kisiasa kutoka chama anachotoka yule Sheha, wakati Sheha amechaguliwa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wote.

Je, Mhe. Waziri haoni kuwa ipo haja hivi sasa kwenye uteuzi wa Wajumbe wa Baraza hili la Ushauri la Sheha kutafutiwa utaratibu mwengine na wakati tumo kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili wapatikane watu watakaoweza kuwatumikia wananchi ipasavyo zaidi ya vile anavyochagua yeye.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, nafikiri atakubaliana na mimi kwamba Sheha ndiye Kiongozi au Governor wa Mtaa, sasa yeye kupata wasaidizi lazima apate wasaidizi wa mtaa, ili watawale vizuri na wala hawezi kutawala peke yake, kwa ajili ya kushauriana pamoja na kupanga.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba labda kulikuwa na kutokufahamu taratibu zinazotumika, lakini kama Sheha lazima apate washauri wazuri wanaoweza kuongoza.

Sasa kama hilo halitendeki ipasavyo, basi tutalifuatilia tuone kwamba washauri anaopata, kwa sababu Mkuu wa Wilaya kazi yake ni kuthibitisha tu, lakini watawala lazima watoke kwenye eneo lile. Kwa maana hiyo, ushauri wako tumeupokea na hasa kwa mustakbali tuliokuwa nao tuone kuwa kila eneo linapata watawala wazuri. *(Makofi)*

Nam. 12

Kupunguza Umaskini katika Ukanda wa Mashariki mwa Kisiwa cha Pemba

Mhe. Viwe Khamis Abdalla – Aliuliza:-

Ukanda wa Mashariki mwa Kisiwa cha Pemba ni eneo la ukame na umaskini wa kipato. Serikali imetangaza nia ya kushughulikia tatizo hilo Kitaifa chini ya Ufadhili wa Mfuko wa *Millennium*. Hatua ya serikali kwa awamu ya kwanza ni kuweka kituo cha Radio Micheweni.

(a) Je, hii radio inasaidia vipi kuwapatia mahitaji yao yote ya lazima?

(b) Watu wa Micheweni wamepatiwa mtambo wa Radio ambao husikika mpaka Wingwi na sehemu ndogo ya Mchanga mdogo. Je, watu wa mjini Kiuyu, Kangagani, Mjini Ole, Vitongoji, Pujini na Chambani na wao kwa awamu ya kwanza wamepangiwa nini?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, nchi nyingi duniani katika hatua za kuondosha umasikini uliokithiri, zimetia saini kufikia utekelezaji wa malengo ya Maendeleo ya Millenia. Hatua hiyo imeonekana itasaidia pia katika kusukuma mbele maendeleo kwa kuanzisha Vijiji vya Millenia.

Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi za Afrika zilizotia saini makubaliano hayo pamoja na kuanzisha Vijiji vya Millenia. Nchi nyengine na Vijiji vyao ni Kijiji cha Sauri – Kenya, Mbola – Tabora Tanzania, Potau – Senegal, Pampaida – Nageria, Tibi na Mwandama – Malawi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuangalia vigezo mbali mbali vya takwimu za umasikini, Wilaya ya Micheweni – Pemba ndio inayoongoza kwa umasikini wa kipato na ule usiokuwa wa kipato kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Katika jitihada za kupunguza umasikini uliokithiri Zanzibar, serikali iliomba Jumuia za Kimataifa kufanya utafiti na kuanzishwa Kijiji cha Millenia huko Micheweni Pemba.

Maombi hayo yalikubaliwa na hatimaye hatua za utekelezaji zikaanza. *Programs* za upelekaji maji safi na salama, kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Sawinga, ufugaji wa mbuzi wa maziwa, ujenzi wa skuli, ujenzi wa kituo cha afya, upelekaji umeme na ujenzi wa kituo cha Redio ni miongoni mwa *programs* zilizoanzishwa ili kutekeleza kuwepo kwa Kijiji cha Millenia. *Programs* zote hizo zilizoanzishwa kwa pamoja imeonekana zitasaidia kupunguza umasikini katika Wilaya ya Micheweni. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Redio Jamii ilioko Micheweni Pemba kazi yake kubwa ni kutoa elimu kwa jamii ya Micheweni, ili kujua na kufahamu shughuli mbali mbali kama zitatekelezwa ndani ya jamii na uzuri na ahtari

zake. Redio Jamii haitoi msaada wala mahitaji yoyote ya lazima kwa wananchi, bali inatoa mwamko na kuiarifu jamii nini cha kufanya ndani ya jamii ya Micheweni kwa faida ya watu wa micheweni.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, kamba Redio Jamii ya Micheweni ni moja ya *program* maalum ya uwanzishwaji wa Kijiji cha Millenia ndani ya Wilaya ya Micheweni na wala haihusiani na maeneo ya wilaya nyengine. Maeneo aliyoyataja Mhe. Mwakilishi yako katika Wilaya ya Wete, Chake-Chake na mengine Wilaya ya Mkoani. Hata hivyo lengo la *program* hii ni kuwapunguzia makali ya umasikini wananchi wa Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake, pia nikiri kwamba kweli kumeanzishwa mambo mbali mbali kama vile mradi wa ufugaji mbuzi, Redio Jamii ya Micheweni. Kwa kweli nikiri kwamba Redio Jamii ya Micheweni inafanyakazi kuliko vile matarajio ambavyo yalikuwa yametarajiwa.

Lakini sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, akubaliane na mimi kwamba katika kuwapunguzia umasikini wananchi wa Micheweni ni kweli kuwa kumeanzishwa mradi wa ufugaji wa mbuzi.

Hivi atakubaliana na mimi kwamba kumpatia mwananchi wa Micheweni mbuzi mmoja kwa ajili ya kuanza ufugaji haiwezi kumpunguzia umasikini na hivi sasa wakati umefika wa kuwaongezea wananchi kipato, ili kuwapa mbuzi ambao wanaweza kufuga na kuweza kujipunguzia umasikini.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alinituma mimi pamoja na Mawaziri wenzangu Mhe. Waziri wa Uvuvi na Mifugo na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwa ajili ya kuitembelea Wilaya ya Micheweni na tuone nini serikali inaweza kufanya katika suala zima la kuwaondolea umasikini Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, anayoyasema Mhe. Mjumbe ni kweli tumegundua, akinamama zaidi ya 20 wanafuga kuku 10 na hivi hatuwezi kuwaondoshea umasikini kwa kiwango hicho cha ufugaji.

Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba kunahitaji msukumo mkubwa katika Wilaya ya Micheweni. Vile vile tumegundua akinamama 15 wanalima kwenye nusu eka na wala hawezi kuwaondoshea umasikini wenzetu wa Wilaya ya Micheweni. Hata hivyo, tumegundua elimu ya kilimo na ufugaji haipo ndani ya Wilaya ya Micheweni.

Kwa manaa hiyo, kuna haja kubwa sana ya kutoa taaluma hizo, ili wananchi wa Micheweni waweze kufaidika na kuondoka na umasikini wao. Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba katika bajeti hii nitaiangalia zaidi Wilaya ya Micheweni na maeneo mengine, ili hatua za makusudi ziweze kuchukuliwa katika suala zima la kuondoa umasikini kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa redio iliwekwa kwa lengo maalum ya kupunguza umasikini katika eneo la Micheweni. Je, tokea kuanzishwa kwa redio hiyo serikali imeshafanya utafiti au tathmini kujua ni kiwango gani cha mafanikio cha kuwekwa redio hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba *program* yote ya jumla ilikuwa ni suala zima la kuondosha au kupunguza umasikini kwa Wilaya ya Micheweni. Redio haina uhusiano wa moja kwa moja na kuondosha umasikini, isipokuwa redio tuliiweka pale, ili wananchi waweze kuelewa na kuelimishwa juu ya mambo fulani fulani ambayo wakiyafanya yataweza kuwasaidia katika hatua na jitihada zao za kupunguza makali ya umasikini.

Kwa hivyo, nataka nimwambie tu kwamba utafiti unakuja, ili kuweza kujua hasa ni kiwango gani cha umasikini wa wananchi wa Micheweni kimeweza kufikiwa.

Nam. 203

Kupitishwa Sheria ya Maadili ya Utumishi wa Umma

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Ili kutimiza maendeleo na malengo ya utawala bora, nchi nyingi duniani zimepitisha Sheria ya Maadili ya Utumishi wa Umma, ambapo baadhi ya watumishi wa umma kwa ngazi tofauti hutakiwa kutangaza mali zao kila baada ya kipindi fulani au mara tu anapoteuliwa kushika nafasi ya juu ya utumishi wa

umma. Pamoja na sababu nyengine sheria kama hiyo hukusudia kuondosha mianya ya wizi, rushwa na baadhi ya watumishi kujilimbikizia mali na utajiri zaidi.

(a) Je, kwa hapa Zanzibar sheria kama hiyo ipo, kama haipo ni kwa nini?

(b) Viwango vya mishahara ya Zanzibar vinajuilikana, lakini ni kwa nini wafanyakazi wenye viwango sawa vya elimu (*same academic level*) wanaonekana tofauti kwa taasisi moja au nyengine kwa kipato na umasikini?

(c) Ni lini hapa Zanzibar, serikali itawaamuru viongozi na wafanyakazi kutangaza mali zao?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny: Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora) – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 203 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya msingi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliunda Wizara ya Katiba na Utawala Bora katika awamu ya sita. Miongoni mwa majukumu yake makubwa wizara hiyo, ilijipangia kutekeleza au kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi. Mhe. Naibu Spika, azma hiyo bado ipo katika awamu hii ya saba chini ya Wizara mpya ya Katiba na Sheria.

Wizara katika kuitekeleza azma hiyo, ilianza na mchakato mzima wa kuandaa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka hiyo kwa lengo la kuipa meno iweze kusimamia utekelezaji wa kazi zake ikiwemo ya kusimamia Maadili ya Viongozi. Suala la Watumishi wa Umma wa ngazi za juu kutakiwa kutangaza mali zao limezingatiwa. Kwa hivyo, hivi sasa rasimu ya awali ya Mswada wa Sheria hiyo imeshaandaliwa na imo katika mchakato wa kupelekwa kwa wadau mbali mbali kwa ajili ya kuitafakari, kuijadili na hatimaye kutoa maoni yao, ili iweze kuwasilishwa katika vyombo vinavyohusika na kupitishwa rasmi.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Hivi sasa Sheria ya Maadili ya Viongozi na Kuzuia Rushwa kwa Utumishi wa Umma hapa Zanzibar haipo, ila serikali imeona umuhimu wa suala hilo ndio maana ikaamua kulifanyia kazi ipasavyo.

(b) Serikali imeliona tatizo la kuwepo tofauti ya mishahara kwa wafanyakazi wenye viwango sawa vya elimu (*same academic level*) na tayari imeshalifanyia kazi, ili kufikia uwiano uliosawa katika ya taasisi moja na nyengine kimapato kwa wafanyakazi wenye viwango sawa kielimu na uzoefu wa kazi.

(c) Mara tu Mswada wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi utakapopitishwa katika Baraza hili tukufu na kuwa Sheria Watumishi wa ngazi za juu na ngazi nyengine tofauti serikalini watawajibika kutangaza mali zao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Mhe. Waziri alikiri kwamba Wizara ya Katiba na Utawala Bora ilianzishwa tangu serikali ya awamu ya sita na sasa karibu miaka mitano tokea kuundwa kwa wizara.

(a) Sasa ni kwa nini hadi hii leo Sheria hii ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi bado haijapitishwa Baraza la Wawakilishi, wakati zipo sheria ndani ya miezi mitatu huangaliwa na kumalizwa?

(b) Kwa kuwa Katiba sasa imeanzisha Tume ya Utumishi wa Umma na kabla ya hapo Mahakama, Baraza la Wawakilishi pamoja na Vikosi walikuwa na tume zao ambazo zilikuwa zikizingatia maslahi yao. Je, sasa kwa mujibu wa Katiba na muundo mpya maslahi ya sehemu hizi tatu yatazingatiwa vipi wakati muamuzi ni Tume ya Utumishi wa Umma?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny: Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Naibu Spika, naomba radhi kama sikumpata vizuri, kwa sababu Mhe. Mjumbe haikaribii *microphone* anazungumza mbali. Kwa hivyo, nitajaribu kuzungumza pale nilipompata na pale ambapo sikumpata vizuri anaweza kuniuliza tena.

(a) Kuhusu suala la wizara kuchelewa kuipitisha sheria hii imeanza awamu iliyopita na hivi sasa ni awamu hii. Kwa kweli suala hili si jepesi, yaani suala hili lina fitina, majungu. Kwa hivyo, lazima tukubaliane kwa sababu sote tunajua mambo yetu hapa. Sasa *draft* zimetayarishwa na zikaja mpaka kwenye vikao vya juu zikarudi kwa ajili ya kufanyiwa kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, suala hili lazima lifanyiwe kazi, kwa mfano tunaona wenzetu Tanzania Bara mpaka leo Bungeni wanatakiwa wajieleze mpaka wanataka kupigwa faini kwamba bado hawajaeleza mali zao, suala hili si jepesi. Kwa hivyo, lazima lifanyiwe kazi pamoja na kuandaliwa vizuri, ili tutakapoanza kutekelezwa basi lisiwe na matatizo yoyote.

(b) Kuhusu Tume ya Utumishi wa Umma na hizi tume nyengine. Mhe. Naibu Spika, tayari sheria tumeshapitisha Barazani, lakini bado matayarisho katika Ofisi ya Rais ili iweze kuridhiwa na kuweza kuanza kazi, basi tutakapokamilika itakuwa hakuna matatizo kila mkondo utafuata upande wake.

Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, serikali yetu imeanzisha Utumishi wa Umma, ili kuangalia mwenendo wa wafanyakazi wetu katika kufanya kazi zetu kwa nia njema kabisa, tangu kuanza kwa serikali hii yenye sura ya umoja wa kitaifa ni mwezi wa saba sasa hivi kama sikosei, na tume hiyo imeanzishwa na wafanyakazi wetu wa Zanzibar tunawajua ni watu wanaopenda penda starehe kupiga urojo maofisini na mambo mengine.

Je, tangu kuanzishwa tume hii ni mara ngapi wamesimamiwa watumishi ili kuangaliwa mwenendo wao wa kazi?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Ni kweli kwamba ilianzishwa tume hiyo ya kudumu ya kupitia haya masuala yote ya utumishi wa umma, kwakweli ile tume imefanya kazi kubwa sana ni wataalam wazalendo wetu wenyewe wanapelekewa vitu kuthibitisha, chini ya Mzanzibari mwanamama mmoja ambae yeye ni mshauri mwelekezi anafanya kazi nzuri sana na tunatambua utendaji wake.

Kwa kweli ndio ametusaidia sana kwa mabadiliko haya ya utumishi ambayo yamefanikiwa kwa hivyo niseme kwamba hawakupita mawizarani, hiyo *document* nafikiri baada ya drafti ya kwanza walipita mawizarani hata sisi Baraza la Wawakilishi nakumbuka walitufanyia semina tokatoa maoni yetu, kwa hivyo niseme Mhe. Subeit Khamis Faki labda bahati mbaya siku hiyo hukuwepo lakini walipita wakatuhoji na tukatoa maoni yetu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa tulikubaliana suala la kuundwa kwa sheria hii lina mantiki kubwa na lina maana kubwa kwa serikali yetu, lakini suala hili kwa mujibu wa maelezo yako lilikwama kutokana na wakubwa kuwa wanaogopa fitna miongoni mwao na hiyo ilikuwa katika serikali ya awamu ya sita.

Je, suala la kuogopa fitna limo katika serikali ya awamu ya saba, na ikiwa serikali ya awamu ya saba haiogopi fitna sasa tuambieni ni lini mswada huo utaletwa ndani ya Baraza hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Omar mimi nilitoa mfano tu hiyo nilisema kwamba haya mambo yana fitna, yana majungu yana mazonge mengi sasa ili kufanywa vizuri kuepuka hayo basi twende kisayasi twende kitaalam, twende kwa nadharia nzuri, tutandike sheria nzuri, vifungu vizuri ili kila mmoja ajue anafuata wapi na anapita wapi.

Sikusema kwamba serikali hii inaogopa fitina nasema haya mambo tuyaepuke kwa sababu tunayo nafikiri utakubaliana na mimi hayo ni mambo ya kawaida katika maisha yetu tunayo.

Nam. 112

Ufaulu Mdogo wa Wanafunzi wa Zanzibar Katika Mitihani ya Taifa

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

(a) Je, ni Wilaya gani ilipata ufaulu mdogo katika mitihani ya Taifa kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita, kuanzia mwaka 2005 hadi 2010.

(b) Je, ni sababu gani za kitaalamu na kijamii zilizopelekea hali hiyo.

(c) Je, Wizara inaisaidiaje Wilaya hiyo pamoja na Wilaya nyengine ili hali hiyo isitokezee tena ili Wilaya zote ziwe na viwango vya kufaulu vinavyowiyana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 112 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Wilaya ambayo imekuwa na asilimia ndogo ya Wanafunzi waliofaulu Mtihani wa Taifa wa kidato ha Pili kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita, kuanzia 2005 hadi 2010 ni wilaya ya Kaskazini "B" Matokeo ya Mitihani ya kidato cha pili yameonesha kuwa skuli za Wilaya hiyo zimekuwa ni za mwisho kwa wastani wa Wilaya kama hivi ifuatavyo:

MWAKA	WASTANI WA ASILIMIA YA WANAFUNZI WALIOFAULU	NAFASI
2005	35.4	10/10
2006	37.2	9/10
2007	40.6	9/10
2008	39.1	10/10
2009	38.3	9/10
2010	51.7	10/10

b) Skuli za wilaya ya Kaskazini 'B' zinafanya vibaya katika mitihani kutokana na upungufu wa walimu wenye sifa ambao ni wakaazi katika wilaya hiyo na hivyo kutegemea sana walimu wanaioshi katika wilaya nyengine na kufanya kazi katika skuli zilizomo katika wilaya hiyo. Pia mwamko mdogo wa Elimu kwa wananchi, utoro wa wanafunzi kutokana na kuingia katika ajira zisizo rasmi zimechangia katika kuwafanya wanafunzi kutochukua juhudi katika masomo yao na hatimae kusababisha kufanya vibaya katika mitihani yao.

c) Wizara inazisaidia skuli zilizoko katika wilaya zote zikiwemo skuli za Wilaya ya Kaskazini 'B' ili ziweze kuinua ubora wa elimu kwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara kupitia vituo vya walimu . Pia Wizara imetoa kipaumbele katika ajira mpya za walimu kwa maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa walimu zikiwemo Skuli za Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja na Wilaya ya Micheweni kwa Pemba Wilaya hizo pia zilipewa kipaumbele katika mradi wa maandalizi kwa njia ya redio ulioitwa *"RISE"* kwa ajili ya kuwahamasisha wananchi wawapeleke watoto wao kupata Elimu ya maandalizi kama ndio msingi wa elimu bora kwa watoto. Pia Wizara imeandaa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za skuli ili waweze kuchangia katika kuwahamasisha wananchi wafahamu umuhimu wa elimu kwa maisha yao na ya watoto wao.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika kujibu suala hili Mhe. Waziri ametuonyesha takwimu kadhaa za wastani na kuonyesha kuwa wako nyuma kama suali lilivyouliza, hii ilikuwa ni wastani. Je, hakuna skuli katika wilaya hizo zilizofanya vizuri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nilichoulizwa katika suala hili ni matokeo ya jumla kiwilaya, lakini unaweza kwenda katika Wilaya hiyo hiyo ukakuta kuna skuli imefanya vizuri lakini ukitafuta wastani kwa skuli zote ndio unapata kwa hizi takwimu ambazo nimezitoa hapa.

Nam. 18

Matengenezo ya Barabara Eneo la Kijini, Matemwe

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi wa eneo la Kijini katika Jimbo la Matemwe wamekosa barabara nzuri inayopitika wakati wote, hali inayoathiri maendeleo ya wananchi hao.

Ni lini barabara hiyo itajengwa hasa katika kuitekeleza ahadi aliyoitoa Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2010 alipokuwa katika Jimbo la Matemwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inalifahamu la usumbufu wa barabara kwa kijiji cha Matemwe Kijini na lipo kwa muda mrefu, hata hivyo Wizara yangu imekuwa na utaratibu wa kuikarabati barabara hiyo kila hali inaporuhusu aidha wizara yangu imekamilisha usanifu na matarajio yetu kwamba barabara hiyo itajengwa katika mwaka huu wa fedha 2011/12 kuanzia eneo la Kiwashangwe hadi Kijini Pwani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza suala moja la nyongeza. Kwa kuwa amesema kwamba Wizara yake imekamisha usanifu na barabara hii itajengwa mapema sana ndani ya mwaka huu. Je, anakusudia kutwambia kwamba bajeti hii ya mwaka huu barabara hii imetajwa na kama imetajwa ni shilingi ngapi zimetengwa kwa ajili ya barabara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Barabara tuliyozungumzia hapa ni miongoni mwa barabara za *fider road* na barabara hii itajengwa kwa kupitia mfuko wa barabara.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Je, barabara hii itajengwa katika kiwango kipi ?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Barabara hii kilio chake kikubwa ni kuisaidia watu waweze kupita malengo ya serikali ni kujenga barabara za lami katika maeneo yote, uwezo wa serikali kwa hivi sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha kifusi lakini itakayoweza kupitika kwa mwaka mzima bila ya tatizo lolote.

Nam. 113

Uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-

Mara tu baada ya kumalizika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

(a) Kwa kuzingatia sifa na taratibu zinazostahiki kufuatwa katika uteuzi wa Majaji kama zilivyofafanuliwa katika Katiba ya Zanzibar; Je, ni sababu zipi zilizopelekea Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar kushauri kwamba uteuzi huo haufai kisheria.

(b) Je, ni chombo kipi ama kiongozi gani anaemshauri Mhe. Rais wakati wa uteuzi huo.

(c) Je, mbali na sifa hizo zilivyoelezwa Kikatiba, Je, Mhe. Rais analazimika kuhakikisha kwamba mteuliwa amekamilisha sifa zote au anaweza kwa busara zake kuteua hata kama mteuliwa hakutimiza sifa zote.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 113 kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Kifungu 94 (2) (3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa, taratibu na sifa za uteuzi wa Jaji wa Mahkama Kuu zimeelezwa kama ifuatavyo:-

1. Majaji wa Mahkama Kuu watateuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Mahkama.

2. Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahkama Kuu mpaka;

(i) Awe na Shahada ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa au Chuo cha aina hiyo;
(ii) Awe au amewahi kuwa Jaji wa Mahkama zilizofanana na Mahakama Kuu Zanzibar kwa kesi zote za jinai na madai katika Tanzania au sehemu yeyote ya Jumuiya ya Madola au Mahkama yenye Mamlaka ya Rufaa katika Mahkama hizo;
(iii) Awe ni Mwanasheria wa Zanzibar au Tanzania kwa kipindi kisichopungua miaka saba.

Hivyo Wizara haifahamu ni sababu zipi ambazo zilizopelekea Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar kuelezea kwamba uteuzi wa Majaji hao haufai kisheria.

(b) Kwa mujibu wa kifungu 94 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaeleza kuwa Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahkama.

Na kifungu cha 94(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinaeleza kuwa Majaji wa Mahkama Kuu watateuliwa na Rais kutokana na Mapendekezo ya Tume ya Utumishi ya Mahkama.

(c) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahkama Kuu mpaka awe na sifa hizo zilizoelezwa kwenye Katiba. Hivyo Mhe. Rais analazimika kikatiba kuhakikisha kwamba mteuliwa amekamilisha sifa zote.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kama ikitokezea majaji wawili wana sifa sawa hata umri wao wa kufanya kazi ni kipengele kipi cha zaidi kinachotumika ili mmoja akabakia mmoja akateuliwa.

Mhe. Waziri Katiba na Sheria: Ikiwa kuna watu wawili ambao wana sifa sawa sawa na umri sawa sawa wa kufanya kazi na ikiwa ni nafasi moja inayotakiwa, kwa hivyo kitu ambacho kitazingatiwa hapa kwanza ni nyendo zake au tabia zipi zilizo nzuri zaidi, kwa sababu jaji wa Mahakama Kuu anatakiwa ni mtu mwenye heshima, mwenye tabia nzuri na asiye pita vichochoroni mara kwa mara.

Mhe. Hija Hassan Hija: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa sifa ambazo Waziri amezitaja kwa wale majaji ambao ni miongoni mwa elimu na muda wao ni sawa ni kutokupita vichochoroni mara kwa mara, lakini Mahakama Kuu ya Zanzibar iko katika eneo la Mji Mkongwe Vuga ambao ni mji wenye vichochoro vingi sana.

a) Huoni kwamba huwezi kufika Vuga bila ya kupita vichochoroni na majaji hawa wakiwa na uwezo sawa wa kielimu, huoni kwamba majaji wetu tutawakosa.

b) Zamani walivyokuwa wakichagua watu wenye busara walikuwa wakichagua watu wenye mvi, kwa nini wasitafutwe wale watu wenye mvi ikiwa watatokea watu wenye elimu sawa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri jibu suali b) suali a) liwache.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheri: Sina uhakika kama nimemsikia vizuri, lakini ninachotaka kujibu ni kwamba Mhe. Muwakilishi ni mswahili na maana ya kichochoroni anajua, kuna mambo mengi ambayo mtu anatizamwa kabla hajawa jaji wa Mahakama Kuu. Lakini pia kuna mambo ambayo ni muhimu kuyatizama ambayo yanaweza kumpa *extra credit* ya kuwa jaji wa Mahakama Kuu.

Nam. 52

Wananchi wa Kipato cha Chini Kupatiwa Nyumba za Makaazi

Mhe. Mgeni Hassan Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya nyumba za makaazi yanaongezeka kila siku na huku wananchi wa kawaida wakishindwa kumudu gharama za ununuaji wa ardhi na gharama za ujenzi.

(a) Je, Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha wananchi hawa wanapata nyumba za makaazi.

(b) Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwapatia wananchi wa kipato cha chini nyumba za kuishi, Wizara imeweka vigezo vipi ili wananchi hawa waweze kupatiwa nyumba.

(c) Je, Wizara haioni haja ya kuwapa kipaumbele wafanyakazi wenye kipato cha chini ikiwa ni pamoja na walimu, wafanyakazi wa Wizara ya Afya na wafanyakazi wa Vikosi vya SMZ.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba, Serikali imejipanga kuwapatia wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba makaazi bora na salama. Katika kutekeleza mpango huu Serikali hivi sasa imetenga maeneo mbali mbali kama vile Binguni, Kibuteni na Chuini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kisasa za makaazi kwa upande wa Unguja, vile vile inaandaa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa upande wa Pemba.

Nyumba hizi zinatarajiwa kujengwa na wawekezaji mbali mbali wa nje na ndani ambao Serikali imefanya jitihada za kuwashajiisha. Hivi sasa tayari baadhi ya wawekezaji wamejitokeza na mazungumzo yanaendelea ili kufanikisha mpango huu wa ujenzi wa nyumba za makaazi.

(b) Serikali itaweka umuhimu wa kuwapatia wananchi wa kipato cha chini nyumba za kuishi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kila muhusika na itahakikisha nafasi ya mwanzo inatolewa kwa yule mwenye shida ya kweli ya makaazi.

(c) Serikali inatoa umuhimu wa kuwapatia makaazi wafanyakazi waliomo katika Taasisi mbali mbali za Serikali kusaidia kuinua kiwango cha maisha.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri nakumbuka mwaka jana kulimalizwa ujenzi wa *block No. 9 na Bloc No.10* na baada ya kumalizika majengo hayo Mhe. Rais mstaafu aliahidi kuwa atawaangalia vikosi vya SMZ kwa kuwapatia baadhi ya nyumba katika *mablock* hayo.

Je, zoezi hili limefanyika?.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzaibr imewakabidhi rasmi vikosi vya SMZ jumba hilo la Michezani kwa kila yule aliyeandikishwa kupewa nyumba ile.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu waziri katika makaazi ya wananchi mnakuwa mnashindwa kusogeza miundo mbinu. Je katika hayo maeneo uliyoeleza Mhe. Waziri na miundo mbinu itakuwepo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Katika maeneo ambayo yatajengwa basi tunategemea miundo mbinu nayo itakuwemo vile vile.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifutavyo:

Utaratibu uliokuwa ukiendelea hata pale tunapopata misaada Mchina (a) na (b) wengi waliopewa ni wale wenye kipato kikubwa na ambao wana uwezo wa kujenga.

a) Je, hivi sasa kumetokea marekebisho gani ili utaratibu huo uweze kurekebishwa na wale ambao hawana uwezo ndio wenye kupatiwa nyumba hizo.

b) Kwa kuwa vijana wengi wanashindwa kuoa kwa sababu hawana makaazi, Je, katika hali hoyo huoni sababu kwamba umefika wakati katika kuzuia maambukizo ya ukimwi serikali ikafanya jitihada za makusudi kwa kuwasaidia makaazi japo ya miaka miwili ili waweze kujisukuma na kuoa upesi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, si kweli kwamba wananchi wanaoishi katika majumba ya Mchina (a) na Mchina (b) wote ni wenye uwezo na waliokuwa hawana uwezo hawaishi katika nyumba hizo, nyumba hizo wanaishi watu wengine hawana uwezo na ni kweli

waliokuwa na uwezo pia wanaishi humo na kwasababu nyumba hizi zilitolewa kwa aliyeomba na kila aliyeomba alipatiwa, ni kweli nyumba hizo hazikutosha kwa kila aliyeomba. Bado wapo watu ambao wameomba na hawakupata nyumba hizo lakini si kweli kwamba nyumba hizo wanaishi watu wenye uwezo.

Suala (b) serikali sidhani kama ina jukumu la kumtafutia mtu nyumba ili aowe, kimaadili sisi wananchi hata wale masikini wanapokuwa tayari kuoa familia zao zinawasaidia au wenyewe wanajisaidia kujitafutia makazi hasa katika maeneo ya vijijini, lakini serikali haijabeba jukumu hilo na sidhani kama inaweza kubeba jukumu la kumtafutia mtu nyumba ili aowe, wapo waliokuwa hawajaoa wanajitunza na wanamaadili mazuri na hawana matatizo hayo, na wapo walioowa ambao hawana maadili mazuri wamebeba ukimwi na wanaueneza katika nchi yetu. Kwa hivyo hilo ndio jibu ambalo nimependa niseme.

Nam. 40

Madakrati wa Kigeni Kutofahamu Kiswahili/Kiingereza

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali zetu za Zanzibar ikiwemo hospitali ya Chake-Chake mara nyingi hutegemea Madaktari wa Kigeni kwa mfano kutoka Cuba, na kwa kuwa baada ya kufanya uchunguzi imebainika kuwa baadhi ya Madaktari hao hawafahamu Kiswahili wala kiingereza jambo ambalo linaleta usumbufu kwa wagonjwa na hata kwa madaktari wenzao.

Kwanini Serikali isiwe na mpango wa kuwapatia madaktari hao mafunzo ya lugha za kiingereza/kiswahili kabla kuanza katika katika hospitali zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 40 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kawaida madaktari wote wa kigeni wanaokuja kutoka nchi za nje wanajua kiingereza hata kama si kizuri. Inavyotakiwa wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa waambatanishwe na wafanyakazi/madaktari wazalendo. Kwa vile madaktari hao wanakuja kwa vipindi maalum ambavyo ni vifupi kwa ajili ya kutoa huduma, si rahisi kwa Wizara kumega muda wao wa kutoa huduma kwa ajili ya kuwafundisha lugha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba anijibu swali langu dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kifungu Nam. 3 cha sheria Nam. 9 ya mwaka 2010 ya Katiba ya Zanzibar ilifanya mabadiliko na kuitangaza Zanzibar kwamba ni nchi huru na yenye kujitegemea.

Kwa kuwa kuendelea kuwategemea madaktari hawa kutoka nje huleta usumbufu pale ambapo muda wao umemalizika na baadae kusubiri kipindi chengine na kuwasubiri wengine, huku watu wetu wakiendelea kudhalilika.

(a) Je, ni lini vyuo vyetu Vikuu ikiwemo SUZA pamoja na hichi Chuo cha Afya Mbweni kitaanzisha digirii ya *medicine* kusudi Zanzibar iweze kujitegemea kwa madaktari, badala ya kutegemea madaktari kutoka nje.

(b) Kuendelea kutegemea madaktari hawa wa kigeni kwa mfano kutoka China, Cuba na Urusi sikwenda kinyume na dhamira ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 yaliyoongozwa na jemedari wetu marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Vile haitakuwa ni kwenda kinyume na ilani ambayo imetangazwa na Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri Mheshimiwa unaifahamu hali halisi ya nchi yetu ilivyo. Tumesomesha wengi na wameondoka wengi. Sababu za kufanyika hivyo pia unazielewa kila siku tunazungumza na ndio maana kuna mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba wanarekebisha mishahara ili watu wabakie.

Jana tuliambiwa hapa madaktari 19 na manesi si kidogo wameondoka nchini. Wengine wala hawaendi mbali, wanakwenda Bara tu, wanatafuta maslahi. Maslahi yetu yalikuwa si mazuri, hayawatoshi na sio wazalendo pia. Maana tusiotoshwa tupo wengi na tulibakia.

Sasa tunapongumza kwamba Chuo Kikuu cha SUZA na vyuo vyetu vya hapa cha Mbweni hakijajitayarisha kutengeneza madaktari, inaonekana huishi Unguja wala huishi Pemba, unaishi nje ya Zanzibar. Kwa sababu Chuo cha Madaktari kimeanzishwa miaka mitatu iliyopita na tuna madaktari katika Zanzibar *medical school* wanaosoma Unguja na Pemba. Wako chini ya Chuo cha Matantas wa Cuba na wanafundishwa hapa kwa miaka mitano na watakwenda Cuba kwa miaka miwili na watapatiwa vyeti vyao. Madaktari tulionao sasa hivi wanaofundishwa katika utaratibu huo wapo 50.

Unazungumzia madaktari kuja hapa kutoka Cuba, kutoka China, kutoka wapi. Jana hapa tumezungumza jamani madaktari wahatoshi ulimwenguni kote. Leo kama watu kwa nia nzuri wanakuja hapa, kutusaidia kutoka China wana mikataba maalum na Wacuba, tena leo liwe tatizo kwamba sisi hatuwezi kujitegemea. Hata tukisomesha hapa bado madaktari kutoka nje tunawahitaji kwa sababu hao tulionao si kila fani tunaiweza au si kila fani tunamtaalamu. Kwa hivyo wao wanapokuja tuwashukuru kwamba wamekuja kutugomboa badala ya kuwalaani na kusema hivyo tunavyosema.

Nafikiri tunapowasemea watu wa nje tufikirie vizuri vyenginevyo wakinuna tutakaoumia ni sisi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kuwa si kweli kuwa wapo Wacuba wasiojua kiingereza na hata hicho Kiswahili.

Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kuwa wapo ambao hawajui kizungu isipokuwa wanajua lugha yao. Kama hivyo ni kweli wapo wa aina hiyo. Wizara yake kwa nini isichukue mkalimani wa kuweza kusaidia tukapata tiba kwa wananchi wetu waliokuwa hawajui kiingereza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwanza katika jibu mama nimesema kwamba hakuna daktari anayeletwa hapa bila ya kujua kiingereza au Kiswahili. Hatakama kiingereza kibovu basi wanajua, kibovu sawa sio kama kile unachokitaka wewe. Lakini la pili wanakuwa wanaambatanishwa na madaktari wa kizalendo ili waweze kuwatafsiria, kuwasaidia.

Kwa utaratibu huo unaosema wewe kwamba sina uhakika mimi ninachokisema nina uhakika na hao wanaokuja wanapoletwa huku kabla hawajaja huku wanahakikisha kwamba kwao wamesoma. Kwa sababu wanajua kwamba lugha tunazozitumia huku kwetu ni mbili Kiingereza na Kiswahili. Kwa hivyo wanaokuja hapa wote wanasema Kiswahili, hakikupendeza wanachosema hayo ni mengine.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa mara nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Makamo Mwenyekiti, wa Kamati ya Wanawake, Ustawi wa Jamii, ambalo eneo langu moja ni Wizara ya Afya. Nilipokuwa naongoza Kamati ya Ustawi wa Jamii Pemba nilishuhudia daktari wa Kicuba ambaye hajui Kiswahili wala Kiingereza. Maelezo hayo yalitolewa na daktari dhamana wa hospital ya Chake-Chake, kama malalamiko yake kwa Kamati.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri anashindwa kutwambia kwamba yeye yahujui ukweli huo au anakusudia kulidanganya Baraza.

(b) Mbali ya tabia hiyo ya kutokujua kusema kiingereza tulimshuhudia daktari huyo akivuta sigara kwenye. chumba ya *operation theater*. Je, pia hayo ni maadili mazuri kwa utumishi wa umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, madaktari waliokuwepo Pemba ninaowajua mimi ni wawili na ambao ndio wanaowafundisha wanafunzi. Mimi mwenyewe nimezungumza nao kwa kiingereza, mimi sijui Kispenish. Tumezungumza na tukafahamiana. Sasa sijui hao uliokutana nao wewe ulikutana nao wapi na wepi.

Suala la kufanya kazi *theater* kwa kuwa hawafahamu kiingereza. *Theater* kinachofanywa pale ni kazi si lugha na waliokuwepo pale wote wanajua wanalolitenda kwa sababu wanakwenda na mgonjwa tayari keshachunguzwa na anajua nini analolifanya. Watu kule wamejipanga kama timu na kila mmoja anafanya kazi yake. Hakuzungumzwi kule, kunafanywa kazi, anaonyoosha mkono, anapewa mkasi, ananyoosha mkono anarudishiwa, anaongoza huku anapandishiwa *pressure*, anaona *pressure* imeshuka, inashushwa. Basi ndicho kinachofanyika *theater*. Sijui kama uliingia huko ukayaona hayo au sijui taarifa ulizipata vipi. Lakini *theater* hakuna mazungumzo. Kwa hiyo daktari kutokujua kiingereza bado halijawa tatizo.

UTARATIBU

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, taarifa yangu ni kwamba kwa niaba ya Wananchi wa Zanzibar nilikuwa nataka kujua kwamba daktari huyo alikuwa akivuta sigara sio mazungumzo. Je, sigara ni miongoni mwa maelekezo ya serikali ndani ya *theater*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Sisi hilo hatujaripotiwa kwa hiyo sina uhakika. Kama kavuta si utaratibu lakini hatujaripotiwa.

Nam. 44

Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Hapa Tanzania tunavyo vyombo viwili vinavyoshughulikia mchezo wa mpira wa miguu, navyo ni TFF na ZFA. Kimoja kinafanyia kazi Tanzania Bara na chengine Tanzania Zanzibar.

(a) Mhe. Waziri, Je, vyombo hivyo hukaa pamoja wakati wa kutayarisha Timu ya Taifa ya Tanzania.

(b) Wakati wa kutangaza Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu vijana kutoka Zanzibar huwa ni kidogo. Je, hii inasababishwa na udogo wa nchi yetu au ni vigezo gani vinavyotumika kuwapata wachezaji wa Timu yetu ya Taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake nam. 44 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hapa Tanzania tunavyo vyombo viwili vinavyoshughulikia michezo wa mpira wa miguu, navyo ni TFF na ZFA. Kimoja kinafanyia kazi Tanzania Bara na kingine Tanzania Zanzibar.

(a) Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba vyombo hivi TFF na ZFA huwa havikai pamoja katika kutayarisha timu ya Taifa ya Tanzania kwa vile jukumu la kutayarisha timu huwa ni la kocha aliyepewa dhamana ya timu ya Taifa na sio vyama vya michezo.

(c) Mhe. Naibu Spika, uteuzi wa wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, hufanywa na kocha anayehusika ambaye huteua wachezaji nchi nzima kwa vigezo vya uwezo wa wachezaji husika bila kujali anakotoka Bara au Zanzibar.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri ni wachezaji wangapi kipindi cha mwaka jana walibahatika kuchaguliwa timu ya taifa kutoka Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ni wachezaji wanne walioshiriki mwaka jana kwenye timu ya taifa kutoka Zanzibar na majina yao naomba nikutajie:-

1. Nadir Haroub Kanavaro
2. Agrey Morris
3. Suleiman Kassim (Selembe)
4. Abdi Kassim Badi

Mhe. Mwakilishi kwa sababu wewe ni kijana unayetoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mhe. Mwakilishi wa viti vya vijana. Nakuomba ushirikiane na timu ya taifa, timu ya Jamhuri iliyokuwepo Mkoa wa Kaskazini Pemba ili uwaendeleze na wewe uwe ni mlezi wa timu ile ya Jamhuri kutoka Pemba.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hiyo kwa kuuliza swali la nyongeza.

Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri hapo nyuma tulikuwa tuna utaratibu wa vyama vya Mipira ya Miguu yaani TFF na ZFA wakati wa kuteuwa timu ya taifa, hususan katika hawa makocha wa timu ya taifa. Anapotoka kocha Mkuu akiwa ni kutoka Tanzania Bara basi msaidizi huwa anatoka Tanzania Zanzibar.

(a) Je, kwa nini hivi sasa kocha msaidizi hatoki Zanzibar.

(b) Wananchi wengi wa Zanzibar hawaelewi maana ya neno TFF, na wengine hawaelewi neno ZFA. Je, namuomba Naibu Waziri atueleze urefu wa maneno hayo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kama alivyotangulia Mhe. Naibu Waziri kusema kwamba tuna vyama viwili vya Michezo, tuna TFF na tuna ZFA. TFF maana yake ni cha Tanzania na ZFA ni kwa ajili ya Zanzibar. Kwa hivyo vyama vyote viwili hivi kila kimoja kinasimamia upande wake.

Katika kuwateuwa wachezaji ni kocha mwenyewe ndiye anasimamia wachezaji gani na sio vile vilabu au vile vyama vya mpira. Mara nyingi kocha huyu Pounsel zaidi anaiangalia ligi ya Bara haiangalii huku Zanzibar. Chanzo ya kutafuta uanachama wa FIFA moja ni hilo ni kutaka kujitanafasi na sisi tutoe vipaji vyetu. Hiyo ni sababu muhimu kabisa kwa sababu tunajua kama kuna matatizo. Mheshimiwa Mjumbe usiwe na wasi wasi imani yangu ni kwamba mwakani na sisi tutachaguliwa mmoja katika *member* wa FIFA.

Mhe. Nassor Salmin Ali: Mhe. Naibu Spika, swali langu lilikuwa uteuzi wa kocha msaidizi, naomba maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, mara hii iliyopita alikuwa ni Moroko. Lakini kama nilivyotangulia kusema kwamba uamuzi anao kocha mkuu. Kwa hiyo akisema kwamba huyu ananifaa au huyu hanifai inakuwa ndio hivyo hivyo. Ndio maana nikasema maana ya kutafuta uanachama wa FIFA ni kuepuka matatizo hayo. Tunataka kujitanafasi ni hilo tu.

Nam. 204

Kuanzisha Kituo cha "Mkono kwa Mkono"
(One Stop Centre)

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa Kuanzisha Kituo cha "Mkono kwa Mkono" (*One Stop Centre*) ambacho kinawaweka wataalamu wa aina tofauti kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya Kijinsia yanayowapata watoto na wanawake, hususan yale ya ubakaji, mimba za utotoni na aina nyengine ya udhalilishaji wa Kijinsia. Juhudi hizo za Serikali na Washirika wa Maendeleo inakwenda sambamba na Sheria ya Hifadhi ya Mtoto na Sheria nyengine zinazokusudiwa kuwalinda watoto na wanawake.

(a) Ni lini Kituo cha *One Stop Centre* kitafunguliwa Pemba.

(b) Pamoja na utaalamu walionao wafanyakazi wa kituo hicho, lakini bado wanahitaji vifaa vinavyoendana na utekelezaji wa majukumu yao. Je, mashine ya DNA itapatikana lini.

(c) Wafanyakazi wa Kituo hicho wanahitaji utulivu na kujengewa mazingira bora ili wasishawishike na baadhi ya mambo hasa fedha. Je, maslahi ya wafanyakazi wa kituo hicho yatakuwaje.

(d) Taarifa za watoto wangapi zimeripotiwa kituoni hapo kwa kipindi cha *January-June 2011* ambao walidhalilishwa Kijinsia.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 204 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Kituo cha *"One Stop Centre"* kwa huko Pemba kitaanzishwa hivi karibuni katika Hospitali ya Chake-Chake baada ya kukamilisha mchakato wa kutafuta vifaa na kuviweka, kutoa mafunzo maalum kwa Madaktari, Manesi, Washauri Nasaha, Polisi, Mahakama na Wanasheria ambao watahusika kufanya kazi katika kituo hicho.

(b) Mhe. Naibu Spika, chombo hichi cha *DNA* ni ghali sana na suala la ununuzi wa mashine ya *DNA* halipo katika Wizara yangu moja kwa

moja. Lakini kutokana na umuhimu wake Wizara yangu tayari imeshatoa ushauri kwa serikali kuhusu umuhimu wa *DNA*. Aidha tayari baadhi ya Washirika wa Maendeleo tunaoshirikiana nao katika kuendesha kituo cha *"One Stop Centre*" wameonyesha nia ya kutusaidia kutupatia chombo hicho hali itaporuhusu.

(c) Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa watendaji wa Kituo cha "*One Stop Centre*" Wizara yangu kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo Save the Children na *DANIDA* tumeandaa utaratibu mzuri wa kuwajengea mazingira mazuri watendaji wote wa kituo hicho ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri, wasiwe na wasi wasi wowote.

(c) Mhe. Naibu Spika, taarifa za watoto zilizoripotiwa kuanzia Januari hadi Juni 2011 ni 117, zikiwemo za kubakwa, mimba, kulawitiwa na kukashifiwa ngono.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana na ya wazi ya Mhe. Waziri ambayo nimeyapenda, niseme tu kwamba hii ni kawaida yake kutuelimisha kwa kweli. Naomba kumuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa yeye ni Waziri mwanamke aliyemstari wa mbele sana kukemea vitendo hivi vya ubakaji na udhalilisha wa watoto. Na kwa kuwa miongoni mwa watoto ambao wanadhalilishwa ni watoto wenye akili taahira. Na kwa kuwa mara nyengine watoto hawa hubakwa na watu wengine wa nje lakini mahakamani huwataja wazee wao, kwa sababu ya upungufu wa akili. Je, wizara haioni haja sasa ya kuwaajiri wakili maalum kwa ajili ya kusimamia kesi za watoto wenye akili taahiri ili wazee wao wasidhalilishwe.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, swali sikulipata vizuri kwa kweli.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwakilishi rejea suali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, swali langu kwamba miongoni mwa watoto ambao wanafanyiwa vitendo hivi ni watoto wenye upungufu wa akili, ambao wanapokwenda Mahakamani hushindwa kutoa maelezo sahihi juu ya matendo waliyofanyiwa na mara nyingi huwataja wazee wao kama ndio wahusika.

Swali langu ni kwamba je, Wizara haioni haja ya kutafuta wakili maalum wakamuajiri kwa ajili ya kutetea kesi za watoto hawa wenye upungufu wa akili?

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niseme hata hao watoto ambao ni taathira kama hujawafanyia kitendo kibaya hawawezi wakakuashiria, kwamba ni wewe ndiye muhusika.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mara tu itakapoanza sheria yetu ya mtoto kama ni baba, kama ni mtu mwengine yeyote atakayembaka mtoto ambaye ni taathira na ikajulikana na akafikishwa katika kituo hiki cha *one stop center*, hatoki.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kuweza kumuuliza Mhe. Waziri.

(a) Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kuwa tayari yumo katika matayarisho ya kuweza kujenga hiyo *One Stop Center*. Lakini je, Mhe. Waziri haoni ikisha bajeti tu kituo hicho kiwe kishamalizika.

(b) Suala la pili wameripotiwa hapa ameeleza Mheshimiwa kuwa ni mia moja na zaidi ambao walioripotiwa kuwa ni watu waliobaka. Ni wangapi ambao wamefikishwa Mahakamani na wakachukuliwa hatua.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika,

(a) Kujenga hivi vituo vya *One Stop Center* si kazi rahisi lakini tunakwenda nayo kwa utaratibu mambo ni kidogo kidogo. Lakini hata hivyo tumeweka Pemba iwepo na Unguja iwepo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuanzisha mambo haya ya *One Stop Center* na kupokea malalamiko mbali mbali kutoka kwa wazee wa watoto wao wanaobakwa ni kwamba kesi zote zilizokuwa zikipelekwa mahakamani zilikuwa hazihukumiwi.

(c) Hatujapata hata kesi moja tukaambiwa kwamba huyu angalau kafungwa kiasi cha miaka miwili au mitatu au mitano.

(d) Sasa hivi tutakuwa mara tu sheria yetu itakapopita tutakuwa tunafuatilia kesi zote za watoto. Kupitia vituo vyetu vya *One Stop Center* kiliopo hapo Mnazimmoja vitakavyofunguliwa katika mawilaya na Mikoa mote humo mpaka shehia. Tutafuatilia na mtasikia, mtapata habari kwa vyovyote atakayembaka mtoto kapelekwa Mahakamani na kafungwa.

Nam. 156

Kupanda kwa Gharama za Maisha

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Mara baada ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, wananchi wa Unguja na Pemba walijenga matumaini makubwa kupata angalau afueni ya maisha. Jambo la kusikitisha ni kuwa ukali wa maisha umeongezeka maradufu kuliko ilivyokuwa kabla ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mfano: bei ya mafuta ya petroli ilikuwa ni Shs. 1,650/= kwa lita sasa ni Shs.2,000/= kwa lita, mafuta ya taa ilikuwa ni Shs. 1,150/= lita sasa ni Shs. 1.650/=, mafuta ya dizel ilikuwa ni Shs. 1,750/= na sasa ni Shs. 2,080, mchele wa mapembe ilikuwa TShs. 900/= sasa ni Shs. 1,200/= kwa kilo, sukari ilikuwa TShs. 1,200/= sasa ni TShs. 1,800/= kwa kilo moja.

(a) Je, Mhe. Waziri, jambo hilo linasababishwa na nini.

(b) Je, Mhe. Waziri, unawaambiaje matumaini gani wananchi wa Zanzibar katika mfumuko wa bei za vyakula.

(c) Je, wananchi wategemee nini siku zijazo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 156 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba bidhaa zimezidi lakini sikubaliani naye kwamba zimezidi mara dufu. Kama alivyoeleza katika suala lake. Bei zimeongezeka kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, bei ya mafuta ya petroli imeongezeka kwa asilimia 14.4 na sio mara dufu, bei ya dizel imeongezeka kwa asilimia 17.7 na sio maradufu na bei ya mafuta ya taa imeongezekwa kwa asilimia 26.2 na sio mara dufu. Kwa upande wa chakula mchele umeongezeka kwa asilimia 9, unga wa ngano haukuongezeka hata asilimia moja na sukari imeongezeka kwa asilimia 16.

Lakini hata hivyo kuongezeka kwa bei hizo kumetokana na sabubu zifuatazo:-

- Mhe. Naibu Spika, mafuriko na majanga makubwa mbali mbali yaliyokumba nchi za Mashariki ya mbali kama Urusi

na Marekani ambao imesababisha kupanda kwa bei za vyakula katika soko la dunia.

- Vile vile kutokea kwa miripuko mbali mbali ya maandamano katika nchi za ghuba kumepelekea kupanda kwa bei za nishati ya mafuta. Hali hiyo hiyo imetokea kwa bahari ya Hindi kupitia Somali ndio vyombo vingi hukamatwa. Kwa hivyo, bei za usafirishaji bidhaa kupitia katika upande huo ni kubwa sana au kuzunguka katika sehemu nyengine ili kuepukana na uharamia wa bahari ya Hindi. Kwa hivyo, hiyo inapelekea kupanda kwa gharama za bidhaa lakini pia kupanda kwa bei ya fedha za kigeni kunasababisha sana kupandisha bei za bidhaa.

Mhe. Naibu Spika, katika kulifanyia kazi suala la bei Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa kanuni maalum zitakazosimamiwa na Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko ambazo zitafuatilia mwenendo mzima wa bei za bidhaa na hasa chakula. Kanuni hizo zinajumuisha utaratibu wa uletaji chakula, mwenendo wa bei za bidhaa, gharama zinazohusiana na chakula utaratibu huu tunategemea kuutumia katika kukuza biashara, tutautangaza kwa wananchi hivi karibuni. Mhe. Naibu Spika, tunaamini kwamba wafanyabiashara wameonesha moyo mzuri kabisa wa kushirikiana na serikali kuzifuata kanuni hizo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kama bei za bidhaa zinapanda siku hadi siku, lakini Mhe. Waziri pia utakubaliana na mimi kama sasa hivi mafuta ya petroli ni 250,000/- kwa lita kama umekubaliana na mimi hali hii tutakwenda nayo mpaka lini.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba upandaji wa mafuta unatokana na kupanda katika Soko la Dunia hatuna ubavu wa kupinga hilo, inabidi tununue mafuta kwa bei kama ilivyo katika Soko la Dunia. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kama mlivyoona katika bajeti haijapandisha ushuru wa bidhaa yoyote.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri siku aliposimama katika kiriri Kibandamaiti baada ya kuteuliwa alisema mapembe sasa basi.

a) Je, nini kauli ya utekelezaji wa jambo lile.
b) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kauli ile ni mbaya kusema kabla ya kutenda.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wote kwamba tangu tumeingia madarakani, tumechukua hatua madhubuti za kudhibiti uingiaji wa vyakula visivyofaa kwa matumizi ya wananchi. Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Afya tumepanga mikakati madhubuti kabisa, naomba niwahakikishie kwamba tangu uanze mwezi wa Novemba mpaka leo hapajaingia chakula chochote, sio kwamba mchele tu lakini ni chakula chochote ambacho hakifai kwa matumizi ya binadamu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011-2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana asubuhi hii ya leo kwa kunipa nafasi hii na mimi nitajitahidi nichukue angalau dakika kumi kwa kuchangia. Mimi nataka nianze kama walivyoanza wenzangu kwa kumshukuru ndugu yetu Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote kwa njia moja au nyengine, waliomsaidia kutayarisha bajeti hii. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri aliisoma bajeti hii kwa umakini, ufasaha, yenye kukubalika na ina kila aina ya vionjo, mimi naita ni *tangible budget* ambayo imemgusa kila mtu. Kwa nini niseme imemgusa kila mtu? Kwa sababu imewagusa wafanyakazi pamoja na wakulima walio wengi.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imezingatia hasa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, inafaa zaidi serikali ichukue juhudi za kulinda vianzio vyake vya ndani ili kuongeza mapato yetu ya nchi. Mhe. Naibu Spika, mwaka jana mapato yetu yalifikia bilioni 444 na hivi sasa tuna makadirio ya 613. Serikali hapa imejitahidi na imeongeza ongezeko kubwa la mapato, tunajitahidi hapa na tunajua uchumi wetu umekua. Kwa hivyo, baada ya kukua kwa uchumi wa nchi tunategemea sana hata wananchi wetu uchumi wao utakuwa.

Mhe. Naibu Spika, kutokuongeza kwa kodi za serika, serikali tunataka ichukue hatua madhubuti ya kuweza kulinda wale wafanyabiashara ambao wataongeza bei ya vitu ili bei zisiwe kubwa. Mhe. Naibu Spika, udhibiti na makusanyo ya mapato serikali inatakiwa ichukue hatua za ziada kwa sababu haijatueleza kabisa itakusanya vipi na itakwenda vipi. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tuna vyanzo vingi tuseme kama air port, kamati yangu ilipita pale kwenye makusanyo ya *visa* tuliona kama pana mmong'onyoko mkubwa wa uvujaji wa mapato ya serikali. Mhe. Naibu Spika, pale wanaweza kuingia abiria 60 lakini tukaambiwa wameingia abiria 30 hivyo hatujui zile 30 visa zimekwenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile uingiaji wa wageni mahoteli hapa kuna ubabaifu mkubwa sana, wale wawekezaji wanaweza kuwa na vitabu viwili au vitatu lakini akenda Afisa wetu wa *ZRB* pale anapewa kile kilichokuwa sicho. Kwa hivyo, serikali ituoneshe nia halisi ya kudhibiti mapato yake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nachangia tena kwenye ukurasa wa 46 ambao unagusa nishati yetu ya mafuta. Sina budi kuishukuru serikali kwa kutekeleza na kupitisha sera ile ya mafuta, mafuta ni yetu. Mhe. Naibu Spika, hapa nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitamshukuru ndugu yangu Waziri aliyepita Mhe. Mansour Yussuf Himid kwa ujasiri wake mkubwa, kwani alitumia ujasiri mkubwa na sote tulimuona mimi nampa pongezi zangu binafsi, ndugu yangu nakushukuru sana kwa ujasiri wako.

Mhe. Naibu Spika, pia nalishukuru Baraza lilopita kwa ujasiri mkubwa uliotumia kwa kuweza kupitisha sera hii, lakini sera hii isibaki kwenye vitabu ikawa kama historia, sera hii tunatakiwa ifanyiwe kazi na itueleze hasa serikali wapi imefikia kwani wananchi wetu huko ni wakali kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, alikuweko mtaalamu elekezi aliletwa hapa lakini mpaka sasa hatujui anaelekeza nini, serikali bado imekaa kimya. Mhe. Naibu Spika, lakini ni imani yangu thabiti Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Umoja wa Kitaifa itatueleza inaelekea wapi na imefikia wapi, hivyo tusifike miaka miwili au mitatu tayari *process* ya kuchimba mafuta iwe imeshawezekana na kutuonesha njia ambayo tuliokuwa tunaihitaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi najali muda wako nataka niende moja kwa moja kwenye vipaumbele. Kipaumbele cha mwanzo mimi nakiita cha uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mhe. Naibu Spika, hii ndio dira ya serikali na hii ndio uso mzima wa serikali yetu kwa sababu tayari tumekabiliwa na tatizo la ajira. Kwa hivyo, kama tutaiwezesha wizara hii basi tutapungukiwa hata na zile ajira zisizokuwa rasmi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tumuwezeshe ndugu yetu, waziri wetu Mhe. Haroun Ali Suleiman yeye ni mtu mahiri sana, tumeona jinsi gani serikali iliyopita ilivyoinyanyua Wizara ya Elimu. Mhe. Naibu Spika, mimi tumaini langu yeye na watumishi wake ni watu bora na ana timu safi sana.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na mikopo ya AK na JK, hii mikopo ilikuwa haikutoka kwa ufasaha, mikopo hii ilitoka kwa upendeleo mwingi bila ya kificho lakini sasa nahisi madhali Mhe. Haroun amekaa hapa basi ataitoa wazi kabisa na jimbo la mwanzo kulipa hii mikopo itakuwa ni Jimbo la Mpendae.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Wizara ya Afya, hii ni wizara ambayo ina mgusa kila mtu na kila pahala. Lengo la serikali ni kuipa kipaumbele wizara hii ni lengo kubwa sana, sisemi hivyo kwa sababu Rais wetu alikuwa ni mtu wa afya lakini nataka kusema serikali imefikiria kutokana na wananchi wake. Kwa hivyo, basi pale Wizara ya Afya kuna kitengo kinaitwa *emergence room*.

Mhe. Naibu Spika, kitengo kile ni kizuri, kilichoelekezwa vizuri lakini sasa baada ya *emergence room* imekuwa *empty room* hakina chochote cha kianzio. Mhe. Naibu Spika, tunamuomba waziri husika akifika hapa katika majumuisho yake atueleze kitengo kile kiko wapi na kinafanya kazi gani kwa sasa hivi kwa sababu hakina hata kifaa kimoja.

Mhe. Naibu Spika, kuna sehemu inaitwa *Orthopedic Clinic* ile sehemu ya viungo, kile kitengo ni muhimu sana. Mhe. Naibu Spika, pale palikuwa na *nursing officer* ambao walikuwa wanasaidia kutia yale mapiopio. Juzi nilishuhudia wakati swahiba yangu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani ndugu yake alipopata ajali, kijana yule alipata ajali tangu saa 10 jioni tumetafuta daktari mpaka saa 5 usiku ndio tunampata na kuwekwa piopio.

Hiki ni kitu cha hatari kweli kweli, hivyo tunamuomba Mhe. Waziri atupe vitu vya ufasaha, atujuilishe na wale *nursing officer* wamepelekwa wapi, daktari anayepangiwa jioni mmoja anakuwa *round* katika hospitali yote, hivyo inakuwa hakidhi haja hasa ya wananchi wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe jibu muafaka kuhusu jambo hili. Mhe. Naibu Spika, vile vile kile kitanda ambacho kinatiliwa mapiopio ni hatari, ukidondoka tu nadhani baada ya kujitibu basi utapata na tetenas hapo hapo kwani ni kibaya sana.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna chumba cha *ICU* ambacho hakina *AC*, hakina *monitor* hii ni hatari kupita kiasi. Hivyo naiomba wizara baada ya bajeti basi ituambie itafanya nini kutekeleza vitu vile na hospitali ile ambayo sisi wenyewe tunaitegemea.

Mhe. Naibu Spika, sasa nagusa tena kwenye Wizara ya Elimu kwani ndio kitovu mama kabisa cha hapa huwezi kuwa na lolote bila ya kuwa na elimu, huwezi kuwa mtaalamu bila ya kuwa na elimu. Kwa hivyo, hii ni wizara kubwa sana, mimi ningeiomba kwanza itizame mitaala yake, irudie tena, ifanye *review* ya mitaala kwa sababu watoto wengi sasa hivi wanafeli anayepasi kwenda darasa la 12 basi huwa hawezi kwenda *form six, form six* akifika huwa anapata ziro kabisa hawezi kufanya chochote. Kwa hivyo, tunaiomba Wizara ya Elimu watizame tena na wafanye *review* ya mitaala hii vipi wajibu wetu tunaweza kufundisha.

Mhe. Naibu Spika, tunaishukuru sana serikali mpaka sasa imepigana vizuri pamoja na Wizara ya Elimu tumepata vyuo vikuu vitatu hili ni suala la kujisifia kweli kweli, tunatamani hata ile Chwaka tupige mbio kiwe Chuo Kikuu cha Nne na hicho kitu kinawezekana.

Mhe. Naibu Spika, pale *Zanzibar University* palikuwa na programu mmoja inaitwa *Pre-University Program* ile ilikuwa ikichukuliwa na wale vijana wetu ambao hawajapata *points* za kutosha. Mhe. Naibu Spika, ile program sasa sijui waziri kama anafahamu hicho kitu au hafahamu ile imefutwa na *TCU*. Mhe. Naibu Spika, mimi napatwa na wasi wasi mkubwa sana pasiwe na mbinu hapa mbadala wa kuondowa kwa sababu wanafunzi wetu wengi hawawezi kupata points za kutosha tukiwapeleka pale *pre- university* wanaweza wakafanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, sina maana kuwa Wazanzibari sio mahodari, ni mahodari kweli kweli lakini sijui wanateleza kwenye mitihani au inakuwaje wanashindwa kupata points za kutosha kujiunga na Chuo Kikuu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili alifikirie na kama halipo alitizame ili kujua anachofanya ni kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye ukurasa wa 61 ambao unasema ukarabati wa mitaro. Mhe. Naibu Spika, naishukuru sana serikali angalau kwa kuwa wameniwekea mitaro ya Mpendae na Kwabinti Hamrani. Vile vile jiografia inaonesha Jimbo la Mpendae limezungukwa na madimbwi mazito, kuna Shehia ya Migombani wananchi wanapata kadhia kubwa sana. Kwa hivyo, naiomba wizara husika ifikirie na ule msingi wa Migombani kuweza na mwenzangu Mwakilishi wa Kikwajuni yeye anaujua zaidi kwani kila wakati inabidi tuitwe kwa kutatua matatizo ya pale.

Mhe. Naibu Spika, labda niende kwenye utamaduni kidogo kama inavyonionesha kamati yangu. Mhe. Naibu Spika, utamaduni haukugusiwa kwenye bajeti hata kidogo, hivyo ninaiomba serikali iweke njia muafaka kwa kuweza kuutambua utamaduni wetu kwa sababu ndio hapa tutakosekana na mmong'onyoko wa kimaadili, huu utatusaidia kwa kila nyanja.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi namalizia kwenye biashara, mimi nataka kumwambia Mhe. Mazrui tuna nini kilichotupata kwani miaka ya 1990 tulikuwa tukiteremsha vitu vingi, meli nyingi zilikuwepo pale lakini sasa hivi ukipita bandari utakuta meli moja tu ndio inayoteremsha vitu.

Mhe. Naibu Spika, hebu tutizame ni kitu gani kwani ana wataalamu wa kutosha sana, basi turudi nyuma ni kitu gani kilichotusibu. Mimi naamini serikali ina vyanzo vya mapato vingi lakini tunatakiwa tuvifanyie kazi. Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Waziri akija kwenye majumuisho yako nitakuomba utwambie ni kitu gani kilichotusibu mpaka sasa hivi biashara mianguka watu wa Tanzania Bara sasa hivi wamekuwa wako juu kuliko sisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo yangu hayo mafupi na kujali muda basi kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Mpendae napenda kuunga hoja hii mkono kwa asilimia mia.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia bajeti ya Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, naipongeza serikali kuweza kuandaa bajeti hii iliyogusa maeneo yote ya wananchi. Mimi nataka nizungumzie kuhusu habari kwani ni chombo muhimu sana nataka niipongeze serikali kwa kukipa kipaumbele na kuweza kuondokana kwenye mfumo wa *analogy* na kwenda kwenye mfumo wa *digital*.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nije kwenye wizara inayohusu vijana, wizara hii kwenye bajeti hatujaliona fungu linalowagusa vijana isipokuwa ni mfuko wa wafadhili kutoka Norway. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aweze kuwaangalia vijana kwani vijana ndio kiungo muhimu katika serikali. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara inayohusu vijana haina fungu lolote ambalo limeingizwa katika bajeti hii namuomba Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuweza kuwaandalia vijana bajeti yao katika bajeti zinazokuja.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi isipokuwa nitakuwa mpungufu wa fadhili kama nitakuwa sijaipongeza bajeti hii, kwa niaba ya vijana wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii, pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Rais wa awamu ya saba Dr. Ali Moh'd Shein, Rais wa kwanza wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa nampongeza kwa kusimamia kwa vitendo ilani ya uchaguzi ya CCM na kuitafsiri kwa vitendo kwenye uongozi wake.

Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi kumchagua waziri ambaye kwa uhakika "pumu imepata mkohozi". Napenda nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha yeye binafsi na watendaji wake kwa kututayarishia bajeti ambayo imeanza kuonesha matumaini kwa wananchi wa Zanzibar ambao ni wafanyakazi na wakulima. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutengeneza bajeti hii serikali ilifanya utafiti wa

kina kupitia wizara zake zote, kutokana na vigezo ambavyo vinafuta dira ya maendeleo, MKUZA, maendeleo ya milenia na bila shaka ilani ya Chama cha Mapinduzi hapo ndipo ikaja na vipaumbele ambavyo vimewekwa mbele katika mpango wetu huu mzima.

Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba wizara zote ni muhimu, lakini kupanga ni kuchagua na hasa ukiwa na fedha kidogo. Mhe. Naibu Spika, labda ningeanza na udhibiti wa mapato, mimi ningependa kugusia points mbili watu wamesema mengi, lakini mimi nimeona kwamba wadhibitiwe wafanyabiashara wakubwa kwa kutumia *machine* zenye kutoa risiti na kuacha kumbukumbu katika sehemu zao ili iwe rahisi kwenda kuangalia. Pia kuweka bei katika bidhaa wanazoziuza. Kwa hivyo, ni rahisi kutia thamani hivyo wenzetu ndivyo wanavyofanya nafikiri tujaribu utaratibu huo labda unaweza ukatusaidia.

Mhe. Naibu Spika, jengine lilozungumzwa hapa jana kuhusu uuzaji wa karafuu hilo ni kweli tukiwa tutaweza kufanya hivyo hawatoweza nchi nyengine kuuza, maana sasa hivi Kenya wanauza karafuu kuliko hata sisi tunaopanda na wao hawana mkarafuu hata mmoja. Kwa hivyo, mimi nafikiri hilo likifanyika kwa kiasi fulani nalo litatusaidia.

Mhe. Naibu Spika, tukija kwenye vipaumbele tunazungumzia elimu, nafikiri tupange tukipangua elimu ndio msingi wa maendeleo yote. Mhe. Naibu Spika, umuhimu wa elimu unajuulikana na hasa sayansi na hesabati. Serikali imejitahidi kwa kiasi kinachoweza kuleta vitabu, maabara zote za sayansi pamoja na za kompyuta, imekopa imejenga maskuli yasiyopungua 18 Unguja na Pemba ambayo yana nyumba za walimu, itakuwa na dakhalia. Mhe. Naibu Spika, hiyo ni kwa dhamira moja tu ya kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma elimu iliyo bora.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningetoa ushauri kwa wazee, kwani tuhakikishe kwamba watoto wetu wanasoma na sisi tuwe tunawasimamia. Mhe. Naibu Spika, pesa zilizotumika ni za mkopo ingawa mkopo ni mali yetu kwa sababu baadae tutalipa, ikiwa hatukulipa kwa sasa hivi tutapeleka mbele ukikopa hufungwi ukisema utalipa. Mhe. Naibu Spika, watoto wakisoma watachangia wao kwa sababu watamaliza kusoma watakuwa wataalamu na watalipa kodi itakuwa ni sehemu ya malipo haya.

Mhe. Naibu Spika, kipaumbele cha pili kilichozungumzwa ni afya. Mimi nataka nizungumzie hili kwa sababu ndiko niliko hasa nataka nianze kuzungumzia kuhusu mambo matatu. Mhe. Naibu Spika, yako mambo matatu ambayo yanatupa shida na sote tunaijua madawa, vifaa na rasilimali watu. Mhe. Naibu Spika, tukizungumzia rasilimali watu tuna Chuo kimoja cha Afya ambako ndiko wataalamu wetu wanakojifunzia. Mhe. Naibu Spika, tunapenda

kukiimarisha chuo hicho na tuko katika utaratibu wa kukiimarisha ili kuweza kutoa huduma zinazostahiki. Mhe. Naibu Spika, chuo chetu kwa sasa kinaanza na ngazi ya diploma kwa sababu tunajiandaa kwenda kwenye digrii. Kwa hivyo, tunahitaji kutoa watendaji bora.

Mhe. Naibu Spika, afya ni sehemu ambayo sio ya kufanyia masihara sio kama kilimo ukilima jua likitoka ikikauka itakuwa basi, maisha ya binadamu yakipotea yamepotea. Kwa hivyo, lazima tuhakikishe kwamba tunatoa watendaji walio bora kitaifa na kimataifa ili waweze kusoma tukiwa hapa kwetu na hata wakitoka nje. Kwa hivyo, tunataka wanafunzi wenye viwango ili tutoe wataalamu wenye viwango, siku zote unavuna unachopanda, ukiweka mtaalamu mbovu utatoa mtaalamu mbovu, ukipeleka wanafunzi wasio na viwango watatoka wataalamu wasiwe na viwango na pale tunachofanya kazi nacho ni maisha ya binadamu akipotea ndio kapotea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu chuo cha madaktari kwenda kumjuilisha mjumbe aliyeuliza suala hapa kwamba chuo tunacho isipokuwa tuna na changamoto. Mhe. Naibu Spika, naomba tutizame kwa jicho la huruma ili tuwe na bajeti endelevu tuweze kuwafundisha madaktari kwa sababu madaktari ukiwafundisha nyumbani wanaobaki ni wengi kuliko watakaofundishwa nje wanaorudi ni kidogo, sikwambii hao walioko hapa wanaondoka. Lakini tukiwa tutawafundisha hapa katika mazingira ya hapa na ikiwa tutawatuza vizuri watakuwa na moyo wa kubaki hapa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo ningependa kuzungumzia masuala ambayo mara nyingi tu huwa yanajitokeza, suala la *coast shearing* katika Wizara ya Afya. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kwa utaratibu kuna makundi yangependelewa kupewa misamaha kama tungekuwa tunacho cha kuwahudumia, lakini kama tuna madawa kidogo, kama tuna vifaa havitoshi suala la *coast shearing* kwa kweli haliepukiki.

Lakini kama tutajipanga vizuri na wizara ikatuonea huruma na serikali tukiwa tutakwenda kama vile ambavyo serikali inavyotaka na kipato chetu kikiwa kizuri mimi sioni tatizo kwa nini kina mama wazae walipishwe, sioni tatizo kwa nini watu wenye maradhi ya muda mrefu walipishe, sioni tatizo kwa nini maradhi sugu watu walipishwe wazee na walemavu. Hayo ni makundi ambayo kwa kweli yanatakiwa yasilipe lakini je hali inaruhusu? Tutajitahidi kujipanga ikiwezekana huko mbele mambo yakiwa mazuri lakini kwa kipindi hiki nafikiri *cost sharing* tutaona jinsi gani tutakavyoweza kufanya kwa wale ambao kidogo tuwapunguzie mzigo na wengine tujitahidi tulipe kwa hicho kiwango kidogo tutakachoweza mpaka tutakapoweka mambo sawa.

Nataka nizungumzie kuhusu uchumi kuwawezesha wananchi. Nashukuru kwamba kuna wizara hiyo imeanzishwa na kwa mtu aliyepewa nina imani itakuwa ni wizara ambayo itatoa huduma inayotakiwa kwa wananchi kuweza kuimarisha uchumi. Lakini katika mazungumzo nilisikia watu wanazungumzia kuhusu mwani, ni moja katika sehemu ambayo inaongeza pato katika nchi hii.

Kwa nini jamani kinamama wanaofanya kazi pale ukiwatizama wengi ni wa rika ya makamo na wazee, ule mzigo wa mwani sio mwepesi na kipato kinachopatikana baada ya kwisha kukaushwa ni kidogo mno. Kwa kweli bei ile wanayopewa si halali ikiwezekana ifanyiwe utaratibu kama kweli na wao wanachangia pato la taifa. Kwa hivyo, nyenzo, vifaa vya kubebea ikiwezekana watizamwe.

Tukizungumzia pia kuwezesha wanawake kiuchumi naona wanawake wengi wanajishughulisha na usindikaji wa matunda na viwanda vya kufanyia hivyo sio vikubwa hata hivyo, hata vya *juice* sio viwanda vikubwa. Wakiwa wanawezeshwa wataweza kutoa hivyo wanavyovifanya kwa wingi vikaweza kusambaa nchini na hata kuuzwa nchi za nje. Kwa hivyo, mimi naomba watizamwe na akina mama hao wasindikaji wapate viwanda vidogo vidogo ili waweze kufanya kazi hiyo kwa vizuri zaidi.

Niunganishe madhali nazungumzia wanawake sasa nizungumze na suala la wanawake kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Panazungumzwa sana hapa suala la ubakaji. Jamani sio suala la ubakaji wa watoto tu, wanaobakwa ni watu wote, mtoto tangu wa mwaka mmoja anabakwa mpaka watu wazima wa miaka 70 wanabakwa, wanabakwa wanawake na wanabakwa wanaume. Hivyo ndivyo hali halisi ilivyo, hamko katika mahospitali mngekuweko kule mngeyaona haya.

Sasa tunapozungumza suala la ubakaji jana palijibiwa swali kwamba labda mtoto akishabakwa wazee wakikubaliana mtoto aozeshwe. Mimi kwa kweli hicho kimeniumiza kwa sababu nawaelewa watoto wanaobakwa hali yao inakuwaje. Leo mtu kambaka mtoto, kesho watu mnakubaliana anaozeshwa, mtu yule yule kamuumiza halafu tena aende akakaenae maisha mtu yule kweli hiyo ni haki? Kama alikuwa anamtaka kwa nini asingekwenda kuposa kwa utaratibu, lakini aende akamfanyie mabaya akisha aozeshwe akakaenaye ina maana unamtosa maisha yake yote.

Mtu anapobakwa anaumia mambo mawili, kiwiliwili na saikologia, lile la kubakwa halitoki maisha kwenye kichwa chake, kwa hivyo, usimtegemee mtu huyo atafurahia ndoa na mume yule aliyembaka. Sio hivyo tu, mara nyingi wanaobakwa watoto wa kike huwa wanachukia wanaume na huwa hawataki maisha yao kuolewa kwa sababu ya kumbukumbu waliyonayo katika maisha

yao. Ushauri wangu anayebaka mtu sio tu asipewe dhamana, ikiwezekana afungwe hata maisha kama adhabu ya kufa haipo na pia ahasiwe ili tendo hilo asilifanye tena.

Nizungumzie mazingira. Tumeona picha mbili tulipokuwa tunafanya ziara ya Rais, Pemba kwa suala la kuchonga matofali ambayo hayazingatii utaalamu, watu hawafukii mashimo wanachimba nje ya kina walichoambiwa, halafu hawapandi miti. Sio matetemeko tu yatakayotuathiri, kuna ajali zinaweza zikatokea nyumba zinaning'inia kule na watoto wadogo wanacheza ni hatari. Mimi naomba wataalamu wawaelekeze na wanaoelekezwa wafuate maelekezo. Kwa sababu litakapotokea watakaoathirika ni wao waliokaribu zaidi na yale maeneo.

Tumekwenda Micheweni nako mazingira katika mabonde ya mpunga nayo ni tatizo maji yameingia mpaka kwenye mashamba, wenyewe wanasema wameweka mikuko ya udongo bado yanabururwa na maji. Lakini tatizo lililokuwa kubwa kule ni ukataji wa mikoko. Serikali ijitahidi kuwajengea hayo matuta lakini na elimu itolewe kwa watu husika wale walioko kule wapande mikoko, waitunze na wailinde ili kuhakikisha kwamba hilo tatizo lisitokee tena. Kwa sababu hata kama huo mkuko utajengwa kama maji ya bahari yatakuja juu mikoko haitopandwa basi tatizo hilo halitoondoka.

Sasa nizungumzie suala la uvuvi. Nasikia watu wengi hapa wanazungumza Bahari Kuu, lakini kuna uvuvi mmoja rahisi tu ambao hata hautaki maji marefu. Mimi nilikwenda Mafia, nimekuta kule wanavua *prowns, prowns* zinaweza zikavuliwa, zikatayarishwa, wakazalishwa, wala hawataki bahari kubwa.

Mazingira yaliyoko Pemba ambapo bahari imeingiliana sana na mito sehemu zile ndizo nzuri kwa kuzalisha *prowns, prowns* zina bei kubwa, mahoteli ya watalii yote wananunua, kama haya yatafanyika tutawasaidia watu wetu hawatokata hayo matofali. Kwa sababu Pemba nzima inaweza kufanya hiyo kazi na kipato kitakuwa kikubwa na baadhi ya sehemu za Unguja. Kwa hivyo, mimi nafikiri hilo nalo lingetiliwa maanani kama hatuyawezi hayo maboti makubwa basi hata uvuvi wa *prowns* ungetusaidia katika nchi yetu na hata kuuza nje. Kwa sababu walioko Mafia wanauza pale na wanauza nchi za nje.

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuzungumzia suala la utumishi. Naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi, mishahara, motisha na kiinua mgongo vimepewa kipaumbele. Na wafanyabiashara tunakuombeni msitumie huo mwanya kwa sababu nyinyi hamkuongezewa kodi, kwa hivyo msiutumie mwanya kuwapandishia bei bidhaa watu tukarudi tulikotoka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge tena mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia leo hii tukawa na afya njema na salama.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kuweza kuwasilisha bajeti hii iliyo na ufasaha wa kutosha kwenye maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nielekee kwenye habari. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa kukaa na kuamua kwa makusudi yeye pamoja na watendaji wake akaliunga mkono suala la habari ambalo ni suala muhimu kwenye jamii yetu na wananchi kwa ujumla.

Pia niende kwenye kilimo na nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kutekeleza wajibu wake na majukumu na kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, niende pia katika maeneo ya elimu nako nimpongeze pia Mhe. Waziri pamoja na serikali kugusa maeneo yote ya elimu na kuweza kudondoa dondoo ambazo zinawahusu walimu pamoja na vijana wetu.

Nikiendelea niende kwenye afya. Pia Mhe. Waziri amelenga lengo kuu la kwenye afya kuboresha vituo vya afya na sehemu zote zinazogusia mambo ya afya.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye miundombinu na nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na serikali kuelekeza nguvu zake zote kwenye miundombinu ya barabara na mingine ambayo imo kwenye nchi yetu kwa maslahi ya jamii na watu wetu. Kwa sababu Mhe. Naibu spika, nimesimama kwa kuipongeza serikali sikusimama kwa ajili ya kutoa dondoo moja moja basi naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kutekeleza wajibu wake na maslahi ya wananchi.

Mimi na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya asubuhi hii ya leo na kutuwezesha kuja hapa kuendelea na shughuli zetu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Lakini pili nikushukuru wewe Naibu Spika kwa imani yako ya kuniona na kunipa wasaa kidogo na mimi kuchangia katika hotuba hii ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 kama ilivyowasilishwa hapa Barazani na Mhe. Waziri wetu. Kwani kwa kufanya hivyo, umenipa fursa ya kuingia katika historia ya kuchangia bajeti hii ya kihistoria ambayo ni ya kwanza katika mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake wote. Kwanza kwa matayarisho mazuri ya bajeti hii ambayo baada ya kuileta humu ndani kila mtu amehemewa kwa mambo ambayo yamo humu ndani, lakini pia kwa kuwezesha kuandaa semina muda mfupi kabla ya kujadili bajeti yenyewe. Katika semina hiyo napenda pia nimshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi ambaye alianza kwa kutoa miongozo kwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi jinsi gani ya kuweza kuijadili bajeti hii.

Lakini pia kwa watendaji wa wizara hii ya fedha kwa kutokuwa wachoyo, kwa uwazi kabisa wakaweza kutuelezea jinsi gani ya kuchambua bajeti. Jambo hilo kwa kweli tunaomba liendelezwe.

Mhe. Naibu Spika, jambo zuri ambalo pia lilifanyika katika siku hiyo ya semina ni pale watendaji wa Ofisi ya Wizara ya Fedha walipoamua kuanza kutanguliza kabisa kutwambia changamoto ambazo zinakabili bajeti hii. Nitapenda nikumbushe hapa tuliambiwa mwanzo kabisa kwamba vyanzo vya kodi bado ni vidogo, lakini pia kuna kazi ya ukuaji wa utalii ambayo hailingani na mapato yanayopatikana, lakini pia mapato makubwa ya rasilimali kwa ajili ya kutekeleza mpango wetu wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo na *resource* ambazo tunazo. Kwa hivyo, hilo Mhe. Waziri alilitanguliza mapema na nafikiri lilifahamika vizuri sana.

Naomba nianze kwa kupongeza vile vile serikali yetu kwa kutopandisha kodi. Tumeendelea mwaka jana vile vile katika bajeti kodi haikupandishwa na mwaka huu tumeliendeleza hilo lakini badala yake tukaona tujikite katika kudhibiti makusanyo ya kodi, kudhibiti pia misamaha ya kodi, lakini pia kuchunga matumizi ya serikali. Napongeza sana kwa hilo.

Kwa kweli jitihada zimeweza kuonekana tayari, kwa sababu kuanzia mwezi wa Januari, Februari na mpaka hivi sasa makusanyo ya kila mwezi ya kodi kwa *ZRB* na *TRA* yalikadiriwa kuwa shilingi 13 bilioni, lakini kwa sasa vyombo hivyo vya kukusanya mapato vimevuka lengo hilo na tayari wako kwenye asilimia 14 hadi 17. Ni jambo la kupongezwa sana na tunaomba liendelee.

Mhe. Naibu Spika, hili linatupa moyo sana kwamba hasa bajeti yenyewe ukiingalia Mhe. Naibu Spika, niko na kitabu cha mwaka jana hapa katika mlinganisho kama tulivyoelekezwa na watendaji wetu jinsi ya kuitazama bajeti na naomba kidogo ninukuu ili kuonesha kwamba bajeti yetu ya safari hii imekuwa bora na inaleta matumaini zaidi. Na kama itatekelezwa ipasavyo ni imani yangu kwamba bajeti ijayo itakuwa bora zaidi.

"Katika mwaka 2009/2010 mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa shilingi 159.6 bilioni, mwaka 2010/2011 mapato hayo yalikuwa shilingi 171.6 bilioni, lakini kwa mwaka wa fedha tunaouzungumza 2011/2012 mapato hayo ya ndani yanakadiriwa kuwa shilingi 221.2 bilioni".

Mhe. Naibu Spika, ninachoomba kwa wajumbe wenzangu tukione hapo ni jinsi gani ukuaji huo wa mapato ambao tutaweza kuufikia. Tofauti ya ongezeko la mapato kati ya mwaka 2009/2010 na 2010/2011 lilikuwa ni asilimia 7.5, lakini tofauti ya ongezeko la mapato kati ya mwezi uliopita (2010/2011) na mwaka tunaouzungumza wa fedha 2011/2012 ni asilimia 28.9. Ni jambo la kupongezwa na kwamba bado jitihada ziendelee kwamba mapato yetu yanaweza kuongezeka na tukapunguza utegemezi. Pongezi sana kwa wizara hii kusimamia ukusanyaji huo wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, tulifahamishwa kuitizama bajeti iliyo bora na watendaji wetu, mimi kwa bahati nzuri sana katika somo la kuiangalia *pro-poor budget* kwangu mimi lilikuwa ni rudio kwa sababu nilipata elimu hiyo nilipokwenda Ghana kuhudhuria semina ya Wabunge. Na kwa kweli ukiivaa ile miwani ya *pro-poor budget* ukiiangalia hii bajeti yetu unakubali kabisa kwamba bajeti hii kweli ni bajeti inayozingatia matatizo ya wananchi wake katika kuwapunguzia umasikini.

Mhe. Naibu Spika, sifa za bajeti inayozingatia kupunguza umasikini kwa wananchi wake zimeelezwa, kwamba kwanza ni kuangalia matatizo gani makubwa ambayo yapo ndani ya jamii, halafu bajeti hiyo sasa ikaelekeza zaidi *resource* zake katika kutatua matatizo hayo.

Mimi nikiiona moja kwa moja niwaelekeze wajumbe wenzangu kwenye ukurasa wa 73 wa kitabu hiki basi pale maeneo ya kipaumbele moja kwa moja yanalenga katika kutatua matatizo ya wananchi wetu katika kuacha utekelezaji wa MKUZA II. Napenda kidogo kunukuu kwamba ni, 'kuimarisha huduma za afya'. Wajumbe wengi waliosimama hapa bado walikuwa na malalamiko kwamba huduma za afya haziko bora. Serikali imeliona hilo na fungu kubwa limetengewa Wizara ya Afya na ni imani yangu kwamba huduma hizi zitaboreka muda kwa muda kwa kadiri tunavyoendelea.

Lakini pia wajumbe wamekuwa wanalalamika sana na wananchi juu ya ubora wa elimu yetu. Serikali imesikia kilio na hiyo ndio kipaumbele nambari mbili katika bajeti hii katika kuboresha elimu.

Pia tatizo la maji bado ni sugu ndani ya nchi yetu na hilo limeonekana na serikali na ni moja katika vipaumbele. Katika kupunguzia wananchi wetu umasikini tunajua kwamba asilimia 40 ya watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi wameajiriwa katika sekta hii ya kilimo. Serikali imeliona hilo na nimpongeze Mhe. Rais aliyeelezea wakati akifungua Baraza hili mwezi wa Novemba kwamba kilimo tunacholima hakiwaletei tija wananchi wetu. Kwa hivyo, serikali imetenga fungu kuona kwamba sasa kilimo kinaboreshwa ili hao walioko kwenye sekta ya kilimo ambao si kidogo ni asilimia 40 ya wote walioajiriwa basi nao wanapata tija kutokana na kilimo hicho.

Lakini pia kutokana na tatizo kubwa sana la ukosefu wa ajira kumeanzishwa Wizara hii maalum ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, fedha zitatengwa na juhudi itafanyika kuona kwamba mazingira yanajengwa ili wale ambao hawajaajiriwa katika serikali wanaweza kujiajiri katika vikundi kwa kukopeshwa fedha kwa ajili ya kufanya miradi ili kuwapunguzia umasikini vile vile, lakini pia kuona umuhimu wa utafiti.

Mambo yote tunayoyafanya kama hatufanyi utafiti tutakuwa hatuwezi kujua kiasi gani tunapiga hatua na changamoto zinazotukabili ni zipi. Kwa hivyo, moja kwa moja mimi naiunga mkono hii bajeti kwamba kweli imekuwa ni bajeti ambayo imewatizama wananchi matatizo gani wanayo na imelenga katika kutatua matatizo hayo. Hongera sana Waziri wa Fedha kwa kutuletea bajeti ya aina hii.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi sana ya kueleza isipokuwa pia naomba nielezee suala zima ambalo lilikuwa ni ahadi ya Mhe. Rais naye wakati akihutubia Baraza hili siku aliyolifungua kwamba maslahi ya watumishi yataboreshwa. Nipongeze juhudi za serikali na kwamba waziri mhusika itakapofika wakati wake atatueleza viwango ambavyo maslahi ya wafanyakazi vitakuwa vimeangaliwa.

Lakini vile vile katika hili naomba niwakumbushe na niwatanabahishe sana wafanyakazi wenzetu kwamba na wao wana wajibu wa kuongeza jitihada katika utendaji wao wa kazi kwa kuzingatia maadili na wajibu wao wa kazi ili kuona kwamba wananchi wa nchi hii wanafaidika na ufanyaji kazi wao. Wakati serikali inafanya juhudi ya kuongeza maslahi yao kuona kwamba inazingatia pia elimu zao na hali ya maisha, basi na wao vile vile wakumbuke kwamba ni vizuri wakarudi kwenye maadili ya utendaji kazi na wakang'ang'ania msimamo wa uwajibikaji ili kuondoa manung'uniko kwa wananchi wetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na niseme kwa niaba ya Jimbo langu la Ikulu naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja nakushukuru sana.

Mhe. Machano Othman Said (Waziri asiye Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya serikali, lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hai na mzima na asubuhi hii kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii.

Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake wote. Mhe. Waziri na timu yake wamefanya kazi nzuri na dalili ya kazi nzuri ni kwamba waheshimiwa wote waliochangia bajeti hii wameunga mkono na wameona kwamba hii ni bajeti nzuri kwa serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, hii ni bajeti ya kwanza katika serikali ya awamu ya saba, kwa hivyo na mimi niseme kwamba, nawashukuru sana viongozi wetu, namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Dkt. Ali Moh'd Shein), Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais. Viongozi hawa wameonesha mwelekeo mzuri wa utendaji kazi serikalini, kwenye timu za mpira unaweza kuwa na wachezaji wazuri lakini unaangalia mambo matatu. Kwanza unaangalia uwanja wenyewe wa kuchezea kama mzuri, unaangalia timu imesajili, lakini lazima iwe na kocha wale wengine wanajiita kina Jose Morinyo *special one*.

Sasa kwetu sisi Zanzibar tumebahatika mwaka huu kwamba tunao uwanja mzuri kwa sababu hali ya kisiasa ni nzuri inaruhusu kufanya shughuli za kimaendeleo kuwahudumia wananchi wa Zanzibar kwa ukamilifu. Hali hii imetokana na busara za viongozi wetu, Mhe. Rais aliyepita Mhe. Amani Abeid Karume tunamshukuru sana kwa juhudi zake za kuleta amani na upendo nchini kwetu na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, lakini hata hawa viongozi tuliowachagua mwaka huu kama wengelikuwa hawana nia njema wangeyumba, lakini kwa sababu na wao ni watu makini na wanaopenda umoja basi kazi haikuwa kubwa.

Lakini la pili baada ya kuchaguliwa wamethibitisha kwa vitendo kwamba ni viongozi bora ambao walihitajika kwa Zanzibar. Kuna Mswahili mmoja alisema kwamba, "Jibu likisadifu swali, muulizaji anakuwa hana swali la ziada". Kwa hivyo, na viongozi wetu hawa wametoa majibu kwa wananchi kwamba wanaweza, wanahitaji mashirikiano tu ili tuweze kusonga mbele.

Mhe. Naibu Spika, bajeti ya mwaka huu ni bajeti ya wananchi ingawa haina jina kama wenzangu walivyosema. Kwa sababu Mhe. Waziri amejali sana maslahi ya wananchi, kama bajeti haiongezi kodi katika nchi yoyote basi bajeti hiyo ni ya kuwajali wananchi. Bahati nzuri kwamba, Mhe. Waziri hakutuongezea kodi, alilosisitiza ni umuhimu wa kukusanya kodi kwa vianzio viliopo na udhibiti wa matumizi ya serikali. Kwa hivyo, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri nasema hongera sana.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii ukurasa wa tano kuna mambo kama manane Mhe. Waziri amesema hayo ni kipaumbele katika ustawi wa wananchi wetu. Kwanza, kuimarisha maslahi ya watumishi wa umma. Ni ukweli uliowazi kwamba kwa muda mrefu watumishi wa umma wamekuwa na malalamiko ya msingi kwamba maslahi ni madogo, lakini kilio chao bahati nzuri serikali imesikia na Mhe. Waziri ametueleza kwamba kitatekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Naomba niungane na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwamba, kwa upande mmoja ni jambo jema lakini kwa upande wa pili na watumishi na wao waoneshe uaminifu wao kwa serikali. Na mimi naomba sio watumishi wa umma tu, lakini Wazanzibari wote sasa kila mtu ambaye anafanya kazi sehemu yoyote iwe binafsi, ya serikali, kajiajiri mwenyewe, tufanye kazi kwa bidii tubadilike ili tuendane na ushindani wa dunia.

Dunia imekuwa mbaya sana kwa sababu hali ya uchumi wa dunia ni mbaya, tangu wiki hii imeanza tunasikia habari za Ugiriki, uchumi wa Ugiriki umetetereka Ulaya nzima sasa hivi inapiga kelele wafanye nini ili kuinusuru Ugiriki. Kwa sababu ikiathirika Ugiriki na Ulaya yenyewe yote inakwenda, kwa hivyo, wanatafuta mbinu za kuwasaidia.

Kwa hivyo, niwaombe na ndugu zangu, wenzangu, Wazanzibari wenzangu tuone kwamba changamoto ya uchumi inaikabili dunia. Kwa hivyo, na sisi tujitahidi sana kufanya kazi kwa bidii, kila mmoja asitake kuhimizwa kwamba fanya kazi akiamke tu mtu afikirie unafanya nini jambo ambalo litaniletea tija ili kupunguza ukali wa maisha.

Jengine Mhe. Naibu Spika, huduma za afya zimezungumzwa humu kwamba zina umuhimu. Na mimi naunga mkono suala hili la serikali la kuimarisha huduma za afya. Ukiangalia bajeti kwa kina na haiwezekani kwa mwaka mmoja tukamaliza matatizo yote ya afya kama yalivyo matatizo mengine, lakini serikali imeonesha na imeweka mkono wake kwamba mwaka huu bajeti hii isaidie kuimarisha huduma za afya. Kuimarisha vituo vya afya, vitendea kazi, maslahi ya watumishi wa afya, kwa hivyo nao hawa wakipata hizi huduma tunatarajia kusonga mbele.

Mhe. Naibu Spika, maji safi na salama pia yamepewa kipaumbele, jambo hili ni muhimu sana na mimi bahati nzuri jimbo langu liko katika Mkoa wa Mjini Magharibi na hapa ndipo penye matatizo makubwa ya maji. Serikali mwaka huu bajeti yake kubwa iko kwenye maji, nafikiri shida kubwa ya Mkoa wetu wa Mjini Magharibi ukiachilia matatizo mengine lakini na idadi kubwa ya wakaazi wa Mkoa huu nao wanachangia ukosefu wa maji safi na salama.

Sasa kwa mradi huu wa serikali na tumemsikia Mhe. Waziri juzi akitwambia kwamba wana mradi mwengine pia wa Wachina wa kuchimba visima 57. Nafikiri Mkoa wa Mjini Magharibi tutapata 9 vitatusaidia sana kupunguza kero ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hizi fedha ambazo mmewapangia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati basi naomba wazipate zote ili miradi hii ya maji iweze kufanikiwa.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, suala la umeme wa uhakika ni jambo muhimu katika kuimarisha uchumi wetu na tunazungumzia kwa sababu tuna mipango mingi ya maendeleo. Tuna utalii, tunataka kuanzisha viwanda, huduma nyengine, kwa hivyo ukiwa huna umeme wa uhakika shughuli hizi zinaweza kukwama. Kwa hivyo, nashukuru naunga mkono wazo hili la serikali la kuimarisha huduma za umeme wa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa barabara za lami ni agenda ambayo kwa muda mrefu imekuwepo bado inaendelea kuwepo, serikali imejitahidi sana kujenga barabara za lami na inaendelea namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa juhudi zao za kuimarisha ujenzi wa barabara za lami.

Mhe. Naibu Spika, aidha katika mambo ambayo yamepewa kipaumbele ni kuimarisha ujenzi wa viwanja vya ndege, bahati nzuri hii kazi inaendelea vizuri sina matatizo nayo naunga mkono shughuli ziendelee.

Lakini uchumi wetu za Zanzibar kwa sababu nchi yetu ni ya visiwa inategemea sana ubora wa viwanja vya ndege na ubora wa bandari yetu. Kwa bahati nzuri shughuli za ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea vizuri na tunatarajia katika miaka mitano mpaka kumi ijayo abiria wetu wataongezeka zaidi.

Nilisoma pahala jana kwamba sasa hivi duniani nchi za Pacific na Asia zinakamata soko la asilimia 40 kwa usafiri wa anga, wamezitoa kutoka nchi za Amerika ya Kaskazini na Ulaya wamechukua wao na kwa sababu ya nchi ya China na Hong Kong. China yenyewe inachukua asilimia 38 ya soko la usafiri wa anga kwa nchi za Asia peke yake.

Sasa ni muhimu na sisi kwetu kujiimarisha zaidi katika viwanja vya ndege na bandari. Uzuri wenyewe ni kwamba hata kwenye bandari tuna mradi wa bandari mpya ya Mpigaduri. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aendelee na juhudi zake pamoja na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakahakikisha kwamba pale Maruhubi Mpigaduri tunajenga bandari mpya.

Mhe. Naibu Spika, eneo lile la Maruhubi Mpigaduri ni eneo ambalo limefanyiwa utafiti na kuonekana kwamba kina chake cha maji ni kizuri zaidi kwa Afrika Mashariki katika ujenzi wa bandari kuliko eneo lolote, labda linafuatiwa na eneo la Pemba kule Mkumbuu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, pale tupatumie kwa shughuli ya ujenzi wa bandari mpya ambayo itakuwa ni kubwa katika eneo hili la Afrika Mashariki na itasaidia kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie pia uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo. Niseme tu kwamba ni vizuri hii nia ya serikali ya uanzishaji viwanda vidogo vidogo na vya kati itekelezwe ili kutoa ajira kwa wananchi wetu na kupunguza utegemezi kwa mataifa ya nje.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wachangiaji ni wengi basi nimalizie kwa kusema mambo yafuatayo. Kwanza mimi kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chumbuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia na pia namuombea mafanikio Mhe. Waziri baada ya upitishwaji wa bajeti hii leo aweze kuyafikia hayo malengo yote ya serikali. *(Makofi)*

Pia niseme tu kwamba bajeti hii ni mwanzo wa utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ya miaka mitano, lakini pia ni utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais wetu. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu na wananchi nilikuwa natoa ombi kwamba tukiona jambo mwaka huu halimo tujue mwakani litakuwemo kwa sababu huu ni mpango wa miaka mitano. Nia njema hairogwi na Mhe. Waziri wetu ana nia njema, kwa hivyo tumpe fursa kwa miaka mitano atuletee maendeleo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata fursa na mimi kuchangia bajeti hii ya serikali ya awamu ya saba inayoongozwa chini ya mfumo wa kimataifa. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa bajeti nzuri aliyoileta katika ukumbi huu. Vile vile niwashukuru na kuwapongeza sana wasaidizi wake wote ambao wametumia umahiri mkubwa katika kutengeneza bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wawakilishi wote ambao tangu siku ya kwanza iliposomwa bajeti hii walikuwa wakakamavu sana katika kuchangia na kwa kweli michango yao ilikuwa mizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba nieleze machache ambayo yamezungumzwa katika hotuba hii ya Mhe. Waziri. Kwanza limezungumzwa suala zima la *Free Port* au Bandari Huru. Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilitayarisha na ilifungua *EPZ,* ikafungua *Free Port,* miradi yote hii kwa sasa iko chini ya usimamizi wa *ZIPA.*

Mhe. Naibu Spika, wengi sana huwa wanajaribu kuzungumza kwamba Zanzibar lazima iwe *Free Port* kwa sababu ndio itakayotuokoa. Sisi tunakubaliana nalo sana suala hilo lakini hatuwezi tu kwenda kichwa kichwa lazima tufanye utafiti wa kina, utafiti wa kutosha kuona kwamba kweli Zanzibar ni viable kwenda katika suala la *Free Port.*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tuwe na subra kwamba tunafanya kazi nzuri sana ya kufanya utafiti wa kina kuona namna gani au mfumo gani ambao Zanzibar utaweza kuwa katika mfumo wa Bandari Huru.

Mhe. Naibu Spika, tayari tumeajiri kampuni ambayo inafanya kazi ya kufanya uchambuzi yakinifu kwa ajili ya kutayarisha maeneo tengefu ya kiuchumi *SEZ* yaani *Special Economic Zone.*

Mhe. Naibu Spika, *Special Economic Zone* ziko nchi mbali mbali duniani ambazo tumeziangalia kwa makini kabisa kama vile India, China, Kenya, South Africa, Mauritius pamoja na Tanzania Bara. Kwa hivyo, *SEZ* inafanyiwa utafiti na baada ya muda mfupi tu tutawaletea wajumbe wataangalia na wao watoe mawazo yao na ikipita tutatunga sheria na itatusaidia katika kuanzisha hiyo *Special Economic Zone.*

Mhe. Naibu Spika, hii *Special Economic Zone* ni *concept* mpya ambayo inaunganisha yote. Katika *SEZ* kutakuwa na *EPZ,* yaani *EPZ* inamezwa inakuwa ndani yake, *Free Trade Zone (FTZ)* imo ndani yake, *Agri Export Zone (AEZ)* imo ndani yake, *Industrial Estate (IE)* imo ndani yake, *Free Port (FP)* imo ndani yake, *Trans Shipment Harbor* na *Urban Enterprises Zone* imo ndani yake, inakuwa ni *umbrella.* Kwa hivyo, *Special Economic Zone* inakumba mambo yote yanayohusu uchumi wa nchi, utalii umo ndani yake.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wawe wastahamilivu ili ripoti ya mwisho kabisa ya *Special Economic Zone* ipatikane tuijadili na tuone kwamba ikiwa Zanzibar iko *viable* basi tutakwenda moja kwa moja katika

suala hili na naamini kwamba litaweza kuchechemua chemchem zote za kiuchumi za Zanzibar na Zanzibar itakuwa ni kitovu cha biashara katika Afrika ya Mashariki.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuelezea suala hilo ningeomba nielezee suala la *ZSTC* ambalo limezungumzwa sana hapa na suala zima la zao la karafuu. Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imelenga kuona kwamba shirika la *ZSTC* linafumuliwa na kuwekwa katika mfumo mwengine kabisa. Mifano hiyo ipo hai kwa sababu Shirika la Bima la Zanzibar lilifumuliwa na sasa hivi linakwenda vizuri tu, Benki ya Watu wa Zanzibar nayo ilifumuliwa sasa hivi inakwenda vizuri.

Kwa hivyo, nawaomba wawakilishi wawe katika mkao wa subra tayari tumeshamuajiri mwandamizi ambaye anafanya kazi kubwa kabisa ya kuliangalia shirika la *ZSTC* na kuona tutumie njia gani ya kulifumua na kulijenga shirika ambalo litaweza kuwa shirika madhubuti la kuweza kuendesha biashara ya karafuu bila ya matatizo yoyote.

Katika shirika la *ZSTC* tutafanya mambo mengi sana na tutabadilisha sheria hasa, itakuja sheria mpya hapa Barazani itapitishwa ili shirika liwe na nguvu, liwe na meno na liweze kufanya kazi zake bila ya matatizo yoyote.

Katika mfumo huo kutakuwa na mfuko maalum wa kuanzishwa mfuko wa maendeleo ya karafuu kwa madhumuni ya kuendeleza zao hili. Yaani Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko itashirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili kuona kwamba zao hili linazidi kufana katika nchi yetu. Kwa sasa hivi tunatoa kama tani 4,000 mpaka 5,000 kwa zao kubwa kwa mwaka ambapo tulikuwa tukitoa zaidi ya tani 10,000 miaka 15 iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia nchi ya Madagascar sasa hivi inatoa tani 12,000 kwa mwaka. Kwa hivyo, lengo ni kuona kwamba tunarejesha uzalishaji wa zao la karafuu ili ufikie angalau tani 10,000 na zaidi katika upatikanaji wa karafuu nchini.

Kwa sasa hivi nchi saba zinazotoa karafuu duniani ikiwemo Zanzibar zinatoa tani 110,000 za karafuu. Indonesia tani 80,000, India tani 2,500, Madagascar tani 12,000, Sri Lanka tani 6,000, Comoro tani 700, Brazil tani 6,000 na Zanzibar tani 5,000.

Kwa hivyo, karafuu zinazotoka duniani ni hizo na sisi tunayo nafasi ya kuongeza utafiti wa karafuu na hiyo ndio azma tutakayoifanya kuona kwamba karafuu tunaongeza kutoka tani 5,000 hadi kufikia tani 12,000 au zaidi.

Malengo haya yatatimizwa baada ya kumaliza suala zima la ukarabati wa *ZSTC* ambapo tutahitajia msaada mkubwa wa wawakilishi wa Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika. Magendo ya karafuu yamezungumzwa kwa kiasi kikubwa hapa katika mjadala wetu. Wizara yetu pamoja na shirika la *ZSTC* tunajua kwamba magendo ya karafuu yanaathiri sana uchumi wetu na ipo haja ya kuweza kudhibiti magendo ya karafuu na kuyamaliza kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana nasema kwamba kwa muda wa miaka 10 kuanzia mwaka 2001 hadi 2010 Zanzibar imeweza kuzalisha tani 40,838 za karafuu. Kwa bahati mbaya sana asilimia 25 ya karafuu hizo zimesafirishwa kwa magendo, tani 9,510 zimesafirishwa kutoka nchini Kenya, hili ni jambo la kusikitisha sana. Sisi tumedhamiria kabisa kuona kwamba tunatumia kila njia inayowezekana kuzuia magendo haya yasiendelee.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2009 Kenya imesafirisha tani 2,269, mwaka 2008 Kenya imesafirisha tani 1,345, mwaka 2007 Kenya imesafirisha tani 7,494. Ukiangalia utakuta nchini Kenya hakuna hata mkarafuu mmoja.

Mhe. Naibu Spika, mvunja nchi ni mwananchi na mjenga nchi ni mwananchi. Natoa wito kwa wananchi wote tushirikiane kwa umoja wetu kuona kwamba karafuu zetu zinatufaa sisi wenyewe tunaziuza katika shirika la *ZSTC*.

Kwa upande wa shirika la *ZSTC* kupitia Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko tutahakikisha kwamba tunatoa bei nzuri sana ya karafuu. Kama alivyoahidi Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dk. Ali Moh'd Shein kwamba tutatoa bei nzuri kwa wakulima basi na mimi naahidi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba tutatoa bei nzuri sana kwa wakulima.

Kwa wito huo naomba Wazanzibari wote tushirikiane kuona kwamba karafuu zote tunaziuza sisi wenyewe na hatuzisafirishi kupeleka nje ya nchi wala itakuwa hatuna sababu ya kufanya hivyo. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekosa mapato kwa muda wa miaka 10 ya jumla ya dola milioni 16 kupitia nchi jirani, hii ni hasara kubwa kwa taifa. Lazima tushirikiane kuona kwamba zao la karafuu tunaliuza sisi wenyewe na tunaahidi kwamba bei ya karafuu itakuwa nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mengine yaliyozungumzwa hapa kwa urefu ni suala zima la kwa nini vyakula vinapanda bei sana na mafuta vile vile. Nimeelezea katika swali nililojibu hapa leo lakini nikitaka tu kueleza bayana kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba ongezeko la bei za bidhaa nchini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haijafunga mikono au kuweka mikono juu kwamba imesarenda hapana. Wafanyabiashara wetu tumewaita na wamekuja na tumekaa nao tumezungumza nao na kwa kweli hawana tatizo lolote ni watiifu kabisa kwa

serikali yao na wamechukua maagizo yote. Tumekaa nao pamoja tumeangalia masoko yote ya bidhaa zote muhimu kama mchele, sukari, unga na hata mafuta ya kupikia.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tunatumia kama tani 61,000 za mchele kwa mwaka, katika hizo tani 53,000 zinatoka nje, ndani tuna uwezo wa kuzalisha tani 8,000 tu. Sukari tunaagiza tani 30,000 na unga wa ngano tunaagiza tani 42,000. Takriban wafanyabiashara wanatumia milioni 92 mpaka milioni 100 kwa mwaka kwa kuagiza bidhaa hizi kutoka nje. Soko la bidhaa hizi ni moja duniani na bei ya mchele tunakonunua sisi ndiko wanakonunua watu wote duniani. Suala kubwa ni kwamba bidhaa hizi zimeongezeka bei katika soko la dunia ambapo imepelekea na sisi huku bei zetu za bidhaa kuzidi.

Tumekaa pamoja na wafanyabiashara tumetathmini hali halisi ilivyo tumezungumza nao tumejadiliana na tumeafikiana kiasi gani ya faida wachukue. Kwa kweli wameridhika na inshaallah kanuni tumeshazitunga naamini kwamba katika wiki hii tutazitia saini tutazitangaza. Kwa hivyo, bei za vyakula tutakuwa tunajadiliana baina ya wizara yetu pamoja na wafanyabiashara, haitokuwa mfanyabiashara usiku analala asubuhi akiamka akapandisha bei ya bidhaa. Lazima kama bidhaa itapanda bei basi itapanda bei kwa sababu zitakazokubalika.

Kwa hivyo, serikali haijafunga mikono tu ikaangalia bei zitapanda lakini tunaangalia vigezo vyote vinavyosababisha kupanda kwa bei. Kama nilivyoulizwa katika maswali kwamba bei imepanda kutokana na ukosefu wa bidhaa hizi katika soko la dunia kupanda bei, la pili uharamia uliopo katika Bahari ya Hindi na tatu kupanda kwa bei za mafuta katika dunia.

Serikali haijapandisha ushuru wa bidhaa yoyote ile na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inajitahidi kama inavyowezekana kuona kwamba bidhaa hizi hazipandishiwi kodi kiholela na bei ya kodi ni ndogo sana, yaani shilingi ishirini kwa kilo moja ya mchele.

Mhe. Naibu Spika, naomba wawakilishi wote wajue kwamba serikali inafanya kazi juu ya suala hili la kupanda bei kwa bidhaa na hatutokubali kuona kwamba mfanyabiashara anapandisha bei za bidhaa kiholela.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii ni bajeti ya wananchi, kwa ajili ya wananchi na kwa maendeleo ya nchi. Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Saba yenye mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeangalia namna gani ya kuwajali wananchi na ndio maana ukaona kwamba imeangalia masuala yote yanayowagusa wananchi. Kuanzia mishahara ya wafanyakazi kwenda katika upatikanaji wa maji safi na salama na kilimo ili tuweze kutokana na shida hii tuliyonayo sasa

hivi ya kupanda bei bidhaa. Tunaamini kwamba kwa bajeti hii tukijidhatiti sote kuisimamia kwa pamoja kutekeleza majukumu yote basi tutaweza kuvuka mkondo huu mkubwa uliopo dunia nzima kwa upandaji wa bidhaa zote kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Naibu Spika, wito wangu ni kwamba viongozi sote pamoja na wananchi wote tuwajibike kufanya kazi zetu ipasavyo. Tukiwajibika sote tukifanya kazi zetu kwa moyo mmoja na kwa imani moja na tukiendelea kushirikiana kwa pamoja basi nchi yetu itaweza kuvuka katika mkondo huu *inshaallah wataala.*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi binafsi na kwa niaba ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Jimbo langu la Mtoni tunasema kwamba tunaiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mia fil mia nasema kila la kheri ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya serikali iliyowasilishwa hapa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii aliyotupa ya amani na utulivu leo tuko hapa tunachangia bajeti hii ya serikali kwa nguvu zetu sote kwa lugha zinazofanana. Tokea tumeanza kuchangia mpaka sasa hivi mwelekeo ni kwamba bajeti hii tumeipokea na tutaikubali ili sasa zile wizara nyengine ziweze kutekeleza na kupanga shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imepewa majina mengi kwa ajili ya furaha ambayo tunayo. Mimi niliita bajeti ya wakulima na wafanyakazi na nina sababu zangu. Bajeti hii ya wakulima kwa sababu sekta ya kilimo imezungumzwa vizuri na Mhe. Waziri ameipa kipaumbele cha kutosha na katika ziara aliyofanya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kokote nilipokwenda Mhe. Mansoor Yussuf Himid alikuwa anawaambia wananchi wamsikilize tarehe 15 nafikiri wakati atakapotoa bajeti yake.

Zaidi alikuwa anawa-*address* wakulima katika yale mabonde tuliyokuwa tunakwenda wanasema mbolea ghali, dawa za magugu hatuna na kadhalika. Mhe. Mansoor Yussuf Himid yeye alikuwa anawaambia sikujibuni sasa hivi sikilizeni bajeti yangu tarehe 15. Lakini Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameanza kutoa *indication* kwamba serikali imetoa kipaumbele sana.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais alikuwa anazungumza kwamba anataka kufanya mapinduzi ya kilimo. Wenzetu Tanzania Bara wanasema kilimo kwanza sisi tunasema mapinduzi ya kilimo. Sasa ndio maana bajeti hii nikasema ya wakulima. Pia bajeti hii ya wafanyakazi kwa sababu Mhe. Waziri amesema amepunguza au ameongeza mishahara halafu ameweka kwenye mabano akasema waziri mhusika atakuja kueleza vizuri. Lakini ametoa *indication* kwamba nyongeza zenyewe zitakuwa ni nzuri. Sasa kama si bajeti ya wakulima na wafanyakazi basi ni bajeti ya nani. Sasa mimi naipa jina hili bajeti ya wakulima na wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, nitoe wito kwa sababu bajeti hii inasema haitapandisha kodi. Mhe. Naibu Spika, tumemsikia Mhe. Waziri hapa akizungumza na naomba iwe hivyo ahakikishe wakulima hawaongezi bei za vyakula kiholela maana hakuna kodi iliyoongezwa. Kwa hiyo, kama hatuongezi kodi kwa manufaa ya wananchi basi wana wa nchi hii wanufaike wasinufaike wafanyabiashara peke yao.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti alipokuwa anasoma hotuba yake alizungumza vizuri suala la ukuaji wa uchumi, maana wengi wanazungumza uchumi huu unakuwa vipi. Hata kwenye kikao hichi walizungumza mbona hatuoni mafanikio, mbona hatuoni mabadiliko, mbona hatuoni hiki. Sasa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti alitoa tafsiri safi sana na sina haja ya kwenda mbali zaidi huku ku-*elaborate* tafsiri ile lakini yeye alisema uchumi unakua na unaonekana. Mimi nataka nimuunge mkono uchumi unakua na unaonekana.

Unaonekana kivipi, kuna aina mbili za kupima ukuaji wa uchumi. Moja ni hii tunayosema uchumi unakua kwa kulinganisha, kama alivyotuambia mwenyewe waziri kulinganisha uzalishaji na shughuli za maendeleo au uzalishaji na ufanisi wa kazi za huduma. Akasema utakapovilinganisha vitu viwili ukiviweka pamoja, sasa hapo ndipo utaona uchumi unakua au haukuwi.

Ni kweli kabisa Mhe. Naibu Spika, hatuzalishi sana katika viwanda, lakini bado takwimu za kilimo zinaonesha ukuaji wa uzalishaji wa kilimo umeongezeka. Vile vile juhudi zinazochukuliwa na serikali pamoja na Wizara ya Kilimo na Maliasili yenyewe inaonekana kwamba mkazo umewekwa sana katika utafiti na tunaweza sasa kuvumbua mbegu ambayo itatupa matumaini makubwa.

Kwa hivyo, kazi iliyobakia kwenye kilimo zaidi ya haya yaliyozungumzwa kwenye bajeti hii, lakini tuweke mkazo tena mkubwa katika umwagiliaji maji. Tukifanikiwa katika hilo, kweli uchumi utaonekana maana chakula kitazalishwa kwa wingi.

Mhe. Naibu Spika, kuna aina nyengine ya kupima uchumi kama unakua au haukuwi. Aina hii inaitwa mabadiliko ya maendeleo yanayoletwa na nchi na serikali kwa wananchi. Sasa kipimo hiki ni kipana zaidi kuliko hata kile kipimo tunachokitumia. Kipimo hiki kinakusanya harakati za elimu, ujenzi wa barabara, ujenzi wa miundombinu, bandari na kadhalika. Ukivipima vyote hivi na kuvitia kwenye mizani na ukiviangalia vinabadilika au havibadiliki.

Mhe. Naibu Spika, yeyote mwenye akili na macho ya kuangalia basi atakuambia vinabadilika. Barabara tulizonazo sasa ni nyingi kuliko tulizokuwanazo miaka mitano iliyopita. Elimu taaluma imeongezeka, wasomi wameongezeka, vyuo vikuu vimeongezeka.

Ukipima hayo na mengine mengi katika hayo *human development index* ndio kipimo safi sana kitakachokuambia uchumi unabadilika au haubadiliki na kama unabadilika unawanufaisha wananchi au hauwanufaishi. Barabara inawanufaisha wananchi, umeme unawanufaisha wananchi, elimu, afya na kadhalika. Kwa hivyo, uchumi unakuwa na unawanufaisha wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nampa pongezi sana Mhe. Waziri, kama wenzangu waliotangulia, lakini mahususi pongezi yangu inakuja katika uchambuzi wake aliotuambia jinsi taathira iliyoukuta uchumi wa dunia. Ni kweli kuna mtikisiko mkubwa sana wa uchumi wa dunia na umetugusa takriban sote, kwa sababu sasa hivi tumefungamana dunia nzima kiuchumi. Wataalamu wanasema dunia sasa ni kijiji. Akienda chafya Mmarekani basi Mzanzibari anapata mafua, kwa sababu ya mfungamano wetu.

Kwa hivyo, maelezo aliyotupa Mhe. Waziri kabla hajatupa maelezo ya athari ya uchumi wetu, yalikuwa ni maelezo safi sana, uchambuzi mzuri sana, Mhe. Waziri mimi nampongeza sana. Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni nimesoma makala moja ya uchumi, inayozungumzia kwamba Muungano wa Uchina, Urusi na Mashariki ya Mbali sasa utaleta ule tunauita ulimwengu wa tatu.

Tulikuwa na ulimwengu wa kwanza baada ya vita vya pili vya dunia, Mmarekani ndiye alikuwa mbabe ana pesa nyingi, ana vifaru vingi, ana vifaa vingi na uchumi wake umekuwa sana kwa sababu hawakujiingiza katika vita vya dunia, wao waliingia katika biashara ya vita vya dunia. Kwa hivyo, Mchina, Mrusi na Mashariki ya Mbali imepata mchupo mkubwa sana ya ukuaji wa uchumi katika nchi hizi. Kwa kweli tumebahatika moja katika nchi hizi ni marafiki zetu sana sisi Wazanzibari naye ni Mchina. Nitakuja kutoa maelezo wakati wa kusoma bajeti yangu tarehe 9/7/2011, lakini sio vibaya nikisema sasa hivi.

Kutokana na ukaribu wetu, kutokana na uwezo wao wa uchumi yaani tatizo la maji wameliangalia kwa ukubwa na kwa upana sana na *Inshaallah* huwenda kama nilivyosema mwaka 2013 hili tatizo litakuwa limeondoka mara moja na kwa miaka yote. Kwa hivyo, wenzetu hawa wanasema wataunda ulimwengu wa dunia ya tatu na kwa bahati nzuri sasa hivi. Haa! sio bahati nzuri kwa bahati mbaya wenzetu wakubwa Marekani na *European Union* wamejiingiza katika vita vya *Middle East.* Wanatoka nchi moja wanakwenda nchi ya pili, wanatoka nchi ya pili wanakwenda nchi ya tatu. Sasa hivi sijui wako Libya au wako Tunisia, wako Yemen, wako Syria. Ilimuradi wanautawala ulimwengu wa *Middle East* kivita.

Kwa hivyo, bila shaka utafika wakati watamaliza nguvu zao wa utajiri, hawa wenzetu watatu Wachina, Warusi na Waindia watapanda juu na Mwenyezi Mungu awajaalie wapande juu kwa njia ya kuzisaidia nchi za ulimwengu unaoendelea, nchi za kimaskini. Sasa uchambuzi alioutoa Mhe. Waziri, unalingana sana na mchambuzi huu ninaozungumza uliotolewa katika vyombo vya habari na vyombo vya maandishi na tuweke tamaa kubwa sana kwamba nchi zetu zitaendelea.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri katika kurasa zake alizozizungumzia kukua kwa uchumi wa Zanzibar. Uchumi unakuwa kwa kuangalia mambo matano muhimu au uchumi unafifia kwa kuambatana na kufifia kwa mambo haya matano muhimu, naomba niyasome.

Kwanza *inflation.* Pili, *unemployment* yaani kutokuwa na kazi. Tatu, huo uchumi wenyewe yaani *growth development index*. Nne, *Capital Income* yaani pato la mwananchi na Tano, ule ukuaji wenyewe wa uchumi yaani *economic growth.*

Katika kitabu cha Mhe. Waziri ametupa hata na michoro inayoonesha ukitizama ukurasa wa 13 wa kitabu hiki cha mapitio ya hali ya uchumi, halafu ukurasa wa 7, 8 na 13 kuna michoro na aina nyengine ya michoro inaonesha *trend* ya kukua sio *trend* ya ku-*fluctuation* kwenda juu na chini au *trend* ya kwenda juu halafu ikaja chini moja kwa moja, inaonesha kuna *trend* ya ukuaji wa uchumi kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika, pato sasa limepungua kwa asilimia 6.1 kama alivyotuambia Mhe Waziri. *Inflation* ina mizengwe mingi, mizengwe ya ndani na mizengwe ya nje. Ikipanda bei ya mafuta basi bei ya vyakula, bidhaa na usafiri inapanda, kwa hivyo *inflation* nayo inaongezeka. Kwa hivyo, hili kwa bahati mbaya hatuna uwezo nalo.

Lakini ukiangalia *inflation* katika sekta ya chakula ya uzalishaji, ndipo hapa tunaweza kupunguza kwa sababu tumezalisha sana na hata Zanzibar tumezalisha sana. Hata uajiri umeongezeka kwa Zanzibar, ingawa kwa asilimia 2.4 lakini umeongezeka. Hiyo ni sekta muhimu sana. Pato letu la taifa limeongezeka, pato la kila mtu limeongezeka. Sasa hizo ndio *indicator* nzuri sana za kuupima uchumi unakuwa au haukuwi. Mhe. Waziri ameueleza vizuri sana kwamba uchumi wetu unakua na *indicator* hizi zote zinaonekana kwamba zinapanda badala ya kushuka, ikishuka ni *inflation*, kwa sababu *inflation* ikipanda ni hatari, kwa hivyo, kilichoshuka ni *inflation* na ni vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie maana mengi yameshachangiwa. Kwanza nataka niwapongeze sana wajumbe wako wa Baraza hili. Kila aliyesimama kuchangia amezungumzia mafuta na gesi asilia. Hii ni dhahiri inaonesha kwamba mafuta yetu hatutaki, hii ni dhahiri inaonesha kwamba uchumi wetu haukuwi kwa haraka kwa sababu bidhaa hizi zimezuiliwa tusizivune.*(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alipochangia hakuchangia kwa hamasa, lakini hata waliochangia kwa hamasa hawakufanya makosa, maana wana *send signal* kwa wenzetu, na *signal* yenyewe wanawaambia wenzetu kwamba tuachieni uchumi wetu na uchumi sio suala la Muungano. Huwezi kunipa gari ukaniambia unanipa zawadi ya gari hii halafu magurudumu ukayatoa ukaniambia niende Donge sifiki. Ukinipa gari unipe na magurudumu na unitilie na mafuta ili nianze kwenda.

Mhe. Ismail Jussa alisema kitu kimoja muhimu sana na hiki tukikumbuke, alisema tupelekeni waraka Bungeni, tukawaambie tukawaambie eneo hili la 15 katika mambo ya Muungano hili litolewe. Nasema ilikuwa ni hoja nzuri sana, kwa sababu unapojadili kutaka chako jenga hoja, jadili kwa hoja, ni chetu kweli lakini tulijadiliana tukitowe tuwape wenzetu wakidhibiti hivyo ndivyo tulivyokubaliana.

Sasa nitachangia zaidi katika bajeti yangu katika sekta ya *energy*, lakini nataka niseme kwamba twendeni Bungeni na sisi tuko wengi kule, sio wengi zaidi ya wao lakini tuko wengi, tukisema tutasikika. Tukatoe shindikizo la kubadilisha katiba wala tusingojee katika wakati wa kubadilisha katiba. Kibadilishwe kifungu hiki nambari 15 tukitowe katika mambo ya Muungano, maana tumeshakubaliana. Tulikubaliana katika Baraza la Mapinduzi na tulikubaliana hapa hapa katika Baraza la Wawakilishi. Tukifanya hivyo wenzetu watatusikiliza, wana mbinu za kutukatalia, maana kulibadilisha hili unatakiwa uwe na *two third majority* ya kila upande. Sasa Wazanzibari sote Wabunge wetu watapiga kura zote watapata asilimia 100, lakini wao wakikataa isitokezee ile *two third* hili suala linaweza likabakia halibadiliki. Sasa hapo ndio tunakwenda kulibadilisha kwa namna tunayotaka sisi.

Mhe. Naibu Spika, nilisema nilizungumze hili, kwa sababu imeshajengeka dhana kwamba Serikali ya Awamu ya Saba inalionea haya suala hili, imeshajengeka dhana kwamba wizara ya nishati ya Zanzibar imeshalionea haya suala hili. Hapana, serikali inaheshimu maamuzi na wizara inaheshimu maamuzi. Maamuzi tushirikiane pamoja tulitowe, wachimbaji mafuta tunao na tumeshawaweka tayari. Nataka nikuthibitishieni Zanzibar mafuta yapo, mafuta yapo Pemba na Unguja, gesi ipo Pemba na Unguja. Hili halihitaji utafiti wala halitaki tochi liko wazi kabisa, tukilifanyia kazi kitaalamu, kisiasa na kiutaratibu basi tutafanikiwa Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mwenyezi Mungu wabariki Wazanzibari wote, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya serikali na baada ya mchango muhimu sana wa jirani yangu hapa, mimi sidhani kama hata hizo dakika kumi nitazichukua zitakuwa nyingi. Mtu akikaa na jirani huwa ana nukia nukia yale mazuri ya jirani. Nilikuwa nakusudia na mimi nizungumzie suala la mafuta, lakini kwa kibwagizo alichomalizia, mimi nadhania nisiliguse maana nitaondoa ule utamu wote wa kibwagizo chake.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba namuunga mkono sana na ninawaunga mkono wote waliozungumzia suala la rasilimali hii muhimu kwa maslahi ya nchi yetu. Kwa hivyo, ni jukumu letu pamoja kuona kwamba pale tulipoanzia katika Baraza lililopita basi tunaendeleza kwa maslahi ya watu wote.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa bajeti yake na mipango yake mizuri ya mwaka huu. Ni kweli kwamba mipango aliyoiandaa na kutuletea hapa kama tutashirikiana katika kuisimamia basi ni dhahiri kwamba baada ya mwaka mmoja patatokea mabadiliko makubwa katika uchumi wa nchi yetu. Kwa hivyo, la msingi ni kwamba sote tumuunge mkono na tumsaidie katika kutekeleza yale yote ambayo ameahidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono sana hotuba yake. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru Mhe. Waziri anayeshughulikia fedha katika mambo matatu au manne ambayo Waheshimiwa Wajumbe hapa waliyazungumzia. Kwanza ni suala la mwani, yeye binafsi Mhe. Waziri alikuwa hafurahishwi hata kidogo na namna biashara ya mwani inavyokwenda na bei yake na namna ya uduni wa nyenzo zinazotumiwa na wakulima wetu. Amekuwa mstari wa mbele na amekuwa akinishauri sana namna gani ya kutafuta namna ya kuondokana na hii hali. Kwa hivyo, mimi naomba

nimpongeze katika hili na naomba tuendelee kushirikiana kuona kwamba yele ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza letu la Wawakilishi wamezungumzia kuhusu suala la mwani, basi hatimaye tunapata ufumbuzi kwa maslahi ya wananchi wetu ambao kwa kweli wanapata tabu sana kwa shughuli hii. Kwa hivyo, bado tutaendelea kushirikiana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la nyenzo za uvuvi wa bahari kuu. Hili nalo Mhe. Waziri amekuwa akilisimamia na kunisukuma mimi kama waziri wa sekta hii kuona kwamba tunawaondoa wavuvi wetu kutoka hapa walipo. Kwa hivyo, nampongeza na namshukuru sana na bado naahidi kwamba tutaendelea kushirikiana ili ile kiu ya wawakilishi kwa niaba ya wavuvi wetu tuone kuwa tunaondokana na matatizo haya.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka miezi miwili iliyopita tulilizungumza kwa kina sana suala la hali ya biashara ya dagaa katika visiwa vyetu. Aliniambia kwamba tunaonekana tunapoteza mapato mengi kutokana na suala hili kwa sababu ni biashara ambayo imeshamiri sana. Ukienda pale Maruhubi utaona hali ya wanawake wengi wameshughulika na hii biashara, Kaskazini ya Unguja kama alivyosema jana Mhe. Panya ni kweli, lakini pia hata pale Kusini Pemba maeneo ya Ndagoni. Serikali kushirikia na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tunaangalia namna gani ya kutafuta viwanda vidogo vidogo usarifu wa bidhaa hii. Kwa hivyo, bado Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika hili ana mkono wake na amekuwa akitushauri na kutusukuma katika kuelekeza hili. Kwa hivyo, hapo nataka nimpongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la ulipwaji wa fidia na hasa wa ujenzi wa barabara. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kweli ndio inayo *custodian* mikataba mingi ya ujenzi wa barabara na mtekelezaji ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Lakini katika utekelezaji wake kuna suala la ulipwaji wa fidia wa majumba na vipando, suala hili kwa kiwango kikubwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imekuwa ikilitekeleza, lakini nahisi kuna eneo ambalo bado tushirikiane zaidi, kwa sababu wananchi wetu hupenda fidia waipate mapema ili waweze kujiandalia mazingira ya kupisha miradi hii itekelezwe vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka juzi tulikuwa Gando na Mhe. Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein na wananchi kwa kweli walifurahi na kumpongeza sana Mhe. Rais kwa namna ambavyo barabara ile ya Wete Gando inavyoanza kujengwa. Lakini walikuwa na masikitiko kidogo kwa namna ambavyo fidia inachelewe kutolewa au inatolewa muda mfupi kabla ya kutakiwa kuhama na barabara ile itekelezwe. Kwa hivyo, kwa niaba yao wananchi wa Gando

naomba niungane nao ili kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika hili kidogo achacharike ili kuona kwamba fidia zinapatikana mapema ili wananchi waweze kuhama mapema ili kupisha miradi ile kutekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, nilikuambia mimi sina mchango mkubwa nilikuwa naomba nitie baraka tu, ili kumpongeza Mhe. Waziri katika bajeti yetu na tuombe tuipitishe kwa pamoja na zaidi tumsaidie Mhe. Waziri pamoja na serikali katika utekelezaji wa bajeti yake. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kupata dakika chache hizi kuzungumza machache sana katika hotuna hii ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Waziri wenyewe ana usemi wa kwamba .'kupokezana vijiti'. Mimi nasema kijiti kakipokea vizuri na anaiendeleza rilei vizuri sana, nampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi niungane na wenzangu kuunga mkono moja kwa moja hotuba hii nisije nikasahau. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dimani naiunga mkono hotuba hii moja kwa moja kwa asilimia mia moja. Kwa sababu kule kuna barabara ya maeneo huru na barabara ile ni sehemu moja ya uchumi na tunazungumzia kuongeza uchumi, basi namkumbusha tu Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba maeneo yale ya uchumi, kuna ahadi ya barabara ile kuitengeneza basi namuomba asilisahau hilo.

Mhe. Naibu Spika, kumsaidia waziri kwa sababu na mimi ni mkulima, waheshimiwa walizungumza sana suala la kufa mikarafuu wakati imepandikizwa shambani. Kwa sababu na mimi nina utaalamu kidogo wa kilimo na pia ni mkulima naomba nimsaidie tu kwa haraka haraka kwa hizi dakika chache ulizonipa.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba mikarafuu ukiitoa kwenye kitalu na kuipeleka shambani, basi ukipata asilimia 50 wewe kwa kweli ni bingwa. Mhe. Naibu Spika, wewe mwenyewe ni shahidi ulisema umepata miwili, mimi nilikuzidi kidogo. Mwaka jana nilipanda miche 300, Alhamdulillah miche 160 nimefanikiwa. Siri ni moja tu na utaalamu, Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili hayupo lakini nitamsemea kwa niaba yake kwamba utaalamu na huu utafiti umefanywa upo na siri yenyewe ni kwamba kule shambani kabla hujapandikiza kwanza uweke hali ya kivuli, hiyo hali ya kivuli utafanya vipi.

Hali ya kivuli ni upande mihogo hizi kabila kubwa kama kaniki, ndege au *agriculture* unapanda kiasi cha miezi sita, halafu ndio unakuja kuipanda hiyo mikarafuu sasa, ukishapanda mikarafuu ile miaka miwili ya mwanzo, ile ni mbegu kubwa za muhogo usiung'owe basi ile mikarafuu mikarafuu wakati iko michanga inalelewa na kivuli utavuka nayo. Kwa mfano, umekosa muhogo hata ile migomba mirefu kama vile kijakazi au mlali maua ama mtikwe, yaani ile mirefu kabisa unaipanda. Sasa ukesha kuipanda kivuli inaki-*establish* na halafu njoo utie mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, hata Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi alizungumza juzi na tumeona mashamba ya mikarafuu pamoja na mikarafuu michanga. Kwa mfano, kulikuwa na shamba moja la ushirika ambalo limependeza na limejaa mihogo, migomba pamoja na hiyo mikarafuu michanga, yaani mizuri tena imestawi na huo ndio utaalamu wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nasema sisi kama Wawakilishi ambao tunao ujuzi kidogo wa kilimo na tunaweza kuwasaidia wenzetu na tuko tayari hata kwenda shambani kwa ajili ya kufanyakazi nao. Vile vile kulikuwa na suala ambalo waheshimiwa walichangia kuhusu JKU, kwamba vijana hivi sasa hawapiti kama ipasavyo na wengine wanachukuliwa JKT na ule utaratibu umebadilika.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba JKU na JKT lengo lao ni moja la kuwatayarisha vijana, yaani kuwafunza mambo ya amali kama vile mambo ya kilimo, ufundi pamoja na taaluma nyengine, ili wakati wanapomaliza waweze kujitegemea.

Sasa tunapowapeleka JKT wale hawatobakia kwenye kazi hiyo, isipokuwa kule wanakwenda kujenga taifa, yaani ni Jeshi la Kujenga Taifa na wala hawaajiriwi kule na JKU ni hivyo hivyo. Kwa hivyo, wanaporudi hapo ndipo wanapojitafutia wenyewe kazi zao ama kama zinatokea nafasi basi zinatafutwa, kwa sababu sio kama tunawapeleka JKU kwa ajili ya ajira si hivyo, nadhani Waheshimiwa Wajumbe tunalifahamu isipokuwa nimeona tukumbushane tu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kulikuwa na mchango kuhusu Baraza la Manispaa haitimizi wajibu wake. Kwa kweli nakubali, lakini nasema linatimiza wajibu wake isipokuwa labda hatukamilishi wajibu wake ipasavyo. Hili sifichi na sote tumesikia na hata Mhe. Rais ametueleza kwamba Mji wetu mchafu. Kwa hivyo, Baraza la Manispaa hivi sasa tunajipanga vizuri na tumeona kabla ya huu mradi mkubwa ambao Mhe. Waziri ameueleza kwa ufasaha kabisa, basi tumeona tujipange kabisa ili mradi ikija sisi tunauchukua mradi na wala sio mradi uje utuchukue sisi. Kwa maana hiyo, sasa tunaanza kujipanga kwa ajili ya kuanza hizo kazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Manispaa kila siku linazalisha tani za taka 216 na uwezo walionao Baraza la Manispaa wa kuzizoa taka hizo ni asilimia 45 tu. Kwa maana hiyo, uwezo wa Baraza la Manispaa wa kuzoa taka ni tani 96 kwa siku, ambapo ni sawa na asilimia 45. Sasa taka nyengine zinakwenda wapi, ndizo zile tunazoziona zinarundikana na nzi wanang'ong'a pamoja na mambo mengine.

Sasa lazima tukiri kwamba kweli kuna mapungufu makubwa. Mhe. Naibu Spika, wizara tunajiandaa na tunajipanga vizuri na tunajitahidi tuweke watu wazima ambao wanaoweza kufanyakazi, yaani vijana na wala ambao hawawezi kazi basi tutawaambia wafanyekazi nyengine.

Lakini kubwa huu mradi unaokuja nadhani utatusaidia sana, kwa sababu mbali ya moja hii ya kazi ya taka, pia utajenga uwezo kama kitabu kilivyoeleza vizuri kwamba utajenga uwezo wa Baraza la Manispaa, Mji Mkongwe pamoja na Mabaraza ya Miji ya Pemba ya Wete na Chake-Chake.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka Mhe. Abdalla Juma Abdalla alizungumza kwamba mbona wao wamepewa fedha kidogo. Nafiriki niseme kwamba fedha sio kama wamepewa kidogo tu, isipokuwa fedha zile zimekwenda kule kwa mujibu wa maandiko au shughuli zilivyowekwa na hivyo ndivyo ilivyokwenda. Kwa kweli mradi tumeubuni pamoja na kuandika wenyewe na hata huo mgao wa fedha ukaja kwa ajili ya hizo shughuli zenyewe, kwa hiyo sio kama zimekatwa tu hizi za Unguja na zile za Pemba, isipokuwa kwa mujibu wa shughuli zenyewe.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Mohammed Said Mohammed alisisitiza suala la Migombani kwamba na wao wasisahauliwe kwenye huo mradi mpya. Kwa kweli hawatosahauliwa kwa sababu kwenye kitabu imeandikwa kwamba *Botanical Garden* hii michirizi itajengwa na kule Jang'ombe kwa Bint Amrani kote kule michirizi hiyo na ninasema kama kitabu kilivyoandikwa vizuri tu tena kwa ufasaha sana.

Mhe. Naibu Spika, kilimo kwa ujmla. Kwa kweli mimi nimefurahishwa sana kama Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine walivyozungumza kwamba kilimo tukipe kipaumbele na tuwasaidie wakulima wetu.

Hili ni suala la msingi kwa sababu bila ya chakula japo tunaagiza kingi, lakini bado wananchi wetu wengi wao kazi yao kubwa ni kilimo, kwa hiyo tuwasaidie kwani ile tija wanayopata hivi sasa kutokana na kilimo ni ndogo. Kwa maana hiyo, kuna haja ya kuwaongezea zaidi mapato.

Mhe. Naibu Spika, vitabu hivi vina picha nzuri sana vyote ukiviangalia nyuma, yaani vyote vinaonesha kilimo, kitabu cha kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar anangalia Shamba la Darasa la Mihogo na kitabu cha hotuba chenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar anaangalia Bonde la Mpunga.

Sasa hapa nataka kuzungumzia kuhusu hili Shamba la Darasa la Mihogo na huu ni ukombozi, yaani hizi zinaitwa (*Farm Field Schools*) na haya ni mafundisho ya kilimo ni *agriculture extension* na utaalamu wote unatolewa hapa na wakulima wetu wengi utaalamu wao ni mdogo. Kwa mfano, matumizi ya mbolea ni madogo na hata kupanda kwa miongo tumesahau kidogo na wao wanaijua miongo yao, lakini mbegu bora hatuwapelekei kwa wakati.

Kwa hivyo, tukishirikiana kwenye Shamba Darasa kwa ajili ya kuwafundisha na sisi kama Waheshimiwa Wawakilishi, basi ningeomba sana kwamba tujitahidi tuwe na wananchi wetu ambao wengi ni wakulima kwa haya Mashamba Darasa na kweli yatatusaidia sana.

Mhe. Naibu Spika, umetupa muda tunataka tumsaidie Mhe. Waziri ili asije kuchukua masaa mawili tena. Lakini itabidi tuache mengine atakuja kuyaweka sawa mwenyewe.

Naomba nimalizie Mhe. Naibu Spika, kwa kutilia mkazo sana suala la Elimu ya Amani. Kwa kweli elimu nayo imepewa kipaumbele katika bajeti yetu, kwa sababu suala la Elimu ya Amali ni jambo la msingi sana, kwani vijana wote wanaomaliza hawa hatuwezi kuwachukua kwenye kazi za serikali, isipokuwa tuwatayarishe waweze kujiajiri wenyewe. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuona kipaumbele hiki kinatiliwa mkazo.

Vile vile ninashauri mbali ya Skuli ile ya Vitongozi na ile ya Mkokotoni na hizi *Secondary Schools* ambazo tayari tunazijenga za Benki za Dunia. Lakini naomba sana hivi Vyuo vya Amali viwe vingi.

Kwa mfano, wenzetu nchi za nje wanavyo vyuo kama hivi wanaviita *Polytechnic* na mule wanafundisha ufundi kama vile Skuli ya Ufundi Mikunguni na Chuo cha Karume Mbweni, yaani anaondoka pale na ujuzi na siku hizi kuna mahoteli kampuni na wanajiajiri. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika nimeona nitilie mkazo sana suala hili.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho kabisa na mimi nitakuwa sijawatendea haki wenzangu nikinyamaza kimya nisipoongeza sentensi moja kuhusu suala la mafuta. Mhe. Waziri mwenyewe amemaliza na mimi nataka kusema moja tu, kwamba tulisomesha na kufundishwa darasa na wataalamu kwanza kutafutaji na tukathibitisha mpaka uchimbaji pale kuna muda kidogo.

Sasa sisi hata ile kutafuta tumesita na Mhe. Waziri amesema yanafoka yapo kwenye. Lakini kuna mambo yake pamoja na taaluma, najua amejiandaa vizuri, isipokuwa naomba kusema Mhe. Naibu Spika, kuwa tuanze na wala tusisubiri, kwa sababu sisi tumesita na wenzetu kule mambo ya magesi. Kwa mfano, kusini Tanzania nasikia wamepata visima vipya ambavyo vinavyozalisha gesi mara dufu, lakini sisi kuyatatufa tu tumesita mpaka lini. Kwa maana hiyo, Mhe. Naibu Spika na sisi tuanze. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia napenda nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa hotuba yake nzuri ambayo inatoa muongozi wa namna ya utoaji wa huduma za jamii kwa wananchi. *(Makofi)*

Muongozo huu naamini ulikuwa na malengo mawili. Kwanza ni kuwanyanyua wananchi katika shughuli zao za kiuchumi pamoja na kunyanyua kipato chao, lakini zaidi kuhusu suala la wafanyakazi ni kuwaongezea mishahara na maslahi yao kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, hatua hii ni nzuri sana kama ilivyooneshwa kwenye hotuba yenyewe, pia hotuba hii ilielezea mambo mengi yanayohusu masuala ya afya, kilimo, biashara pamoja na sekta nyengine ambazo zote hizo zilikuwa zina lengo la kusaidia wananchi wetu kwa ujumla. Lakini kwenye hotuba hii pamoja na michango Waheshimiwa Wajumbe walizungumza masuala mawili makubwa, ambayo yalikuwa yanahusu katika Wizara ya Katiba na Sheria. Jambo la kwanza ambalo lilipata mjadala mkubwa ni kuhusu muungano.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli napenda nikiri kwamba kuna matatizo kwenye muungano wetu na matatizo haya yapo, lakini kama nilivyozungumza mwanzo kwamba masuala haya tunajaribu kuyashughulikia kidogo kidogo na ndio maana serikali ikaunda Kamati hizi za Mawaziri kutoka Jamhuri ya Muungano na Zanzibar, ili kujaribu kuyarekebisha matatizo haya ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, hapa kitu ambacho ninapenda kukisema ni kwamba hivi sasa kuna suala zima la mchakato wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli mchakato huu ni nafasi pekee ya Wazanzibari kuweza kuweka yale matatizo yote ambayo wanahisi ni ya Muungano, ili hapo ambapo Tume ya Kutafuta Maoni ya Katiba itakapopita basi waweze kuelezea kinaga ubaga, ili maeneo hayo yaweze ku-*accommodated* katika Katiba mpya.

Kwa hivyo, ombi la kwa wananchi wa Zanzibar kwamba tusiogope wakati huo itakapokuja Tume basi tuwaelezee matatizo yetu yote, kwa sababu hii ndio nafasi peke yake ya Wazanzibari ya kujikomboa katika masuala haya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa wizara yangu tukishirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, sisi ndio serikali tutawaelimisha wananchi wetu masuala haya kwa undani na urefu zaidi, ili kila mwananchi au Mzanzibari ajue matatizo ambayo tunayo na ajue ni kitu gani ambacho tunakitaka kwa ajili ya kuufanya Muungano wetu uwe mzuri zaidi. Kwa hiyo, hilo ni ombi ambalo ninapenda kulitoa kwa niaba ya wizara yangu. *(Makofi)*

Pili lilizungumzwa kuhusu suala zima la sheria. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika sheria ambazo tunazo, kuna sheria nyingi ambazo hivi sasa zimepitwa na wakati na nyengine kwa mfano hazikidhi haja. Kwa kweli hayo, yote tumeshayaona na tunajitahidi katika wizara yetu kujaribu kuyaondoa matatizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, tunachokiomba kwa sababu hivi sasa kuna suala zima la mchakato huo na utaratibu wa utungaji wa sheria hizi ni kwamba sisi tunayo Tume ya Kuchunguza Sheria. Katika tume hiyo anaruhusiwa mwananchi yeyote ambaye anahisi kuwa sheria hii ina matatizo, basi ni vyema na yeye akafika katika Tume ile, kwa ajili ya kueleza maelezo au matatizo yake na sisi kiwizara tutaichukua na kuzingatia na tunaweza kuanzisha katika utaratibu mzima wa kurekebisha sheria hizo.

Kwa kweli sekta hii ni muhimu sana kwa sababu unapopata sheria nzuri na unapopata utekelezaji wa sheria katika utaratibu ambao uliowekwa, basi naamini kuwa amani na utulivu ndio zitapatikana. Sasa unapopata amani na utulivu bila ya shaka maendeleo ya nchi ndio yanazidi kupatikana. Kwa hivyo, ninachokiomba ni kuwa tujitahidi katika kutizama ni mambo gani, ambayo kwa kweli tunahisi yamepunguka katika sheria zilizopo na tuarifiane kiwizara na tuafiriane hata kwenda kwenye Tume ya Kuchunguza Sheria, ili na sisi tuweze kuziandaa na hapo tuwezi kuzirekebisha kwa utaratibu ambao unakubalika.

Mhe. Naibu Spika, tukifanya hivyo naamini kwamba tutafika pahala ambapo sheria zetu zinaweza kuwa nzuri na kukidhi haja na zitakapokidhi haja, basi amani na utulivu utazidi kuwepo na hapo ndipo baraka zitaweza kupatikana kwa wingi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo ambayo ndio mambo mawili muhimu yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo, napenda tena nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ilionesha kutilia nguvu mambo haya ambayo nimeyazungumza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mgogoni tunaunda mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninamshukuru Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kubakisha dakika 2 na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameniambia naweza kutumia dakika 5 zake, kwa sababu yeye yake ni mafupi tu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mchana huu wa leo kuendelea kuichangia bajeti hii muhimu sana ya serikali. Nitangulize kwa kusema kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na hadith ndogo ambapo katika dakika mbili za Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ndio nitakazozitumia, kujadili au ku-*analyze* michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe humu ndani na itawiana na hii hadith nitakayoitoa.

Kwa kweli hadith hii wapo baadhi wanaijua lakini kuikumbusha si vibaya, kulikuwa na mzee wetu mmoja alikuwa na shida, yaani alikuwa na tatizo la kutaka apatiwe miwani. Wakati nilipokuwa Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Haile Silasie walikuja madaktari wanaohusika na *Lions Club* na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alikuwa mwalimu pale mwaka 1979.

Sasa yule mzee wetu aliniambia anataka miwani, basi nilimwambia twende, na mimi ndio Mwalimu Mkuu pale nilitumia *influence* yangu nikaingia ndani kule na kuanza kupimwa miwani, alipewa *lens* zenye *zero point five* akasema mizuri, alipopewa *lens* zenye *one point zero* akasema mizuri zaidi, akapewa ya *lens* zenye *zero point seven five* akasema huu nahisi ndio unaonifaa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nilimwambia daktari huyu mpe miwani ya *frame* tu na wala usimtilie vioo, basi alipopewa ule akasema huu naondoka nao ndio ninaoutaka. (*Kicheko*/*Makofi*)

Hii maana yake nini, kwa kweli kila lens aliyopewa au aliyokuwa akiekewa anaiona ni nzuri zaidi kuliko nyengine na michango iliyotolewa hapa wa mwanzo mpaka wa mwisho unamshindwa mwenzake kwa uzuri. Kwa hivyo, nashukuru sana na mimi nataka niondoke anayo yote. (*Kicheko*/*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na wala sioni ajabu kama nilivyosema kwamba mimi namfahamu zamani tokea mwaka 1979 wakati tulipokuwa tukisomesha pamoja.

Vile vile tumekutana katika shughuli zetu mbali mbali wakati alipokuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mipango, Bungeni kipindi kilichopita mimi, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Fatma Abdalla Tamim tulikuwa Bungeni pamoja na maeneo mengine. Kwa kweli uwezo wake kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwenye Bunge ulionekana wazi wazi, yaani akizungumza anazungumza *with authority*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jinsi alivyoweza kuziunda wizara hizi na kuwatafuta watu ambao ni muafaka kabisa katika wizara zetu. Kwa hivyo, kazi iliyopo mbele yetu sisi ambapo Mhe. Rais ametupa au amejenga imani juu yetu, basi ni kushirikiana kwa pamoja na kuweza kutekeleza. *(Makofi)*

Kwa kweli bajeti hii ambayo imewasilishwa hapa ni ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, isipokuwa ni bajeti yetu sote na kuna haja ya kuisimamia kwa makini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa wale ambao waliochangia, nadhani kuna baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza na wamechangia *concerns* zao. Lakini kama watasoma hivi vitabu, yaani cha kwanza na cha pili viko *very details* Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli hata mimi nilikuwa na mashaka masuala ya uwezeshaji wa wananchi mbona kwenye bajeti ni *paragraphs* mbili tu, lakini nilipotizama humu ndani kumbe mambo mazuri. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Vile vile niwapongeze sana watendaji wa Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa jumla. Kwa kweli wamefanyakazi kubwa na wala sishangai Mhe. Naibu Spika, kwani uwezo wanao na sababu za kufanya hivyo wanazo na zaidi ni ule uzalendo wao wa kuipenda nchi yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie maeneo mawili kwa haraka. Kwanza nitazungumzia masuala yaliyopewa kipaumbele kama vile suala la kilimo, elimu, afya na maji. Kwa kweli suala la maji ni muhimu sana na maji ndio kila kitu, kwa sababu tunasema maji ni uhai na uchumi upo hapo, maisha na mambo mengine.

Lakini kuna haja kuhusu suala la maji liangaliwe kwa makini sana na tunashukuru kuwa serikali yetu imelipa kipaumbele suala hili la maji na wizara inayohusika na maji inafanya juhudi kubwa, isipokuwa mahitaji ni makubwa.

Kwa hiyo, kuna haja ya kuyaangalia kwa makini kwa kushirikiana kwa pamoja na matatizo ya maji yapo hata Makunduchi pia tatizo la maji lipo, lakini *Alhamdulillah* sihaba yanapatikana japo kuwa ni kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la afya ni vyema tukaliendeleza na hata kwa *private* na ni hakika kabisa.

Suala la kilimo, nimepata nafasi mimi wakati nilipokuwa kwenye ziara ya Mhe Rais tumeona juhudi za wananchi Mhe. Naibu Spika, pia kwenye ziara zetu tulipokuwa tukitembelea Vyama vya Ushirika katika maeneo ya kilimo tumeona.

Kwa kweli kuna mambo ambayo utahisi wananchi wetu wako tayari, isipokuwa wanachokihitaji ni kuwawezesha wale wananchi, ili waweze kufanya shughuli zao kwa makini. Mhe. Naibu Spika, hilo ndilo jukumu ambalo nitakuja kulielezea mwisho wa maelezo yangu namna gani tutaweza kuwa-*empower* watu wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alizungumzia suala kuhusu vijana kwamba wamesahauliwa. Katika kitabu cha Mapitio ya Hali ya Uchumi tukiangalia basi kuna eneo ambalo limeelezwa kwa makini sana, suala zima la vijana hasa ukurasa wa 240 hadi 243 na umeanzishwa ule Mfuko kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ambao Norway wanatusaidia. Kwa hivyo, pale utaona vijana wamepewa fursa kubwa sana. *(Makofi)*

Lakini suala la uwezeshaji Mhe. Naibu Spika, halimuangalii kijana tu, yaani rika zote kuanzia mdogo hadi wenye umri mkubwa kabisa, kwa sababu wakulima wetu vijijini si vijana tu na wengine ni watu wazima. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kazi ilioko mbele yetu Mhe. Naibu Spika, na hili nataka nilieleze na lifahamike kwamba kazi yetu moja ni kutoa mafunzo kwa hawa wajarisiamali, wakulima na wananchi wetu kwa jumla. Kwa mfano, hivi sasa tumeanzisha vituo na tumeanza kuzindua hivi sasa Kamati Maalum ambazo zinapita katika kila Wilaya hivi sasa.

Kwanza kutoa elimu juu ya ajira, kwamba njia gani tufanye ili tuweze kupata ajira kwa wingi, njia moja ya kupata ajira ni kujikusanya katika vikundi mbali mbali vya ushirika na kuweza kuwa-*empower* watu wale. Kwa kweli

empowerment hata ukitoa elimu ni *empowerment* na sio *necessary* kwamba utoe fedha, yaani ile ni elimu peke yake, kwa sababu watu wapo na sio kama hawana ujuzi, isipokuwa wanachohitaji ni kuongozwa ili waweze kutoa *production* ya kuridhisha.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la elimu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alilizungumza. Kwa kweli mimi nilipata bahati ya kuhudhuria Mkutano wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Miongoni mwa mambo au nchi zote zilizowasilisha ripoti zao pale walizungumzia sana kuhusu suala la *Vocational Training* na hili linaweza kutusaidia sana Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Zanzibar *population* yake ni *1.2 million*.

Kwa maana hiyo, mimi nina hakika tukiweza kuimarisha suala hili basi tunaweza kufikia hatua nzuri, kwa bahati nzuri sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali baada ya vile vituo viwili tayari kuna mpango na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ninahakika atakuja kulieleza kwenye bajeti yake. Kwa kweli kuna ujenzi wa vituo vyengine vitatu vya *Vocational Training* katika mikoa mitatu iliyobakia.

Lakini na sisi kwa upande wetu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika tunakusudia kujenga *Skills Development Centers* katika kila wilaya, ili ziweze kutusaidia kwa ajili ya kuwa-*empower* watu wetu, kuwapatia mafunzo na wakati wanapoondoka pale basi waweze kujiajiri wao wenyewe na kuweza kuwaajiri na wengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hili ni muhimu na ninaomba sana tufanye kila litakalowezekana kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ili ahakikishe kwamba masuala haya ya *Vocational Training* yanasimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Kwa kweli hivi sasa hali ya nchi ni nzuri imetulia, Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa umetusaidia sana kutekeleza kazi zetu. Kwa hivyo, naomba nishukuru na kupongeza sana viongozi wetu waliosimamia *Government National Union (GNU)* na hatimaye tumefikia hatua hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala la msingi hapa ambalo tunataka kujipima sisi wenyewe kwanza ni kutathmini. Kwa hiyo, hivi sasa tunatoka wapi, tupo wapi na tunaelekea wapi na bajeti hii kwa bahati nzuri imetoa jawabu hiyo. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wamechukua kila sekta na kueleza hapa na kazi iliyobakia kwa mawaziri sisi wakati tutakapokuja kuwasilisha bajeti zetu kwenye *details* zaidi kuhusu masuala yetu.

Naomba nimalizie na suala la ajira. Mhe. Naibu Spika, ajira tafsiri yake nini, tafsiri yake ni mtu kupata riziki yake kihalali yoyote, iwe ndani ya serikali au nje ya serikali. Kwa kweli Sekta Binafsi ina mchango mkubwa sana katika suala la ajira na ninashukuru *Alhamdulillah* hivi sasa ajira zipo, kwamba sasa wizara yangu imeanza kupokea maombi kutoka nchi mbali mbali za nje, yaani wanataka vijana kutoka Zanzibar waende wakafanyakazi katika nchi zao.

Jambo la muhimu na hili lilizungumzwa katika Mkutano huo wa *ILO* ajira yenye staha sio kumchukua Mzanzibari au mfanyakazi kutoka Zanzibar na halafu akapata matatizo nje ya nchi. Kwa hivyo, kitu ambacho tunachokifanya tunakuwa na mikataba ambayo itawalinda vijana wetu watakaokwenda kule, ili wafanye kazi za staha. Kwa maana hiyo, kazi zipo hivi sasa na tunashukuru na tayari mashirika yanakuja.

Pamoja na hayo, nilipata bahati ya kuonana na Mhe. Waziri Anayehusika na Masuala ya Kazi wa Qatar. Waziri huyo anasema hakuna matatizo tena bila ya kujali hata kiwango cha elimu kwa sababu kazi wanazo na wale hivi sasa wanaandaa Kombe la Dunia mwaka 2022, yaani maeneo karibu yote wanahitaji wataalamu na sisi hapa kuna watu ambao wenye *Degree* za *Business Administration*, Sheria na wengineo. Kwa kweli wapo vijana wetu na tutatumia fursa hii Mhe. Naibu Spika na tumekubaliana tutakutana hivi karibuni, ili tuweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mwisho nimalizie dakika mbili zilizobakia Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizungumzia kuhusu suala la *exploration* mafuta, mimi nakubali na kwamba inawezekana tunaweza kulifanyia *exploration*.

Kwa mfano, hata wakati tulipoanzisha Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* Mhe. Naibu Spika yalikuja maneno hapa kidogo. Lakini tulihcokifanya tukasema hebu tumuombe Mwenyezi Mungu na tuanze kile Chuo Kikuu cha Taifa kile mwaka 2001, tulipata uthibitisho kutoka *High Accreditation Council* haikuwa rahisi na baadaye wenzetu walituelewa na hatimaye Chuo Kikuu leo kina *extend* na kinaendelea vizuri. Mhe. Naibu Spika, ninachokiomba kwenye *exploration* hakuna *harm on that* tunaweza kufanya, kwa sababu itatusaidia kujua hatma yake. *(Makofi)*

Baada ya hayo, Mhe. Naibu Spika na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi naomba sana kuiunga mkono bajeti hii na tunaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba bajeti yetu tumeshaipitisha na watekelezaji ni sote na tukaifanyie kazi kwa lengo la kuendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimkumbushe Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kunikopa dakika zangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa namna alivyowasilisha bajeti hii vizuri. Aidha niwashukuru na kuwapongeza sana watendaji wa Wizara hii ya Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutayarisha bajeti nzuri sana. *(Makofi)*

Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru sana Rais wetu kwa muongozo wake alioutoa na ndio maana tukafikia kiwango hiki cha bajeti hii. Aidha niwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa namna ambavyo nimewaona wameipokea bajeti hii vizuri na ninaamini watashirikiana na serikali yao katika kutekeleza vizuri sana bajeti hii. Kwa kweli hii ni bajeti yao ambayo imejielekeza kwao kwa nia ya kutatua matatizo yanayowakabili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imewagusa wananchi wote, kwa sababu imegusa sekta zote muhimu za wananchi zikiwemo kilimo, afya, elimu, maji, uwezeshaji wa wananchi, kuimarisha kipato cha wafanyakazi wa serikali, taasisi nyengine mbali mbali, pia kuimarisha miundombinu pamoja na kuishirikisha Sekta Binafsi katika kujenga nchi yetu.

Kwa hiyo, ni bajeti ya wananchi na mimi naunga mkono wale wenzangu waliozungumzia kwamba bajeti hii ni ya wananchi, kweli ni ya wananchi na imejielekeza kwa wananchi, tunaishukuru sana serikali yetu kwa uamuzi huo.

Mhe. Naibu Spika, yako mambo yaligusa wizara yangu na ninapenda niyatolee ufafanuzi wa haraka. Moja lilikuwa linahusu Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, kazi ya rasimu ya sheria hii iko katika hatua nzuri na ninataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba *Inshallah* kikao kinachokuja cha Baraza lako tukufu, basi tutaileta hapa sheria ili iwe sasa inatekelezwa, kwa ajili ya kutoa nafasi zaidi kwa Baraza hili tukufu kuweza kufanya shughuli zake kwa umahiri zaidi.

Vile vile Sheria ya Mfuko wa *Constituency Development Fund (CDF)* nayo iko katika hatua nzuri na ninawahakikishia katika kikao kijacho tutaileta hapa Barazani kwa ajili ya uamuzi wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la Mfuko wa Maafa hivi sasa tunashughulikiia sera nayo imeshafikia hatua nzuri pia. Kwa hivyo, sina shaka yoyote kwamba

mara tutakapoipitisha na kutoa baraka za Baraza lako tukufu kwa sera hii, basi hatua zitachukuliwa kuhakikisha kuwa Mfuko wa Maafa unaanzishwa ambao licha ya kusaidiwa na Serikali Kuu. Kwa kweli, tutaweka nafasi nzuri, ili Taasisi za Kimataifa, watu binafsi na wale wote ambao watakuwa tayari, kwa ajili ya kushirikiana na serikali katika kuimarisha Mfuko huu basi wapate fursa hiyo.

Kwa maana hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wafute subiri huku tukitayarisha Mfuko ambao utakidhi haja kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Kuhusu suala la *TASAF* ni kweli limezungumziwa hapa na Waheshiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakaonesha wasi wasi wao kwamba bado haujatoa sura nzuri katika upunguzaji wa umasikini. Mhe. Naibu Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kuwa mfuko huu nia yake ni kusaidia kupunguza makali ya umasikini kwa wananchi wetu na ulijielekeza vizuri katika maeneo ya sekta muhimu ambazo zinasaidia kupunguza umasikini huo.

Kwa mfano, Sekta ya Elimu tumesaidia kujenga madarasa karibu 51, kujenga Nyumba za Walimu, Vituo vya Afya, Nyumba za Madaktari, kutia kufusi barabara zile ambazo zinazokwenda katika kilimo, kusaidia miradi ya umwagiliaji maji, kuhifadhi mazingira. Pamoja na hayo, kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuweza kujisaidia kuimarisha miradi yao ya kiuchumi, pia kwenye eneo la uvuvi na ufugaji, yaani mfuko huu umesaidia sana. Kwa hivyo, si rahisi kuwaona moja kwa moja, isipokuwa tumejielekeza kwenye maeneo ambayo yatasaidia kupunguza ugumu wa maisha ya watu wetu na msaada wake ni kama hivyo.

TASAF III inajielekeza zaidi kwa wananchi moja kwa moja katika kuondoa umasikini wa kipato. Kwa hiyo, nitazidi kuchangia katika kuimarisha jitihada za serikali za kuimarisha hali ya wananchi wetu na kupunguza umasikini.

Mhe. Naibu Spika, maeneo mengine ambayo pia yamegusa kwa kiasi fulani wizara yangu ni Bandari ya Mpigaduri. Kwa kweli nataka niseme kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika ziara yake kula Abudhabi alikutana na viongozi na walilizungumza jambo hili vizuri na wamefikia muafaka mzuri kwa nia ya kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ajili ya kuanzishwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, kwa kiasi fulani itakuwa ni suluhisho kubwa sana kwa nchi yetu. Kwa hivyo, nataka nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Vile vile ninapenda nizungumzie kuhusu suala la ushiriki wa Zanzibar katika Jumuia ya Afrika Mashariki. Mhe. Naibu Spika, kwa mazingira yetu ya sasa Zanzibar inaposhiriki kwenye Jumuia ya Afrika ya Mashariki inapata haki zake

kwa ukamilifu. Kwa kweli kwa kiasi kikubwa Waheshimiwa Wajumbe ni gharama kubwa sana kushiriki peke yetu, maana yake kila mwanachama anatakiwa kulipa zaidi ya bilioni kumi kwa mwaka kuwa manachama wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki.

Lakini chini ya kivuli cha Jamhuri ya Muungano, ambapo na sisi ni miongoni mwa nchi mbili zilizoungana, kwa hiyo ule muungano ni haki yetu na ownership yetu ipo pale ndani. Kwa maana hiyo, hakuna kosa hata kidogo kushiriki kwa kivuli kile kwa maana ya kupunguza gharama, kwa sababu tunaweza kuwakilishwa vizuri.

Hata hivyo, upo muongozo unaotayarishwa kwa ajili ya mambo haya ya kimataifa kwa upande wa SMZ kuweza nayo kushiriki moja kwa moja kwenye masuala ya kimataifa. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kama ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupima namna gani tunavyoona, ikiwa utaratibu wa sasa unakidhi haja basi twende nao kwenye Jumuia ya Afrika ya Mashariki tunayo haki hiyo laa! Tukiona tunaweza kuamua vyengine kwa sababu muongozo mpya unakuja karibuni basi uamuzi ni wetu.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna suala hapa ambalo lilizungumzwa kwamba baadhi ya watendaji wa serikali kutokutii Kamati za Baraza. Kwa kweli nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba mtendaji yeyote wa serikali anatakiwa kabisa kutimiza wajibu wakati anapoitwa na Kamati hizi za Baraza.

Utaratibu mzuri tuliojiwekea ni kwamba Kamati hizi kupitia Katibu wa Kamati ni kuwaandikia Katibu Mkuu wa Wizara husika, ili mtendaji yeyote wa serikali ambaye anatakiwa na Kamati hizi za Kudumu, basi aweze kufika na kutoa taarifa zinazohitajika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tutachukua hatua za kinidham kwa mtendaji yeyote ambaye hatofuata utaratibu huo wakati anapoitwa na Kamati hizi za Kudumu za Baraza. Vile vile nataka nizungumzie kuhusu suala la moja ambalo lilizungumzwa sana ni kuhusu utafiti wa uchimbaji wa mafuta na hapa nataka kuungana mkono na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba kazi hii ya utafiti ianze, ili tuweze kujua hasara na faida. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika pamoja Waheshimiwa Wajumbe, naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii.

Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ahsante sana kwa michango mizuri na hivi sasa tumefikia tamati kwa michangio. Kwa hivyo, tunaona jioni tuje mapema kwa ajili ya kumsikiliza Mhe. Waziri na baadaye tupitishe Bajeti yetu Kuu ya Serikali.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa
mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ninayo taarifa kwamba Naibu Spika, alimaliza mjadala na nawashukuru kwamba mambo yamekwenda vizuri pamoja na kwamba baadae muda tuliubana bana kidogo, lakini nafikiri Mhe. Waziri amesaidiwa vya kutosha na kwa maana hiyo sasa kama tulivyopanga kabla ni wakati wa kumuomba mwenzetu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha Uchumi na mipango ya Maendeleo, ili sasa tufanye majumuisho na hatimae tufanye kazi tunayokusudia.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kwanza nataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote wazima na kuwepo hapa, baraka za Mwenyezi Mungu zimekuwezesha wewe Mhe. Spika, pamoja na Naibu Spika, kuweza kuendesha mijadala yetu hii kwa salama na amani namshukuru sana.

Pili nataka nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Moh'd Shein kwa kuniteua nimsaidie katika masuala ya fedha uchumi na mipango ya maendeleo, nataka nimuahidi Mhe. Rais niwaahidi Waheshimiwa Wajumbe na Wananchi wa Zanzibar kwa ujumla kwamba sitowaangusha. Nitajituma kadiri ya uwezo wangu na pale ambapo mtaona nimekosea basi niko tayari kuelekezwa kwa faida ya wananchi wetu na nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile nataka niwashukuru sana Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais wakati wa maandilizi ya bajeti nilikuwa nikipata ushauri na mwelekezo kutoka kwao nawashukuru sana, nawaomba sana waendelee kunisaidia kwa faida ya nchi yetu na wananchi wetu.

Mhe. Spika, nataka vile vile niwashukuru Waheshimiwa wote kwa pongezi walizonipa, lakini nataka niwaambie mimi ni tumbo tu viungo ni watendaji wangu, pongezi mulizonipa nataka nizipeleke kwa watandaji wangu wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wangu Ndugu Khamis Mussa, kwa kweli

wamefanya kazi nzuri tumeshirikiana tokea Rais aliponiteua hadi hii leo, nawaomba watendaji wangu waendelee kunisaidia ili tuweze kuivusha nchi yetu katika neema na faraja inshaalla.

Mhe. Spika, kila kwenye mafanikio ya wanaume na mwanamke yupo ubavuni, nataka nimshukuru sana sana mke wangu pamoja na watoto wangu wote, kwa kweli wamenipa nafasi ya kuweza kutekeleza majukumu yangu nashukuru sana. Nawaomba waendelee kunipa nafasi hiyo kwa sababu wao vile vile ni Wazanzibari na mimi naitumikia Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo nataka nithubutu kusema kwamba michango ya Waheshimiwa Wawakilishi nimeipokea kwa roho ya ukunjufu sana, michango yenu ilikuwa na dira kwa kutekeleza majukumu yetu. Tunaweza leo tusiwe na jibu la moja kwa moja lakini yametusaidia sana kuweza kutekeleza majukumu yetu kwa siku zijazo, nakuombeni sana muendelee kushirikiana na mimi na muendelee kushirikiana na Afisi yangu.

Mhe. Spika, nathubutu kusema tumepata faraja kubwa sana waheshimiwa (53) Waheshimiwa (4) wamechangia kwa maandishi Waheshimiwa (49) wamechangia kwa kusema. Kati waliochangia kwa kusema Waheshimiwa (38) walikuwa ni kutoka maeneo mbali mbali na waheshimiwa (11) walikuwa ni Manaibu Mawaziri na Mawaziri ambao nawashukuru sana, wamenisaidia kutoa ufafanuzi baadhi ya hoja.

Mhe. Spika, kazi iliyobakia mbele yangu sasa hivi ni ndogo kwa sababu sekta nyingi zimetolewa ufafanuzi na waheshimiwa Mawaziri, nitawaomba waheshimiwa niwataje wale ambao wamechangia bajeti hii kwa heshima na taadhima.

1. Mhe**.** Hamza Hassan Juma
2. Mhe**.** Shawana Buheti Hassan
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Asaa Othman Hamad
5. Mhe. Rashid Seif Suleiman
6. Mhe. Abdi Mossi Kombo
7. Mhe. Ali Abdalla Ali
8. Mhe. Omar Ali Shehe
9. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
10. Mhe. Mussa Ali Hassan
11. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
12. Mhe. Asha Bakari Makame
13. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
14. Mhe. Abdalla Juma Abdalla

15. Mhe. Hassan Hamad Omar
16. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
17. Mhe. Raya Suleiman Hamad
18. Mhe. Saleh Nassor Juma
19. Mhe. Salmin Awadh Salmin
20. Mhe. Asha Abdu Haji
21. Mhe. Fatma Mbarouk Said
22. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
23. Mhe. Panya Ali Abdalla
24. Mhe. Hija Hassan Hija
25. Mhe. Mohammed Haji Khalid
26. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
27. Mhe. Mgeni Hassan Juma
28. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
29. Mhe. Ali Salim Haji
30. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
31. Mhe. Subeit Khamis Faki
32. Mhe. Abdulla Mohammed Ali
33. Mhe. Farida Amour Mohammed
34. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
35. Mhe. Nassor Salim Ali
36. Mhe. Ashura Sharif Ali
37. Mhe. Moh'd Said Moh'd
38. Mhe. Viwe Khamis Abdalla

Waheshimiwa Mawaziri na Naibu waziri waliochangia**.**

39. Mhe. Sira Ubwa Mamboya
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
41. Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej
42. Mhe. Machano Othman Said
43. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
44. Mhe. Ali Juma Shamhuna
45. Mhe. Said Ali Mbarouk
46. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini
47. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
48. Mhe. Haroun Ali Suleiman
49. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed

WALIOCHANGIA KWA MAANDISHI

50. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman
51. Mhe. Salim Abdulla Hamad
52. Mhe. Salma Mohammed Ali
53. Mhe Salma Mussa Bilali

Mhe. Spika, hoja za waheshimiwa ni wengi na mimi nataka nithubutu kusema kwa kiwango kikubwa waheshimiwa Mawaziri wamenishaidia kutoa ufafanuzi katika maeneo yao, nitajikita katika maeneo yaliyosalia ambayo hayajapata majibu kutoka kwa Weheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Spika, kwanza nataka nianze na hoja ambayo ningependa nichukue muda kidogo kwa faida ya wananchi wetu, hoja ya ukuwaji wa uchumi na hali halisi ya pato la kila mwananchi. Katika hotuba yangu ya bajeti nimeeleza kwamba ukuwaji wa uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa asilimia 6.5 nimeeleza vile vile wastani wa pato la kila mwananchi ni 7,083,000/= zimeibuka hoja kwamba wapo watu ambao hawapati hela hizo imekuwaje.

Kwa maana nyengine tafsiri ya ukuwaji wa uchumi na pato la mtu mmoja mmoja haionekani kwa kila mmoja wetu, nataka niseme kwamba kwanza lazima tuangalie muundo wa ukuwaji wetu wa uchumi, ukuwaji wetu wa uchumi umechangiwa zaidi na sekta mbili. Sekta ya huduma ambayo imechangiwa zaidi ya asilimia 42 na sekta ya kilimo ambayo imechangiwa asilimi 32.8. Mhe. Spika, nataka nianze hapo ili kila mmoja wetu aweze kutufahamu takwimu zetu zinasema kwamba asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea kilimo ambao mchango wake ni asilimi 32.8 katika pato la taifa.

Nitatoa tafsiri ya hisabu ili kila mmoja wetu aweze kuiona asilimia 70 ya watu wetu ni watu 8,050,000 wanategemea kilimo ambacho kinachangia asilimia 32.8 tu katika pato letu la taifa, hii ina maana gani ina maana watu hawa ukiwagaiya mchango wao katika pato la taifa hawatapata shilingi 7,083,000 kwa mwaka watapata shilingi 3,065,000 kwa maana nyengine kwamba watu hawa wanaotegemea kilimo kwa siku watakuwa wanaishi kwa shilingi elfu moja. Hii ina maana kwamba nchi yoyote duniani inayotegemea kilimo watu wake ni masikini, nitatoa takwimu ili tuweze kuthibitisha haya tunayozungumza halafu nitaeleza nini tufanye katika hili.

Mhe. Spika, nikianza na kisiwa kidogo cha Seychelles ambayo ina watu 89,188 mchango wa kilimo katika pato la taifa la Seychells ni asilimia 3. Lakini mchango wao wa viwanda ni asilimi 23, wastani wa pato la taifa kwa kila mtu kwa Seychells ni dola 23,000, mchango wao wa kilimo ni asilimi 3.

Tukiondoka Seychells nchi ndogo iliyoko katika bara la Afrika hebu tumuangalie Mmarekani, mchango wa kilimo katika pato la taifa la Marekani ni asilimia 1.2 lakini mchango wa viwanda ni asilimia 22.2, pato la taifa kwa kila Mmarekani ni dola 47,000 hebu tuondoke tumtizame Mchina.

Mhe. Spika, mchango wa kilimo kwa nchi ya China kwa pato lake la taifa ni asilimia 9.6 na mchango wa viwanda ni asilimia 46, pato la taifa wastani wa kila mtu kwa wachina ni dola 7,600. Nitoe mfano mwengine wa Mwisho Mhe. Spika.

Sasa tuiangalie Moritious ni kisiwa kidogo kiko katika Afrika mchango wake wa kilimo katika pato la taifa ni asilimia 4.8 mchango wa viwanda ni asilimia 24, wastani wa pato la kila mtu Moritious ni dola 14,000.

Mhe. Spika, hii ina maana gani ina maana wenzetu hawa ili waweze kupiga hatua wameona kuna haja kubwa sana ya kuwekeza katika viwanda, lakini kwa kiwango kikubwa hawakusema kwamba kilimo wanakipa mgongo, kilimo wanacho kwa sababu ile ile ya kuwa na *food security* uhakika wa chakula na katika Baraza hili tumepitisha uhakika wa Baraza la Chakula.

Mhe. Spika, hizo ni nchi za wenzetu lakini nataka tuangalie kwetu asilimia 48 ya Wazazibari ni watoto walio chini ya miaka kumi na sita ambao hawa hawana tija katika ukuwaji wa uchumi, hawana mchango na asilimia 6.5 ni Wazee zaidi ya miaka sitini kitakwimu hawa wanatakiwa wapumzike na sisi tuliosalia ndio tunatakiwa tuchangie katika ukuwaji wa pato la taifa. Hii ina maana gani ina maana kwamba ukuwaji wetu ni mkubwa asilimia 3.1 ndio maana ukiangalia kuna kitu kinachoitwa *population pyramid* utaona kwamba *base* yetu ni kubwa sana watoto ni wengi, ndio maana mpaka hii leo takwimu zetu zinatwambia kwamba pato letu la taifa ni dola 561.

Mhe. Spika, nini tufanye tuna mambo kadhaa ya kuweza kufanya na yako ndani ya uwezo wetu, la kwanza serikali ya awamu ya saba ikiongozwa na Dk. Ali Moh'd Shein tuhamasishe uwekezaji katika viwanda, hapa hatuna ujanja ni dhahiri kwamba tukihamasisha katika viwanda *population* ambayo inategermea kilimo itakuwa nyengine inakwenda kutegemea viwanda, tutakiwacha kilimo na idadi nzuri ya wale ambao wanaweza kukitegemea. Lakini vile vile maamuzi yetu tuliyoyafanya Mhe. Spika, kupitia bajeti hii ya kuimarisha sekta ya kilimo nayo vile vile yatatusaidia sana, leo kilimo kimekuwa ni kimbilio cha watu wengi kwa sababu *in put* yake yaani thamani yake ni ndogo, kwa maana kwamba mtu yoyote leo akishakuwa na shilingi kumi na tano akishanunua jembe basi anakimbilia kilimo tunasema ili kupunguza watu kule wengine waende huku.

Kwanza tununue matrekta ya kutosha, tununue *power tiller* za kutosha utafiti huu wa mbegu mbali mbali uendelee tumezungumzia mirika sasa hivi inaweza kuota popote pale, nashukuru wakulima wanaitafuta wapi wataipata mirika nataka niwaambie wastahamili kidogo Mhe. Mansour atakapokuja atatangaza wapi inapatikana mbegu.

Lakini jengine ambalo tunaweza kulifanyia kazi ni kutizama sekta ya kilimo kwa upana wake siku zote tunaitizama sekta ya kilimo kwa maana ya kilimo cha *production*, hatuangalii uvuvi wala mifugo tuna nafasi kubwa sana ya kuweza kukua kwa mifugo na uvuvi, kinachohitajika ni kuwa majasiri katika kuwawezesha wafugaji wetu na wavuvi wetu. Na mimi naamini dhana ya Mhe. Rais ya kuunda Wizara ya Uvuvi na mifugo ilikuwa ni kutuelekeza huko, nataka kuthubutu kusema Mhe. Spika, waziri aliyemteua ni mahiri na naamini atatuvusha.

Mhe. Spika, uwezo wa kukua kiuchumi Wazanzibari tunao na nia tunayo hatuna sababu ya kuogopa, la msingi nataka niwaombe ndugu zangu wazanzibari ni kujituma bila ya woga na Mungu akitujaalia katika kipindi kifupi uchumi wa Zanzibar hautokuwa ndoto. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kiuchumi sasa nataka niendeleze hoja zangu katika masuala ambayo yameulizwa na waheshimiwa wawakiilishi.

Kwanza nianze na suala zito liloulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma mwenyekiti wa wanyeviti, suala la kuimarisha utawala bora katika hotuba yake Mhe. Hamza Hassan Juma ameeleza mambo mengi nataka nimshukuru sana hotuba ile itakuwa dira katika kutekeleza shughuli zetu ndani ya serikali ya awamu ya saba, lakini naomba kidogo nitoe ufafanusi katika baadhi ya maeneo.

Kwanza amesema suala zima la ukubwa wa serikali nataka niseme amenipa changamoto kubwa Mhe. Hamza Hassan Juma ya kwenda kusoma, kutazama maana ya serikali kwenye *dictionary* nimelazimika kulitafuta *dictionary* na kusoma nini maana ya serikali. Katika *dictionary* ambalo nimelisoma mimi bahati nzuri hakuna idadi ya Mawaziri waliotajwa katika serikali, wanasema ni chombo cha kutunga sera na kuongoza wananchi haijataja idadi wangapi wawemo kwenye chombo hicho. Kwa maana hiyo ile imenipa faraja kwamba yoyote yule anayekuwa rais wa nchi yoyote anaunda serikali yake kulingana na matakwa yake, kulingana na muono wake.

Mhe. Spika, nitatoa mfano ili sote tupate kuona *Seychells* ina watu 89,000 ina mawaziri tisa ingekuwa Zanzibar tunagawa kila watu 89,000 tunaweka mawaziri tisa tungekuwa na mawaziri wangapi, lakini kama hiyo haitoshi nitatoa takwimu nyengine vile vile. India ina watu bilioni 1,189,773,906. Yaani bilioni 1.1 ina mawaziri 77 hebu tumtizameni na Mchina basi 1.3 bilioni ana mawaziri 22 inategemea na muono wa Rais aliyekuweko madarakani anataka kufanya nini.

Mhe. Spika, nitatoa kidogo kwa muhtasari Dk. Ali Moh'd Shein ukilinganisha na awamu ya sita na awamu ya saba amezidisha Wizara tatu kubwa mpya, dhamira yake ni nzuri naomba niwasaidie ndugu zangu na wananchi

wanifahamu, ameunda Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, siku zote tulikuwa tunalilia maslahi ya watumishi wa umma ni mabovu kwa sababu idara haiwezi kuona zaidi ya Wizara, ile Idara ya Utumishi tumeitia ndani ya Ikulu pale ilikuwa haiwezi kuona. Leo Waziri ameona ameangalia maslahi ya watumishi wetu hakuangalia kupandisha mishahara. *horizontal* ameangalia mpaka *vaticol*, Waziri ametwambia hapa katika majibu yake aliyoulizwa juzi mishahara itatofautiana, kwa mujibu wa miaka yetu mliyoanza kufanya kazi halikuwepo hilo, kwa hivyo watumishi wa umma hii Wizara ameiunda makusudi ili tuangalie sisi watumishi wa umma. Leo tunamtetezi.

Lakini vile vile Mhe. Rais alivyokuwa anafanya kampeni alipita huko katika maeneo yetu, akaona umasikini ulikithiri ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar. Ameunda Wizara ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Wizara hii haitakuja ikaniwezesha mimi Omar Yussuf Mzee,itamuwezesha mwananchi wa Micheweni, mwananchi wa Chakechake, wananchi wa Wilaya ya Magharibi, wanawake kwa wanaume, wale ambao hali zao ni duni. Bila ya wizara hii hatutoondokana na umasikini.

Mhe. Rais akasema jamani kuna sekta hizi mbili zina *potential* kubwa sana Zanzibar nayo ni sekta ya uvuvi. Ndugu yangu Jussa jana alipokuwa anazungumzia mafuta anasema kwamba uchumi nimeukalia. Nataka nimwambie na Mhe. Said Ali Mbarouk naye vile vile kaukalia. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna potential kubwa sana katika sekta ya uvuvi lakini ilikuwa imeunganishwa na Wizara ya Kilimo kwa ujumla wake. Tulikuwa tunaangalia *production* kwa maana ya mazao ya mpunga, muhogo, mahindi basi. Leo ninamuona Mhe. Saidi Ali Mbarouk alivyokuwa anachacharika kila wakati anakuja ofisini anataka kuwawezesha wavuvi.

Nataka niseme ndugu zangu, Waheshimiwa wenzangu nia ilikuwa ni nzuri ya Mhe. Rais kuunda wizara 16. Pale atakapokuwa anaona kwamba sasa nimefikia malengo haimkatazi Mhe. Rais kuvunja Wizara akaziunganisha. Na mimi nitamuomba sana Mhe. Rais wa Zanzibar, akifikia malengo basi aunganishe. Na kama hajafikia malengo hata kama akiona hii wizara niliyonayo mimi Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo bado anataka kuivunja, aivunje. Akitaka kufanya tatu afanye tatu. Mimi naamini kwamba atafanya kwa maslahi ya taifa hili na sio kwa maslahi yake binafsi.

Mhe. Spika, hoja nyengine ya Mhe. Hamza ilikuwa ni kuunda mfuko maalum kwa ajili ya Baraza la Wawakilishi na Mahakama. Sina tatizo na hili. Nataka nimwambie Mhe. Hamza mdogo wangu Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Wenyeviti. Sina ogomvi na hili. Tutaliangalia ili tuweze kuona ni kwa kiwango gani tunaweza tukauunda mfuko wa Mahakama na mfuko wa Baraza la

Wawakilishi. Katika hili nataka niseme Mhe. Spika, suala la matumizi, *discipline* ya matumizi itahitajika sana. Kwa sababu sasa hivi kila mmoja tukimaliza hili atakuwa na mfuko wake. Utakapokuwa umemaliza huna pa kukimbilia. Kwa hivyo tulioneni kabisa hili. Lakini mchakato nadhani tunakwenda nao, ili tuweze kuona ni kiasi gani tutakuwa na hii mifuko ili iweze kusaidia katika kutekeleza shughuli zetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo Mhe. Hamza ameligusia ni suala la ushirikiano baina ya sisi watendaji Serikalini na vyombo vya habari. Alikwenda mbali kidogo Mhe. Hamza akasema kwamba kwa faida ya kuwaelimisha wananchi wetu. Nakubaliana na yeye bila ya sisi watendaji kushirikiana na vyombo vya habari wananchi wetu watakosa elimu. Watashindwa kujua serikali inafanya nini, watashindwa kujua matatizo ya serikali ni nini. Watashindwa kujua wapi serikali tumekosea. Nawaomba sana Makatibu wakuu wawakaribishe waandishi wa habari pale wanapotaka kuelewa yale tunayofanya katika maofisi yetu.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza alitaka vile vile tuandae sheria kwa ajili ya viongozi kutangaza mali zao. Nakubaliana na wewe. Mhe. Dokta Mwingi Haji amelieleza hili asubuhi, tumo humu ndani kwa uzoefu wa kutangaza mali, Makamo wa Pili wa Rais, ameanza kutangaza mali zake kupitia Bungeni. Mimi mwenyewe nimetangaza mali zangu kupitia Bungeni, Mhe. Abubakar katangaza kupitia Bungeni, Mhe. Moh'd Aboud katangaza kupitia Bungeni, Mhe. Fatma Fereji, Mhe. Haroun, hao wote wametangaza kupitia Bungeni mali zao. (*Makofi*)

Nataka nikwambieni ndugu zanguni kule Bara huwa wanafanya *sample*, wewe unatangaza mali zako, lakini siku utakapoingia katika ile *sample*. Wanakuletea Barua sasa wanataka kuona mali zako na *account* zako. Mimi nililetewa na Mhe. Haroun aliletewa. Nikawaruhusu waende wakatizame nyumba nilizonazo, nikawaruhusu waende wakatizame *account* zangu nilizonazo.

Kitu kimoja nataka nikujengeeni *confidence* ndugu Wawakilishi kama mali yako umeichuma kihalali huna woga, huna wasi wasi. Viongozi hatujakatazwa kufanya biashara. Kama biashara tunazozifanya ni za halali na kila mmoja anazijua mali ile umeichuma kihalali usiwe na wasi wasi. Namuomba sana Mhe. Waziri Dokta Mwinyi Haji lete sheria haraka sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo waheshimiwa wengi wameigusia huduma za afya ziimarishwe. Mhe. Shawana Bukheti, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe. Ashura Sharif na wengine wameigusia hoja hii. Nataka nisema Mhe. Spika, kwa nini serikali ya awamu ya saba ikasema afya ni kipaumbele cha kwanza. Bila ya afya hakuna shughuli hapa.

Awamu ya sita imefanya kazi nzuri. Nathubutu kusema ya kuangamiza maradhi ya malaria,lakini tuna changamoto zimejitokeza katika sekta ya afya na ndio maana tukasema kwamba sekta hii tutaipa kipaumbele cha kwanza. Tuna uhaba wa vifaa, tutanunua vifaa. Tunauhaba wa dawa muhimu, tumeweka kwenye bajeti yetu, tutatumia fedha zetu na fedha za misaada kwa ajili ya dawa.

Uchache wa watumishi, tutasomesha ndani na nje, watumishi katika sekta ya afya. Yamezungumzwa vile vile maslahi madogo ya watumishi wetu katika sekta ya afya. Nathubutu kusema watumishi katika sekta ya afya wakae mkao wa kula. Kama kuanzia basi tutaanza na wao, ili watumishi wa sekta ya afya wabakie na waweze kuwatumikia Wazanzibari wenzao.

Vile vile jambo moja ambalo lililozungumzwa katika sekta hii ya afya ni utendaji wa wafanyakazi wetu wa afya. Nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, wazungu wanasema "*seeing is believing"* Kuona ni kuamini. Makamo amekwenda usiku ameamini yale wananchi wetu wanayopigia kelele. Nitawaomba sana ndugu zangu wanaofanya kazi katika sekta ya afya, wawatumikie wananchi wetu. Wawatumikie wagonjwa, wazima hawendi pale, wanaokwenda pale wagonjwa.

Utendaji katika sekta ya afya Mhe. Spika, unafanana katika sekta nyengine. Nataka nimwambie Mhe. Makamo wa Rais changamoto tunazo mawaziri sote. Hii hali ni lazima tuibadilishe. Sasa hivi Wazanzibari kuwambiwa ni wavivu tuondokane na jina hilo. Lazima sasa tufanyeni kazi, tujitumeni wazanzibari kwa faida ya Wazanzibari wenzetu na kwa faida ya nchi yetu. Mhe. Spika, ninaamini mwanzo mzuri aliouanza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mawaziri watafuatia.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa wengi ni suala zima la upatikanaji wa maji safi na salama na hasa katika miji. Mji wa Zanzibar, Mji wa Chake-Chake, Mji wa Wete, Mji wa Micheweni na Mji wa Mkoani, hoja hii imeletwa na Wawakilishi wengi, akiwemo Mhe. Shawana, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Mwanaidi, Mhe. Hamza na wengine.

Tatizo la maji sio dogo, zinahitajika dola milioni 123 kuweza kuliondosha kabisa kabisa tatizo la maji. Serikali ya awamu ya saba imeamua kutafuta karibu nusu ya fedha hizo zinaingia kwenye bajeti hii. Tuna miradi mikubwa sana chini ya Jemedari Mhe. Ali Juma Shamuhuna itaanza hivi karibuni. Tuna miradi ya maji, vijijini Pemba, tuna miradi ya maji vijijini Unguja, na tuna miradi ya maji mijini Pemba, halafu tuna mradi wa maji wa mji wa Zanzibar. Imani yangu hakutakuwa na haja ya kuwapa wanajeshi kufanya kazi hiyo.

Wataalamu wa Kizanzibari wapo watafanya kazi hiyo. Naamini Mhe. Ali Juma Shamuhuna atafatilia kwa karibu zaidi.

Mhe. Spika, haya tunayoyazungumza nikilimaliza hapa dhamana yote nawaachia Mawaziri. Baraza hili tusiwe tunawalaumu watendaji, watendaji hawaingii humu, tuwalaumu mawaziri. Ukimpata waziri aliyekuwa hapendi kufatilia majukumu yake na watendaji wake watalala. Niwaombe sana waheshimiwa mawaziri tusimamie majukumu yetu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, suala jengine ambalo liloulizwa na wajumbe wengi ni uimarishaji wa kilimo. Hili limechangiwa sana.Limechangiwa *any positive way*, wametupongeza waheshimiwa na wengine wametupa maeneo ambayo ya kuyafanyia kazi. Wengine wametuonesha kuwa kuna mabonde ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Mhe. Mansour Waziri wa Kilimo amesikia ni msikivu na atayafanyia kazi mabonde yote hayo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nini tunatarajia kufanya katika sekta hii ya kilimo. Kwanza ni utafiti wa mbegu bora. Zanzibar ni kisiwa Mhe. Spika, hatuna eneo kubwa la kulimia lazima tuwe tuna mbegu ambayo mazao yake ni mengi. Wizara yetu ya Kilimo kupitia kitengo chetu cha utafiti kimeamua kufanya kazi hiyo na tayari kuna mbegu nzuri zimeshaanza kutolewa, mbegu ya mpunga ya Amerika.

Mhe. Dokta Mwinyi Haji leo amenisomesha Mkarafuu jinsi unavyoutunza mpaka ukaweza kumea vizuri, Mhe. Naibu Spika, na yeye amepata taaluma, naamini mikarafuu yako sasa itakuwa haifi. Na mimi niliwahi kupandisha mikarafuu kule shambani kwangu 20, sikupata hata mmoja, kumbe hii noleji aliyotupa Mhe. Waziri ni nzuri. Nitaomba sana Mawaziri kama tuna noleji kama hizo basi tuwasaidie wakulima wetu. Kwa hivyo suala la mbegu bora tumelipa kipaumbele.

Mhe. Spika, suala la mbolea serikali itatoa ruzuku kwa mbolea. Suala la umwagiliaji tumelipa kipaumbele na suala la elimu kwa wakulima. Haya yote Mhe. Spika, yatakuja kuelezewa zaidi na Mhe. Waziri wa sekta husika atakapokuja kuwasilisha bajeti yake.

Mhe. Spika, tunasema kilimo cha mboga mboga tuko nyuma sana Zanzibar. Mboga mboga tunahitajia maji tu. Asilimia 70 ya mahoteli yetu yaliyokuwepo Zanzibar yananunua mboga mboga kutoka nje ya Zanzibar. Tuwashajihisheni wananchi wetu kulima kilimo cha mboga mboga na vile vile viungo.

Leo Mhe. Spika, katika soko hiliki kilo moja ni 95,000. Mimi si mkulima sana lakini ninaamini mihiliki mitano inajaza kilo ikizaa vizuri. Tuwahamasisheni

sana wakulima wetu waweze kulima viungo ili waweze kupata eneo dogo lakini lina tija zaidi.

Zao jengine ambalo limezungumziwa sana na hili wala sitaki niliongelee kwa sababu namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara amelizungumzia sana leo ni zao la karafuu. Serikali ina mipango mizuri tu ya kuliendeleza zao la karafuu. Tatizo letu lilikuwepo kwenye bei. Nataka niseme Waheshimiwa Wawakilishi wanifahamu na wananchi wetu hasa wale wakulima wa karafuu.

Sisi tulitawaliwa na kumuuzia mtu wa kati karafuu. Sisi ni wakulima, mtumiaji wa karafuu yuko huku, sisi wakulima tupo huku, mtu wa kati kati ndie anayekuja kwetu kununua karafuu. Tukatawaliwa na kumuuzia mtu wa katikati karafuu, hatima yake yule ndiye aliyapata faida kubwa zaidi. Na ndio maana Mhe. Mazrui Waziri wa Viwanda na Waziri wa Kilimo Mhe. Mansour wanafanyia kazi suala la *branding*.

Naamini kazi nzuri inayofanywa sasa na Wizara ya Biashara ikishirikiana na Wizara ya Kilimo ya kufafuta mlaji wa mwisho ndiyo itakayotuletea tija na hatimaye wakulima wetu watafaidika.

Mhe. Spika, suala la maslahi ya watumishi wa umma limezungumzwa sana na waheshimiwa Wawakilishi. Nataka niseme lengo la Rais Dokta Ali Mohammed Shein la kuunda hii wizara ni kuangalia maslahi ya watumishi wa umma. Namshukuru sana Mhe. Waziri muhusika ameangalia maslahi. Namuomba Mhe. Waziri tuwe tunashirikiana kila pale hali ya uchumi itakapokuwa nzuri basi na maslahi ya watumishi wetu nayo yawe mazuri.

Mhe. Spika, wahenga wanasema mganda hajigangi. Waheshimiwa wawakilishi wamechangia sana kuhusu habari ya uimarishaji wa mapato ambayo yapo kwangu. Na wamegusia sana uvujaji wa mapato hasa katika njia zetu kuu Bandarini na *Airport.* Nataka niwahakikishie tu kwamba Kamati ya Mhe. Hamad Masoud Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano imefanya kazi zake nzuri na tutaendelea kuangalia jinsi gani ya kudhibiti mapato katika maeneo haya.

Hali kadhalika tumeshauriwa vile vile malipo yote ya kodi yapitie Benki. Nataka niseme wazo ni zuri, nimelipokea na tumeshaanza kulifanyia kazi. Kuanzia mwaka ujao wa fedha tutahakikisha kwamba kwa kiwango kikubwa malipo yanalipwa kupitia benki. Katika uimarishaji wa mapato tumeshauri vile vile kudhibiti misamaha. Hapa nataka niseme kigogo serikali ya awamu ya saba haijafuta misamaha bali tunatoa misamaha kwa ile iliyokuwa ya lazima. Misamaha iliyokuwa sio ya lazima iko nje ya sheria, iko nje ya taratibu hiyo tumesema basi.

Mhe. Spika, tumeshauri vile vile suala zima la kuangalia ruzuku. Taasisi unazozipa ruzuku maana yake tunakupa muda ili ukue halafu tuachane na wewe. Sasa kama taasisi hii miaka na miaka inapewa ruzuku tu inapewa ruzuku tu, hawa hawatajikunjua, hawatajituma hawa. Nilichokigundua katika utafiti wangu wa haraka haraka, baadhi ya taasisi wana mali nyingi sana, lakini mali zao zinaliwa na mgema.

Mhe. Abubakar Waziri wa Katiba na Sheria ni shahidi kama hili ninalolisema wao wanakodisha kwa mtu wa kati halafu mtu wa mwisho kabisa ndiye anayepata pesa nyingi zaidi. Tutakaa nazo taasisi zote hizi moja baada ya moja ili tuweze kuwasaidia kwa lengo la kuhakikisha kwamba wao wanakuwa na serikali inapata mapato. (*Makofi*)

Suala jengine ambalo limetakiwa kutolewa ufafanuzi ni suala la kufunguliwa kwa *account* ya pamoja. Waheshimiwa wengi wamesema waliochangia eneo hili wamesema kwamba tunavunja Katiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatutaka tuwe na *account* ya pamoja *joint account* ambayo mapato yake yote ya Muungano yatakwenda katika *account* hiyo.

Nataka niseme tu kwamba kikundi kazi kimemaliza kazi yake. Na ripoti ya kikundi kazi tayari imeshawasilishwa ni matarajio yangu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika muda mfupi ujao wataifungua *account* hii ya pamoja. *Account* hii fedha zake ni zile vyanzo vya Muungano. Sio mapato yote yayokusanywa na TRA Tanzania Bara. Baadhi ya sehemu si mapato ya muungano. Kwa hivyo vyanzo vya mapato kwenye *account* hii ni fedha za muungano. Utaratibu vile vile utawekwa jinsi gani ya kutumia fedha zilizokuwemo ndani ya *account* hii. Itakapokuwa tayari Mhe. Spika, tutakuja mbele ya Baraza lako tuutolee taarifa.

Mhe. Spika, jengine ambalo liliulizwa na Waheshimiwa kuhusu misaada ya kibajeti. Walitaka kupata ufafanuzi wa kina fedha hizi zilizoahidiwa vereje Zanzibar tunapata bilioni 30, fedha zilizoahidiwa zote zilikuwa ni bilioni 834. Naomba kidogo nitoe takwimu ili tuweze kufahamiana.

Mhe. Spika, ndani ya fedha hizo bilioni 834 kulikuwa kuna mikopo kutoka Benki ya Dunia bilioni 111.61,kulikuwa vile vile kuna mikopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ADB bilioni 60.57. Vile vile kulikuwa kuna mkopo kutoka Japan bilioni 27.6. Jumla ya mikopo katika hizo bilioni 834 ilikuwa ni milioni 199.78. Hii ndio mikopo.

Kulikuwa kuna fedha za misaada bilioni 473.11 na kulikuwa kuna fedha ambazo zimekwenda katika sekta moja kwa moja, bilioni 161.11. Mgawanyo wa Zanzibar wa asilimia 4.5, upo kama ifuatavyo.

Sisi tumepata kwenye mikopo asilimia 4.5 ambao asilimia 4.5 ya mikopo niliyoitaja hapo bilioni 8.99 na tumepata asilimia 4.5 ya kwenye misaada, bilioni 21.29 zote ni bilioni 30.28. Tatizo lipo wapi? Tatizo lipo katika fedha zilizokwenda kwenye sekta. Tunaendeleza mazungumzo na wenzetu. Fedha hizi zimekwenda kwenye sekta bilioni 161.11, hazikufika hapa, zimekwenda kwenye sekta. Tunaongea na wenzetu sekta zile sio za Muungano, lakini na sisi tunazo. Kama ni msaada umekwenda kwenye sekta basi na sisi sekta zile tunazo. Tumeanza mazungumzo na wenzetu, inawezekana mwaka huu ikawa tumechelewa lakini **"penye nia pana njia".** Tutafika pahala wenzetu watafahamu kwamba na sisi tulikuwa tuna haki ya kupata 4.5 katika zile zilizokwenda katika sekta.

Mhe. Spika, jengine ambalo lilozungumzwa ni suala zima la uimarishaji wa elimu. Mimi nataka niseme elimu tumeiweka kipaumbele cha pili, baada ya kuangalia changamoto tulizonazo ndani ya sekta ya elimu uhaba wa walimu hasa wa Sayansi, English, Hisabati na Kompyuta. Waheshimiwa wanataka niseme tu kwamba muda mrefu watoto wetu wameogopa masomo ya sayansi na sisi tukayawacha masomo hayo. Muda mrefu watoto wetu wameogopa Hisabati na sisi tukawacha somo hilo, leo tumejivuta katika wimbi la upungufu wa watu wa aina hii.

Mhe. Spika, tuna walimu wengi hawana ajira lakini chekecha utazame, kwenye somo la sayansi hayumo humu wengi ni *art*. Mhe. Spika, tuna kazi nyingi sana na zipo ajira nyingi sana lakini ukitazama *qualification* sayansi hamna. Mhe. Spika, wataalamu wa kilimo Waziri wa Kilimo anawahitajia pale, juzi nilikuwa nazungumza na Mhe. Rais watu wa *soil* ni wachache sana Kizimbani, wataalamu wanautazama udongo wanakuja kukwambia kwamba udongo huu unaweza ukaotesha embe, apple pia unaweza ukaotesha ndizi.

Mhe. Spika, lazima tupate vijana wetu waliosomea sayansi ili tuwapeleke wende wakasome *Soil Chemistry*, tumeshituka lakini sio kama ule msemo unaosemwa na waswahili "tumekumbuka shuka kushakucha". Mhe. Waziri wa Elimu atakapokuja kutoa hotuba yake atasema skuli 19 ziko mbioni kumalizika mwezi wa Septemba mpaka Disemba tunakabidhiwa. Mhe. Spika, skuli hizo 19 zote zina maabara, maabara ya *Chemistry, Biology, Physics na Computer.* Tena nataka niseme kwamba maabara sio majengo tu bali zina vifaa na funiture, lazima watoto wetu sasa hivi wasome sayansi.

Mhe. Spika, juzi nilikuwa ninawachokoza wenzangu hapa waheshimiwa wawili, sio vibaya kuwataja kwa sababu wenyewe wamo ndani, Mhe. Haji Omar Kheir na Mhe. Thuwayba Edington Kisassi. Tumo wengi humu ndani lakini Mhe. Thuwayba ana watoto wake wawili wanafanya *medicine* mmoja yuko China na mmoja yuko Urusi. Mhe. Haji Omar Kheir kijana wake

anampeleka na yeye kufanya *medicine* na mimi mwenyewe nina binti yangu yuko Muhimbili anafanya hivyo hivyo. Kwa kweli tuna matatizo lazima tuwapeleke vijana wetu katika sekta ambazo sisi wenyewe ndani tuna matatizo nazo ili warudi waje wasaidie wenzao. Mhe. Spika, hawa vijana mimi nina amini watarudi kuja kusaidia.

Mhe. Spika, kwa hivyo sasa hivi tukimaliza hizi skuli vijana wetu sasa wataanza kupenda sayansi. Mhe. Spika, enzi zetu kulikuwa hakuna mitandao, lakini leo kuna mitandao binti yangu huyu aliyeko Muhimbili wakati ule yuko *Form Six* alikuja siku moja akaniuliza Baba hebu nisaidie *life circle* ya nzi. Mhe. Spika, mimi nilipokuwa skuli nilikuwa napenda sayansi lakini sio *Biology*, mimi nilikuwa napenda *Physics, Chemistry* na *Mathematics*. Nikamwambia nenda kwenye internet utakuta kila kitu, basi akenda kwenye website akakaa muda wa saa moja baadae akashuka. Basi Mhe. Spika, alikuja akanisomesha mimi sasa hivi watu wanatumia mitandao tukiwahamasisha vijana wetu hawa mimi nina amini Zanzibar itabadilika.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wametaka nitoe ufafanuzi ni kwamba bajeti hii wamesema haijaonesha jinsi ya uzalishaji, wengine wamenambia wanataka kujua ni ajira ngapi zitazalishwa ndani ya bajeti hii. Mhe. Spika, kweli mimi ni mtu wa hesabu lakini ndani ya bajeti hii siwezi nikasema kwamba ajira kumi, ishirini, thalathini, elfu, elfu mbili siwezi nikathubutu kusema hivyo. Lakini nataka nikuhakikishie Mhe. Spika, na niwahakikishie wajumbe kwamba bajeti hii itazalisha ajira nyingi sana.

Mhe. Spika, kuna programu ambazo ziko za kilimo huwezi ukawa una bajeti ya kupunguza umasikini isizalishe. Kuna programu za ujenzi wa barabara hizo nazo zitazalisha ajira, kuna programu za utalii ndani ya bajeti hii zitazalisha ajira. Mimi nina imani kwamba bajeti hii kuna ajira zitakazozalishwa za muda mfupi na ajira zitakazozalishwa za kudumu. Mhe. Spika, nimemsikia Waziri wa Elimu akisema kwamba ana upungufu wa walimu katika bajeti hii nina amini kwamba ataajiri walimu, Waziri wa Afya na yeye atasema katika bajeti hii nina amini ataajiri madaktari na wauguzi, Waziri wa Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi atawawezesha wananchi waweze kujiajiri. Vile vile na Waziri wa Kilimo ataajiri mabwana shamba.

Mhe. Spika, nataka nithubutu kusema kwamba baada ya miezi sita ijayo Mwenyezi Mungu akitupa uhai na uzima mawaziri wote hawa kila mmoja alete takwimu zake aoneshe kazalisha ajira ngapi, pale tutaziona. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Makamo wa Rais tulisimamia hili ili tuje tutoe taarifa kwa Waheshimiwa Wawakilishi tumezalisha ajira ngapi ndani ya bajeti hii. Katika kipindi cha miezi sita na baadae tuje tutoe katika kipindi cha miezi tisa ijayo.

Mhe. Spika, kuna hoja ambayo imeulizwa hapa wawekezaji wa ndani hatuwasaidii, hii imepigiwa kelele sana na mifano imetolewa, kimetolewa Kiwanda cha Saruji na kiwanda vyengine. Mhe. Spika, mimi nataka niseme nia yetu ni kuwasaidia zaidi wawekezaji wa ndani, hatuna sababu ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani labda kama kulikuwa kuna matatizo kidogo yamejitokeze nathubutu kusema Mhe. Spika kwamba nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tukae pamoja ili tuweze kuona kwamba ni jinsi gani tutakavyoweza kuwasaidia wawekezaji wetu. Mhe. Spika, hili halina mjadala, kila mwekezaji kwetu sisi ni muhimu, na huyu wa ndani ni muhimu zaidi maana yake fedha zake hazitoki kwani kila atakachokizalisha huyu kitabakia hapa hapa.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wawakilishi na walitaka nilitolee ufafanuzi kidogo ni kwamba hawajaona jinsi ya kuwashirikisha Diasporas Wazanzibari walioko nje katika kujenga uchumi wa Zanzibar. Mhe. Spika, nataka niseme kwamba tunaandaa programu chini ya kitengo ambacho kilichopo chini ya Ofisi ya Rais nina imani sana Mhe. Dk. Mwinyihaji atakapokuja hapa atazieleza programu tunazoziandaa. Mhe. Spika, hawa ni wenzetu lazima na wao washiriki katika kuijenga Zanzibar yao.

Mhe. Spika, kabla sijaja hapa nimezungumza na Wazanzibari wawili wazuri sana wako Deutschewelle pale, wanasema wanatutakia kila la kheri katika kufanikisha majukumu yetu. Hawa ni Diasporas na wao mimi nina amini kabisa watatusaidia.

Mhe. Spika, jengine ambalo lilozungumziwa ni kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, hapa kulikuwa kuna maneno kidogo nitaomba niyatolee ufafanuzi. Kwanza mfuko wa JK na AK namshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Wenyeviti ametukumbusha anasema ulipaji wake unasuasua. Ni kweli wananchi wamekopeshwa lakini kiwango kilicholipwa sijui kama kinafika asilimia 50, hivyo tunaandaa utaratibu muafaka kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na mabenki tuweze kuona basi wale waliokopa wanarudisha ili tuweze kuwakopesha wengine.

Mhe. Spika, vile vile hapa yalitoka maelezo kwamba tumewakopesha watu ambao hatujawaandaa. Mimi ni imani yangu kwamba waziri anahusika ameyasikia haya atafanya maandalizi ya kutosha taarifa tulizonazo Mhe. Spika wengine wamefanyia harusi, wengine wameolea ndio mkopo huo anasema ni wa kwake. Kwa hivyo, haya yamepelekea kushindwa kulipa kwa sababu ukishakuongeza jiko hakuna tena kitakachozalishwa hapo labda watoto. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili tumelisikia na nataka nimwambie Mhe. Hamza tutamfuata atupatie hii ripoti zaidi inaonekana amelifanyia kazi vizuri zaidi kwa hiyo tutamfuate ili tuweze kufanikisha malengo yetu.

Mhe. Spika, vile vile tumepata maelezo na maelekezo kwamba tuwaelimishe vijana katika elimu ya ujasiri amali. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji amelitolea ufafanuzi hili leo asubuhi, lengo letu ni hilo na vyuo vyetu hivi vya amali vinavyojengwa vitatusaidia katika kufikia malengo.

Mhe. Spika, jengine ambalo liloulizwa waheshimiwa wametaka ufafanuzi, ni kuhusu benki zilofunguliwa Zanzibar hazijanufaisha wananchi wa Zanzibar kiuchumi. Mimi nataka niseme ni kweli lakini kuna sababu. Mhe. Spika, benki zina sababu na sababu ya kwanza ni:

Mhe. Spika, la kwanza ni kwamba tuna mabenki kumi lakini *shear* kubwa imechukuliwa na PBZ, benki hii sote sisi ni mashahidi ilikuwa kwenye matatizo. Mhe. Spika, ilipokuwa kwenye matatizo benki hii kimsingi ikazuiliwa kukopesha isipokuwa kuwakopesha wafanyakazi ambao dhamana ni mishahara yao. Lakini nataka nikubaliane na waheshimiwa kuna haja ya mabenki haya yaweze kusaidia Zanzibar tayari mimi na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Waziri Wanawake na Watoto tumeshazungumzia na *CRDB*, ili iweze kusaidia ile biashara wanayoifanya ndani na faida wanayoichuma Zanzibar irudi kwa Wazanzibari wenyewe. Mhe. Spika, nashukuru na nathubutu kusema kwamba wametufahamu tutaendelea kuyahamasisha mabenki mengine nayo vile vile yatufahamu.

Mhe. Spika, lakini riba ni kubwa kwenye benki hizo, benki zina sababu kwa nini wanaweka riba? Kwanza urejeshaji sio mzuri hata kidogo imefika pahala tumesikia kuna nyumba zinapigwa mnada zinauzwa. Kwa hivyo, kama huna dhamana ya kuweka benki atakuwekea riba kubwa sana. Lakini Mhe. Spika, AG yupo hapa mfumo wetu wa uendeshaji wa Mahakama sina haja hata kuuzungumza tunauelewa, wewe benki unaweza kumdai mtu huyo hapo namdai fedha zangu akenda yeye Mahakamani ukajikuta wewe ulokopesha umeingia kwenye matatizo.

Mhe. Spika, tunaiona mifumo yetu na tunaisikia, hivyo kwa utaratibu huu kama hatujajirekebisha katika nyanja tofauti kwa utaratibu huu mheshimiwa hii riba itakuwa haishuki. Lakini mimi nataka niwaahidi wenzangu mimi nitaendelea kuzungumza na mabenki ili kuwasaidia Wazanzibari.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa wengi ni kuhusu bei za vyakula ziko juu. Kuna wengine hapa wamependekeza serikali iondoshe kodi katika mchele, unga, sukari na mafuta ya kupikia. Mhe. Waziri wa Biashara jambo hilo ameshalitolea ufafanuzi mzuri tu asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, mimi nataka nichangie kidogo kuhusu hili ni kwamba zaidi ya asili 50 ya mfumko wa bei unachangiwa na bidhaa za vyakula. Mhe. Spika,

namshukuru sana Waziri wa Kilimo anatuonesha mwelekeo wa kujikomboa kwenye mpunga. Mhe. Spika, tatizo letu sisi Wazanzibari tena hili ni tatizo kubwa sana kwa Wazanzibari ni kwamba hatuji-*proud* kwa kitu chetu, tutazalisha huu mpunga wa nerika badala ya kusema tununue nerika tule, utataka upate basmat ya India au wa Pakistan. Mhe. Spika, hebu tujisifie na vile tunavyovizalisha huyu nerika atakuwa mkombozi katika bidhaa hizo ambazo tunaziagiza kutoka nje kwa kiwango kikubwa mchele ndio unaochukua asilimia 70. Mhe. Spika, tukiweza kujitosheleza na chakula cha mchele ndani mfumko wetu wa bei utapungua.

Mhe. Spika, nataka niwaambie waheshimiwa kwamba takwimu zinatuonesha kwamba bei za samaki nazo zimepanda. Hii kwa upande mmoja ni faraja kwa sababu wavuvi wetu wanauza samaki katika mahoteli ni bidhaa pekee ambayo mpaka sasa haiagizwi kutoka nje. Mhe. Spika, kama wavuvi wetu wanauza samaki kwenye mahoteli *purchasing power* zao na wao zitakuwa kubwa. Vile vile watakuwa na sauti sasa kuweza kupa-*gain* na *management* za hoteli, ngisi hawa nataka kiasi fulani, pweza huyu nataka kiasi fulani.

Mhe. Waziri wa Uvuvi endelea kufanya kazi vizuri kuongeza vitoe ili wavuvi pamoja na wafugaji tuna tatizo moja sasa hivi la kuku. Mhe. Spika, kuku wanaotoka Brazil wameingia katika soko la Zanzibar nilimuuliza Waziri wangu wa Uvuvi, Mheshimiwa kuku wanatoka Brazil wanauzwa Zanzibar kwa shilingi elfu tano na mia tano, lakini kuku wa hapo Kibweni naambiwa elfu kumi na tano. Mhe. Spika, lazima tutafute majibu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kabla hujamwambia kutoka Brazil asije lazima tupate jibu la ndani, nimemwambia Mhe. Waziri wa Uvuvi katika kuchangia nikamwambia nenda basi huko ukatazame wanafanya vipi yule kuku wanamzalisha vipi mpaka wanamleta hapa kwa shilingi elfu tano na mia tano. Mhe. Spika, ni bora ende aje atupe na sisi taaluma ili tujue tumetembea sana na Mhe. Rais tumekuta wafugaji wa kuku wengi tu wapo, lakini wanasikitika kuwa kuku wao hawana soko kwa sababu ya kuku wa Brazil.

Mhe. Spika, hili nalo tuliangalie inawezekana kwamba hawajitangazi, lakini vile vile inawezakana na bei zao ni kubwa. Moja wanalosema kwamba bei zao ni kubwa ni kwa sababu ya chakula na wao wananunua kwa bei kubwa. Kwa hivyo, kuna haja ya kuyaangalia haya ili tuweze kusaidiana katika suala zima la kupunguza bei za vyakula.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limeulizwa sana na hili kidogo nitapenda nilitolee ufafanuzi ili tuweze kulifahamu kwa kina sote. Mhe. Spika, tumesema katika bajeti hii tutakopa na tutakasema hatutakopa kwenye mabenki, hapa ikaja hoja nakataa kwenda kukopa kwenye benki nataka kukopa pesa za

wafanyabiashara na mfanyabiashara gani huyo mwenye pesa zote hizo, faida yake nini tunapata. Mhe. Spika, kidogo naomba nitoe ufafanuzi kwa faida yetu sote.

Mhe. Spika, kina kitu kinaitwa hisa, naomba ni *declare interest* Mhe. Spika mimi nina hisa kwenye Twiga Cement, nina hisa katika Benki ya NMB pesa zangu mimi na wenzangu wote waliokuwa na hisa katika maeneo mbali mbali wengine wana hisa katika Swissport, wengine wana hisa katika bia. Mhe. Spika, pesa hizi zote ndio pesa ambazo ziko kwenye soko tuna uwezo wa kwenda kukopa kwenye soko la hisa.

Dhamana ni Benki ya Tanzania, uzuri wake nini? Mhe. Spika, uzuri ni kwamba hata haya mabenki unayosema tukakope na wao wanakopa huko wakitaka kufanya biashara zao na wao wanakwenda kukopa huko. Kwa nini wanakwenda kukopa huko? Kwa sababu kule riba ndogo, riba ni kati ya asilimia 7 mpaka 8. Hayo mabenki mnayoyaona yanakwenda yanakopa kule pesa ndio inakuja huku halafu wanatukopesha sisi kwa asilimia 18 mpaka 24.

Mhe. Spika, awamu ya saba tumesema tutakopa huko na sisi kwenye riba ndogo, huku kwenye riba kubwa hatuwezi tukawabebesha mzigo wananchi wetu. Lakini vile vile tukasema kuna *guarantor ready made guarantor BoT* hata ukifanya nini benki hii ndio *guarantor,* tukasema kwamba sifa hizi na sisi ndio tunakwenda huko.

Mhe. Spika, sisi kama serikali unapokwenda ukakopa katika benki za biashara maana yake wewe unashindana na public, unashindana na wananchi, unashindana na wafanyabiashara. Sisi tumesema tukakope huko ili hizi benki tuwaachie wafanyabiashara wetu na wananchi wetu na wao wakope. Mhe. Spika, hilo ndio lengo letu hasa la kusema tunataka kwenda kukopa kwenye fedha hizo na hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanakopa huko huko. Mhe. Spika, hii inasaidia sana kufanya mabenki yenu haya kuwa na pesa za kutosha kwa ajili ya kuwakopesha wananchi.

Kwa hivyo, ndio lengo letu sio zile pesa kwamba ni za mtu kama Kombo, Faki ata sio hivyo, pesa zile zetu ziko pale zinafanya biashara na sisi tunapata. Hata hii mifuko inaruhusiwa kwenda kukopa hapo, ZSSF wakitaka wanaruhusiwa kwenda kukopa hapo na dhamana ni BoT. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimeona nalo hili vile vile nilitolee ufafanuzi ili kila mmoja wetu aweze kulifahamu.

Mhe. Spika, mafuta ni suala la uchumi na masuala ya uchumi si masuala ya Muungano. Kwa hivyo, hoja ya Baraza la Mapinduzi na hoja ya Baraza la Wawakilishi kwamba mafuta yatolewe ni sahihi.

Lakini Mhe. Spika, nataka kidogo niwarudishe Waheshimiwa kwenye *hansard*, kwa vile hati zake ni ndogo ngojea nivae miwani niisome. Mhe. Spika, kikao kilichofanyika tarehe 8/4/2009 kilitoa maadhimio na *hansard* yake ni hii hapa. Naomba nisome kidogo tulichokubaliana wawakilishi, pendekezo la kwanza.

"Hoja imetolewa, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na pendekezo la kwanza kuhusu ardhi ya bahari na ndani ya Zanzibar kwamba suala la mafuta liwe katika mikono ya Zanzibar wainue mikono".

Mhe. Spika, hii ilikuwa ni wakati huo, Mhe. Haji Omar Kheir kapatia anasema hii ni ya wakati huo. Hii ilikuwa ni ya wakati huo, lakini sasa hebu tuangalie naona Waheshimiwa Wajumbe wote wameunga mkono pendekezo hili. Hii ni *hansard* si maneno yangu nasoma *hansard* Mhe. Spika.

Pendekezo la pili, "Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wanaokubali pendekezo la kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba sasa wakati umefika kuunda chombo chake cha kusimamia utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesiwanyanyue mikono".

Kilichojitokeza wakati huo Mhe. Spika, naona Waheshimiwa wote waliokuwepo wanakubali. (*Makofi*).

Mhe. Spika, haya ndio mapendekezo ambayo tumekubaliana Baraza la Wawakilishi. Labda nitoe tafsiri kidogo ya mapendekezo haya. Mapendekezo haya kwa tafsiri fupi tumekubali kulitoa katika Muungano, kwa tafsiri fupi ndio kuyatoa mafuta katika Muungano.

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba, hakuna aliyetuzuia kuchimba mafuta Zanzibar, tatizo liko moja tu, tukisema leo tuchimbe, kuna dada yangu mmoja jana alisema kama ni masururu basi tuje na masururu yetu tuanze kuchimba, tukisema leo tuchimbe mafuta Zanzibar hakuna atakayetuzuia. Sisi wenyewe tumezuia kwa sababu tukichimba tutachimba kwa kutumia sheria ya Muungano, wameshakuja wawekezaji wengi wanaotaka kuchimba kwenye sekta ya mafuta, wengine wamemuona Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati wengine wameniona mimi, wengine wamemuona Mhe. Mansour Yussuf Himid wakati ule Waziri wa Maji, Ujenzi, Nisharai na Ardhi na wengine wamemuona Mhe. Rais aliyestaafu na wengine wameshamuona Mhe. Rais wa sasa Dkt. Ali Moh'd Shein.

Sheli ya Uingereza imekuja, Mrusi amekuja, Brazil amekuja, wengi tu wanataka kuchimba na Zanzibar tuna *block* nne ambazo zinaonesha kwamba maeneo ya mafuta, lakini tukichimba leo tukiseme sasa hivi watachimba kwa kutumia sheria ya Muungano. Vyombo hivi au wawekezaji hawa watapewa

leseni kupitia sheria ile ya Muungano, ndio tukasema hapa ni kuku na yai, kipi kianze mwanzo. Tuchmbe kwa sheria ya Muungano tuje tufike pahala tuanze sasa kujadili au tusubiri tujadili tuyatoe halafu tuje tuchimbe, lakini hakuna aliyetuzuia kuchimba.

Sasa hivi Baraza hili Mhe. Spika, likiamua tuchimbe Mhe. Waziri wa Nishati ataleta hoja yake serikalini lakini *consequence* zake ni kwamba tutachimba kwa kutumia sheria ya Muungano.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu baadhi ya Wajumbe walisema kwamba tutakaa miaka mitatu tukisubiri kulitoa katika Muungano mpaka katiba mpya ianze, inahitaji *good will*, tukiamua kulitoa Bunge lijalo wataitoa. Wenzetu wa Tanzania Bara na sisi Zanzibar kinachohitajika ni two third ya Wabunge kutoka Zanzibar na *two third* ya Wabunge kutoka Bara wakubali.

Kwa muono wangu si tatizo kubwa hata kidogo inahitajika *goodwill* tu, *the understand after all* tumejipa matumaini makubwa mafuta tunayo, lakini uthibitisho zaidi tutauona baada ya kuanza kuchimba.

Kenya walikuwa wana matumaini makubwa na katika eneo lao la kwanza lililowapa matumaini kuliko hata Uganda, kuanza kuchimba shimo la kwanza tu ambalo limewapa matumaini makubwa wakagundua hawana kitu, wakasema basi wakafunika hawaendelei tena. Kwa hivyo, uthibitisho tutaupata baada ya kuchimba, tunaweza leo tukaona mafuta juu yanaelea kwenye maji, unaweza ukapita ukasikia harufu ya petroli, pengine jamaa tu gari lake bovu pale limeharibika kamwaga petroli wewe ukafikiria ndio petroli yenyewe ile. Nathubutu kusema kwamba tutapata uthibitisho tukianza kuchimba.

Waheshimiwa Wajumbe mimi niliyepewa dhamana ya fedha nataka jana tuchimbe mafuta sio leo, kama kuchimba nataka jana tuchimbe sio leo, lakini tunachimba kwa sheria gani? Tutalazimika kufuata sheria ile ya Muungano, tukiamua tuchimbe kwa sheria ile tuendeleeni, tukiamua tuanze kuyatoa kwanza tu-*push* zaidi kama *speed* ya ku-*push* tunaona ni ndogo tuiongeze mara mbili tuiongezeni zaidi ili tulitoe na baadae tuweze kuchimba.

Mimi nasema ni *goodwill* tu, kwa ninavyomuona Dkt Ali Moh'd Shein na Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, *I beleive green light* inaweza kuonekana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilisema niwarudishe wenzangu katika *hansard* ili tuweze kufanya maamuzi ya pamoja. Nini tunataka katika mafuta? Tuchimbe kwa kutumia sheria ya Muungano au tuanze kulitoa kwanza baadae tuchimbe? Wachimbaji wapo.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba tuna kila sababu ya Wazanzibari sasa kubadilika, tusiseme sana lakini tutendeni sana. tumepoteza miaka madhaa kugombana wenyewe kwa wenyewe Wazanzibari. Wazanzibari walio wengi wamechuma halafu Wazanzibari wenzao wameenda kuwatilia moto wamerudisha umasikini kwa pande zote. Leo amani imepatikana hatuna sababu kwa nini Wazanzibari tusiendelee, leo umoja umepatikana namshukuru sana Dkt. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif. *(Makofi)*

Mhe. Spika, muda mrefu tulikuwa tunatafuta kitu hiki Wazanzibari kukaa pamoja tukajenga nchi yetu badala ya kulumbana, tumepoteza muda miaka zaidi ya kumi tumeipoteza, lakini wanawahenga wanasema, "kama umeshindwa kufanya jana, leo ipo fanya leo ili kesho uone matunda". Mhe. Spika, *it can be done play your part.*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sasa naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutoa majumuisho na majibu kwa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa katika uchangiaji. Kiutaratibu na leo nimeamua kwa sababu hili bango linanizuia nisione vizuri, kiutaratibu tuna hoji kwa ujumla, kama linatokea tatizo tunakwenda kwenye hatua nyengine ama ya kuita majina au kuhesabu *whatever*, lakini tunahoji kwa ujumla na kukiwa na tatizo basi hoja inaweza ikatolewa na mjumbe yeyote kwamba mimi naomba tutoe hoja kwamba tuhesabu kura au tuite majina vyovyote vile itavyofikia.

Kwa hivyo, baada ya majumuisho ya Mhe. Waziri wa Fedha Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na Bajeti hii ya Serikali iliyowasilishwa na kutolewa majibu hivi punde wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepitishwa rasmi na Baraza hili. Naomba kuchukua nafasi hii tena kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, pia kuwashukuru sana kwa kuanzia na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri wote, Manaibu wao pamoja na Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kauli moja na kwa umoja wetu kupitisha Bajeti ya Serikali.

Tulifahamishwa mapema kwamba hakuna ongezeko la kodi kwa hivyo, haja ya kuleta mswada wa *Finance Bill* haipo, vyenginevyo baada ya kazi hii ilikuwa kazi nyengine kwanza tupitishe *Finance Bill* ili wakusanyaji kodi waweze kukusanya kodi kwa sheria mpya. Lakini kwa kuwa hakuna ongezeko la kodi yoyote basi sheria iliyopo ndio itayofanya kazi ya kukusanya kodi kuanzia Julai

na hivi tunaendelea na ukusanyaji wa kodi kwa mujibu wa sheria ile ambayo ilikuwa imepitishwa mapema.

Kwa hivyo, kwa leo itakuwa tumemaliza shughuli zetu nafikiri hakuna jambo jengine. Kwa kuwa shughuli zote zimekamilika zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya kikao cha leo, sasa nichukue nafasi hii kuahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 23/06/2011 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 6:44 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23/6/2011 saa 3:00 asubuhi)